# Nipashe

Jumatano Septemba 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581082

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS. 1,034,905,195

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Mlinzi** anyongwa lindoni, mchele kilo 500 waibwa

UKURASA 3



LULU AMSIFIA ZUCHU KWA UZURI WA ASILI

UKURASA 27



# Panga lapita vigogo CCM

• **Yachukua** uamuzi mgumu, uchaguzi UVCCM, UWT wafutwa... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MWENYEKITI KIJIJI ASIMULIA MAUAJI YA WATUHUMIWA WA UJAMBAZI

SIKU tano baada ya mauaji ya watu watatu wanaodaiwa kuuawa na Jeshi la Polisi wilayani Serengeti mkoani Mara...

UKURASA WA 23

### KESI ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR ZAWAPONZA

KESI 14 za udhalilishaji zinazohusu makosa ya kutorosha, kubaka na kuingilia kinyume cha maumbile...

## Masharti 7 ufadhili wa Samia haya hapa

UKURASA 3



Askari kanzu wakimbeba mmoja wa vijana waliojeruhiwa kwa kipigo kutoka kwa wananchi, baada ya kutuhumiwa kuvamia na kumjeruhi mfanyakazi wa ofisi ya kampuni ya michezo ya kubahatisha eneo la Mwenge, Dar es Salaam jana. **Picha ndogo:** Kijana mwingine akiwa hoi mtaroni baada ya kipigo. **PICHA: MAULID MMBAGA**



# Watuhumiwa 'panya road' wanusurika kifo kwa kipigo

UKURASA 2

**MICHEZO** CEO AIPA JEURI YANGA KUITOA AL HILAL UK.32 **KABWELA** UK.7



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na mkewe Mary Majaliwa (wa pili kushoto), wakiweka maua wakati wa mazishi ya kitaifa ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, yaliyofanyika jijini Tokyo, Japan jana. Kushoto ni mke wa Balozi wa Tanzania nchini Japan, Consolata Luvanda na (kulia) ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk. **PICHA: OWM**

# Panga lapita vigogo CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeanza kuchukua hatua kwa wanachama wake wanaokiuka maadili kwenye uchaguzi uliofanyika kwa ngazi mbalimbali za jumuiya ikiwamo kufuta baadhi ya matokeo ya uchaguzi kutokana na dosari zilizojitokeza.

Mbali na kufuta uchaguzi katika wilaya za kichama kwa ngazi za jumuiya zake, taarifa kutoka ndani ya chama hicho zinasema baadhi ya wenyeviti wa CCM Wilaya wameenguliwa katika kinyag'anyiro kitakachofanyika mwishoni mwa mwaka huu kutokana na sababu mbalimbali.

Licha ya kuchukua uamuzi huo, CCM imeonya na kusisitiza kufuatilia kwa karibu wagombea wote wanaotoa rushwa na kukiuka kanuni za uchaguzi, ikiwamo kupanga safu za uongozi, ili wachukuliwe hatua.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, aliyasema hayo jana jijini hapa alipotoa taarifa ya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya wenyeviti ngazi ya wilaya za kichama 168.

Awali, waandishi wetu waliokuwa wakifuatilia orodha ya wagombea walioptishwa, wakiwamo wa nafasi ya uenyekiti ngazi ya wilaya, waliahidiwa ingetolewa jana lakini hadi tunakwenda mitamboni ilikuwa haijapatikana.

"Maofisa wa chama wanafanya uhakiki wa majina yaliyopitishwa ili kutokufanya makosa na kuwatangaza ambao hawakupitishwa, hivyo kuwapa nafasi isivyostahili," ofisa mmoja (jina linahifadhiwa), alikaririwa akisema.

Shaka alisema NEC imeelekeza kuhakikisha haki inasimamiwa na kulinda maadili ya uongozi kwa kukemea vikali vitendo vya rushwa katika uchaguzi wa ngazi mbalimbali ndani ya chama, akiweka wazi kuwa kuna uchaguzi umefutwa kwa jumuiya za Umoja wa Vijana (UVCCM) na Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT).

Alisema hadi kufikia juzi, uchaguzi katika maeneo matano ya UVCCM ulifutwa huku UWT wakisimamishwa kufanya uchaguzi katika maeneo matatu kutokana na dosari.

Alisema malalamiko mengine yanaendelea kufuatiliwa.



"Kuna uchaguzi umefanyika tunaendelea kujiridhisha kutokana na malalamiko, CCM kwa mujibu wa kanuni tutasikiliza na itakapobainika kanuni na taratibu zimevunjwa, hatua zitachukuliwa ikiwamo kutengua na kufuta uchaguzi," alisema.

Aliwataka wanachama kuheshimu kanuni ili kupata viongozi walio bora wa kukitumikia chama hiko.

"Chama kinafuatilia kwa karibu sana mwenendo wa uchaguzi ngazi zote, niwahakikishie wana CCM kila ambapo haki imepinda, basi haki itatendeka," alisema.

Alisema wagombea hao ngazi ya wilaya uchaguzi wao utafanyika Oktoba Mosi hadi 2 mwaka huu.

"Jicho la chama linafuatilia kwa karibu sana kila hatua zinazoendelea kwenye uchaguzi huu, yeyote atakayebainika kwenda kinyume cha taratibu za uchaguzi unaoendelea kufanyika kuanzia ngazi ya wilaya tutachukua hatua kwa kuwa eneo hili ni matumizi mabaya ya madaraka," alisema.

Shaka alisema lengo ni kuimarisha msingi wa CCM na kupata viongozi bora na siyo bora viongozi.

Kuhusu kuongeza muda nafasi ya NEC, Shaka alisema "Halmashauri Kuu imeongeza muda wa kuchukua na kurejesha fomu kwa nafasi za ujumbe wa NEC kwenye ngazi za mikoa na taifa, ambapo sasa ni kuanzia Oktoba Mosi hadi 5 mwaka huu."

Alisema zaidi ya wanachama milioni mbili wamejitokeza kuomba kuteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi ya shina hadi taifa.

"Chama chetu tumepanua wigo ili kutoa nafasi zaidi kwa wale wenye sifa kuomba nafasi hizo, mchujo wa nafasi za taifa utakuwa mwezi Novemba mwaka huu," alibainisha.

# Watuhumiwa 'panya road' wanusurika kifo kwa kipigo

**Na Maulid Mmbaga**

VIJANA wawili wanaodhaniwa kuwa sehemu ya kundi la wahalifu wa mitaani, maarufu panya road, wamenusurika kifo baada ya kupokea kipigo kutoka kwa wananchi wenye hasira wilayani Kinondoni mkoani Dar es Salaam jana.

Kipigo hicho kilichohusisha matumizi ya mawe na silaha nyingine za jadi, kiliwakumba vijana hao walipodaiwa kumjeruhi kwa kisu mfanyakazi wa kike aliyekuwa kwenye ofisi ya kampuni ya michezo ya kubahatisha ya PremierBet iliyoko Mwenge.

Baada ya wananchi kupata taarifa za tukio la kujeruhiwa kwa mfanyakazi huyo wa PremierBet, vijana hao walizungukwa na wananchi na kuanza kupigwa mawe, mengi yakielekezwa kichwani, mmoja akitumbukia mtaroni na mwingine barabarani.

Licha ya kudondoka chini, Nipashe ilishuhudia wananchi wakiendelea kuwashushia kipigo vijana hao, baadhi wakiwaponda miguu na magoti kwa kutumia mawe.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo lililotokea majira ya saa tatu asubuhi, walidai kuwa vijana hao walikuwa watatu na baada ya wananchi kuwashtukia, wawili walikabiliwa na mmoja wao alikimbia.

Mmoja wa mashuhuda hao, Rashidi Abrahamu aliiambia Nipashe kuwa vijana hao walipofika kwenye duka hilo, waliingia ndani kama wateja na walimkuta mfanyakazi huyo na kumtishia kwa kisu huku wakimtaka atoe fedha.

Alisema dada huyo alikurupuka na kutaka kukimbilia nje ya duka hilo huku akipiga kelele ya mwizi ndipo mmoja kati ya vijana hao alipomjeruhi.

"Watu waliposikia kelele walikwenda haraka kwenye duka na waliwakuta huku mmoja akiwa ameshika kisu, mmoja alifanikiwa kukimbia lakini wawili walipigwa sana. Baadaye askari (polisi) walifika, ni asubuhi lakini watu wanafanya uhalifu huu, hii hali siyo nzuri," Abrahamu alilalamika.

Zaituni Kiango ambaye ni mmoja wa wanaofanya biashara jirani na eneo lilikotokea tukio hilo, alisema dada aliyejeruhiwa alikimbizwa hospitalini, huku akishauri serikali kutowaachia wahalifu kama hao wanapokamatwa kwa kuwa kuwaachia, kunahatarisha usalama wa watu.

"Watu kama hawa siyo wa kuwaachia, kila siku wapo, hali siyo nzuri, hii inatishia amani, saa tatu asubuhi watu wanafanya mambo kama haya, serikali ifanye kazi yake, watu kama hawa siyo wa kuwaachia, wanafanya tukio baada ya muda unawaona tena mtaani wanafanya tena uhalifu, hao ni wakuwafunga tu," alisisitiza Zaituni.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro (pichani) alikiri jeshi hilo kuwashikilia watuhumiwa hao na walikuwa chini ya uangalizi wa madaktari, huku akiahidi kutoa taarifa kamili ya tukio hilo leo.



HABARI KITAIFA

# Vigezo vya kupata ufadhili mpango wa Samia vyatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza vigezo saba kwa wanafunzi 640, watakaopata ufadhili kupitia 'Samia Scholarship' ikiwamo wastani wa ufaulu wa alama 3.8 (GPA) kwa mwaka wa masomo.

Wanafunzi hao ni wale waliopata ufaulu wa juu kwenye masomo ya sayansi na kwamba atakayepata kiwango cha chini atasitishiwa ufadhili mwaka wa masomo unaofuata.

Wanafunzi watakaopata ufadhili huo ni waliopata ufaulu wa juu kwenye mitihani ya kidato cha sita mwaka huu iliyoendeshwa na Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), kwa tahasusi za sayansi zikiwamo Fizikia, Kemia na Baiolojia (PCB), Fizikia, Kemia na Hisabati (PCM), na Fizikia, Jiografia na Hisabati (PGM).

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo jana jijini hapo huku akibainisha kuwa maombi hayo yataanza kuwasilishwa leo kwa njia ya mtandao ndani ya siku 14 kupitia tovuti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

"Samia Scholarship itagharamia kwa asilimia 100 masomo ya chuo kikuu kwa wanafunzi ambao wamepata udahili kwa fani za teknolojia, uhandisi, hisabati na tiba," alisema.

Alisema, wanafunzi watakaofadhiliwa, watagharamiwa kati ya miaka mitatu na mitano kulingana na programu husika walizodahiliwa.

Prof. Mkenda, alitaja masharti ya ufadhili kuwa ni kusoma, kuelewa na kutia saini mkataba wa makubaliano ya ufadhili wa masomo kati yake na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"Anapaswa kuwa na akaunti ya benki kwa ajili ya fedha atakazolipwa moja kwa moja. Mnufaika hataruhusiwa kubadilisha programu ya masomo aliyopatia ufadhili bila barua ya idhini ya maandishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia," alisema.

Masharti mengine ni mnufaika kutoruhusiwa kuahirisha masomo isipokuwa kwa sababu za kiafya na kuthibitishwa na chuo husika na ikiwa mnufaika atagahiri fursa ya ufadhili kabla ya kuanza masomo, atapaswa kuwasilisha taarifa ya maandishi kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"Iwapo kiwango cha ufaulu wa mnufaika kitashuka chini ya GPA 3.8 katika mwaka wa masomo, ufadhili utasitishwa, mnufaika anapaswa kujisajili katika Mfumo wa Usimamizi wa Wanafunzi unaopatikana kupitia https://scholarships.moe.go.tz/,"alisema.

Alitaja sifa za kupata ufadhili huo kuwa ni kuwa Mtanzania, ufaulu wa juu wa tahasusi za sayansi, kupata udahili katika programu za sayansi, teknolojia, uhandisi, hisabati au tiba katika chuo kikuu nchini kinachotambuliwa na serikali ambazo zimetajwa katika kundi la kwanza kwenye mwongozo wa utoaji mikopo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa mwaka 2022/2023 na awe ameomba ufadhili kwa usahihi kwa njia iliyoelekezwa.

"Ufadhili utazingatia viwango na miongozo ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kugharamia ada ya mafunzo, posho ya chakula na malazi, posho ya vitabu na viandikwa, mahitaji maalum ya vitivo, mafunzo kwa vitendo, utafiti, vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na bima ya afya," alisema.

Alisema, uchambuzi wa wanufaika umezingatia uwiano wa kijinsia ambapo wasichana ni 244 na wavulana ni 396 huku shule zilizotia fora kwa kuwa na idadi kubwa ya wanufaika ni pamoja na Tabora Wavulana, St.Mary's Mazinde Juu, Kisimili, Mzumbe, na Tabora Wasichana.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein, alisema Sh. bilioni tatu zitatumika kwa ajili ya wanafunzi hao kwa mwaka 2022/23.

Alisema, ufadhili huo utaongeza hamasa kwa wanafunzi na idadi ya wanufaika itaongezeka zaidi.

## Mlinzi anyongwa lindoni, mchele kilo 500 waibwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MLINZI wa Kampuni ya Ndelumo Security, Geofrey Justine (45) ameuawa kwa kunyongwa na watu wasiojulikana katika Kata ya Didia wilayani Shinyanga akiwa kwenye eneo lake la ulinzi katika mashine ya Richard Mwagi huku waliotekeleza mauaji hayo wakidaiwa kuiba kilo 500 za mchele.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Didia wilayani Shinyanga, Mrisho Hamadi alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya simu huku akisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Septemba 24, mwaka huu.

Alisema watu hao walimvamia mlinzi huyo kwa kumvizia na kisha kuanza kumshambulia na kumnyonga shingo na kusababisha kifo chake.

"Mwili wa marehemu tumeukuta na majeraha katika kichwa chake huku akitokwa na damu mdomoni. Katika mashine ambayo alikuwa akilinda, tumekuta kumefanyika wizi wa kilo 500 za mchele wenye thamani ya Sh. milioni 1.2," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema mlinzi aliyeuawa alikuwa mkazi wa wilayani Karagwe mkoani Kagera na alikwenda kijijini huko kwa ajili ya kutafuta riziki na kupata kazi ya ulinzi katika mashine hiyo.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa mlinzi huyo alivamiwa na watu wasiofahamika ambao pia waliiba kilo 500 za mchele katika mashine hiyo.

"Ni kweli tukio hilo limetokea katika Kata ya Didia wilayani Shinyanga na watuhumiwa wa tukio hilo tunawatafuta," Kamanda Janeth alithibitisha.




**HABARI KITAIFA**

# Kizimbani kwa mashtaka ya kumzushia kifo Mwakyembe

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza imemhukumu kifungo cha maisha jela Alphonce Ngassa, maarufu kama Dutwa (51) kwa kumnajisi mtoto wake wa kike mwenye miaka tisa (jina limehifadhiwa).

Mshtakiwa huyo alihukumiwa kifungo hicho baada ya kutiwa hatiani kwa kumweka binti yake katika nyumba ya kulala wageni na kumfanyia vitendo hivyo mwezi mzima huku akimziba mdomo asipige kelele.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Mwandamizi Juma Mpuya, alisema mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo mwishoni mwa mwaka jana.

Hakimu Mpuya alisema mashahidi sita, akiwamo mtoto aliyefanyiwa kitendo hicho, walitoa ushahidi katika mahakama hiyo.

Kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo, alisema mahakama imejiridhisha pasipo kuacha shaka kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo, hivyo kumtia hatiani.

Mahakama hiyo ilielezwa kuwa, mshtakiwa huyo alimchukua binti yake huyo kutoka Kahama mkoani Shinyanga alikokuwa anaishi na mama yake mzazi ambaye walitengana na kwenda naye Jijini Mwanza kwa ahadi ya kwenda kumnunulia viatu vya kanisani.

Aidha, ilidaiwa kuwa ahadi hiyo haikutekelezwa na mshtakiwa badala yake alimpeleka kwenye nyumba hiyo ya kulala wageni na kuanza kumfanyia vitendo hivyo.

Taarifa za mtoto huyo kufanyiwa unyama huo zilitolewa na mtu aliyejulikana kwa jina la Minja, ambaye alibaini mwenendo wa mtoto huyo haukuwa sawa na kuanza kumdadisi ndipo akamwambia kuwa baba yake mzazi alikuwa akimfanyia vitendo hivyo.

Minja alidai katika mahojiano, mtoto huyo alikiri kufanyiwa vitendo hivyo, huku akidai baba yake alikuwa akimziba mdomo wakati akimnajisi ili asipige kelele.

Kutokana na hali hiyo, Minja alimpeleka mtoto huyo kituo cha polisi na kufungua kesi namba 162 ya mwaka 2021 ya ubakaji na kupewa fomu namba 3 ya polisi kisha akampeleka hospitalini.

Majibu ya daktari aliyemfanyia vipimo yalionyesha kuwa binti huyo aliingiliwa mara nyingi na sehemu zake za siri zilikuwa katika hali mbaya.

Daktari aliyempima alitoa ushahidi wake mahakamani hapo ikiwamo kuwasilisha fomu hiyo namba tatu ya polisi kama kielelezo.

Baada ya mahakama kujiridhisha na ushahidi wote uliotolewa na mashahidi sita akiwamo mtoto mwenyewe, ilitoa nafasi kwa mshtakiwa kujitetea kutokana na shtaka linalomkabili, lakini alikataa kujitetea.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Ghati Mathayo, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa kutokana na kufanya kitendo kibaya dhidi ya mtoto wake wa kumzaa ambaye ni mdogo na kumharibu sehemu zake za siri, na kumharibu kisaikolojia kwa kumnajisi mwezi mzima.

Kutokana na ushahidi pamoja na maelezo ya mwendesha mashtaka, mahakama ilimhukumu kifungo cha maisha jela.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (katikati), akikata utepe kufungua mafunzo ya mwongozo wa taarifa wa utambuzi wa mapema na afua stahiki kwa watoto wenye ulemavu kwa maofisa ustawi na maendeleo ya jamii kutoka Tanzania Bara, jijini Dodoma jana. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi Huduma za Jamii Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Amina Mfaki na Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Festo Fute. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mwenyekiti kijiji asimulia mauaji watuhumiwa ujambazi yalivyokuwa

**Na Said Muhibu,** SAUT

SIKU tano baada ya mauaji ya watu watatu wanaodaiwa kuuawa na Jeshi la Polisi wilayani Serengeti mkoani Mara, mwenyekiti wa kijiji cha Nyamehuru wilayani humo, David Chacha Mgendi, amesimulia mkasa mzima.

Mgendi akizungumza na waandishi wa habari juzi alisema Septemba 21, mwaka huu walifika kijijini kwake askari polisi wakiwa na magari matatu na kumkamata Simon Mwise na Antony Machota kwa madai kuwa walikuwa ni majambazi.

Mgendi alisema baada ya kuwakamata watu hao, waliondoka nao hadi kituo cha polisi cha Majimoto wilayani Serengeti.

Alisema kabla ya kuwakamata watu hao wanakijiji walipiga yowe ili wajikusanye kwa ajili ya kujua kulikuwa na tukio gani nyumbani kwa Mwise na kwamba baada ya wanakijiji kujikusanya, walibaini kulikuwa na askari waliofika kijijini kwao hawakufanya chochote na kwamba walishuhudia ndugu zao wakiondoka na polisi wakiwa wazima.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa alipiga simu kwa mkuu wa kituo cha polisi cha Majimoto kutaka kujua kama hao askari walikuwa wametumwa kijijini hapo na kujibiwa kuwa kulikuwa na oparesheni.

Pia alisema baada ya kupata majibu hayo, aliwapigia simu ndugu wa marehemu ili kuwapa taarifa hiyo na walikwenda kituoni na kumkuta Mwise akiwa mzima.

Septemba 22, alisema walisikia milio ya risasi usiku na kulipokucha walikwenda eneo la tukio na kukuta damu nyingi na walipofuatilia waliambiwa Mwise mwili wake ulikuwa chumba cha maiti.

# Hakuna atakayelazimishwa kuwa na bima afya - Waziri

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema hakuna Mtanzania ambaye atakamatwa, kufungwa wala kulipishwa faini kwa kutokuwa na kitambulisho cha bima ya afya.

Alitoa ufafanuzi huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam kuhusu Bima ya Afya kwa Wote ambayo muswada wake tayari umeshawasilishwa bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza.

Akifafanua kuhusu mapendekezo yao ndani ya muswada huo, Waziri Ummy alisema serikali ilianza maandalizi mwaka 2012 ya kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ili wananchi wapate huduma bora.

"Hakuna Mtanzania atakamatwa, atafungwa, atalipishwa faini kwa kutokuwa na bima ya afya, hakuna hicho kifungu. Lakini tunawapataje Watanzania ambao hawaumwi wajiunge na bima ya afya? Ndiyo maana tumependekeza kuifungamanisha na baadhi ya huduma," alisema.

Ummy alisema ili watu waingie ni lazima waifungamanishe na baadhi ya huduma ndiyo maana wamepeleka mapendekezo bungeni ili kutungwe sheria.

Alisema kilio cha wananchi ni gharama kubwa za matibabu ambazo hawazimudu na kilichothibitika kitaifa na kimataifa ili wamudu ni kulipa kabla ya kuugua.

"Haitakuwa kwamba wote wajiunge na NHIF (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya), hapana! Utachagua mwenyewe kama ilivyo kwa bima ya gari," alisema.

Ummy alisema katika muswada huo wanapendekeza kuweka kitita cha mafao chenye usawa ambacho kila mwananchi anayetaka kujiunga na bima ya afya atakipata.

Alisema: "Kitita cha msingi ni kipi? Tutasema kumwona daktari ni lazima, kupata vipimo tutaweka vipimo basic (msingi) labda mara moja kwa kila familia. Tutakuja na viwango mbalimbali mtu atajipimia, tunataka tu kile cha msingi uwe nacho angalau umwone daktari ufanye vipimo muhimu vya maabara, radiology (x-ray mashine, CT-Scan, Ultra Sound).

"Mwananchi atapima, nichangie hivyo vitatu ili nikipata tatizo lolote nitapata CT-Scan ambayo kupima kwa sasa ni Sh. 200,000, tutaweka nguvu kubwa kwenye elimu, tuwaelimishe na kuhamasisha umuhimu wa kuwa na bima ya afya."

Waziri Ummy alisema sheria ikipita bungeni, watakwenda hatua kwa hatua na wasio na uwezo watatambuliwa kwa mujibu wa mpango au mfumo kwa wasio na uwezo ambapo wanaweza kutumia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Alisema kipaumbele cha serikali ni watu waingie kupitia kaya kwa kuwa hawawezi kuumwa wote kwa wakati mmoja lakini kutakuwa na utaratibu wa kulipa mtu mmoja mmoja.

Alisema endapo muswada utapita bungeni, utekelezaji wake utaanza Julai Mosi, 2023.

Kuhusu mgonjwa mmoja kwa siku kwenda hospitali mpaka tatu, Waziri Ummy alisema kupitia bima ya afya kwa wote, wataweka utaratibu mzuri.

Alisema kwa sasa pamoja na kuwa na idadi nzuri ya watumishi wa afya, vifaa tiba na dawa, kuna kero mbili ambazo ni ubora wa huduma na wananchi kugharamia huduma za afya kwa sababu matibabu ni gharama.

Waziri Ummy alisema kwenye ugharamiaji wa huduma za afya, kwa mwaka 2019 matumizi ya malipo ya papo kwa hapo, kwa kaya moja ya watu sita yalikuwa Sh. 560,000, sawa na Sh. trilioni 1.7 kwa mwaka.

TANGAZO

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISRTATION AND LOCAL GOVERNMENT
## MLELE DISTRICT COUNCIL

# MLELE DISTRICT COUNCIL FINANCIAL STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2021

| | Notes | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 23 | 1,172,659 | 1,276,590 |
| Receivables and prepayments | 24 | 575,092 | 465,665 |
| Inventories | 25 | 82,450 | 101,399 |
| | | 1,830,201 | 1,843,654 |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 26 | 7,064 | 7,064 |
| Property, plant and equipment | 29 | 13,294,191 | 10,506,588 |
| | | 13,301,255 | 10,513,652 |
| **TOTAL ASSETS** | | 15,131,455 | 12,357,306 |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Deferred income | 11 | 166,879 | 23,560 |
| Payables | 34 | 311,768 | 498,483 |
| Employee benefits | 37 | 834,462 | 967,908 |
| Provisions | 38 | - | - |
| | | 1,313,109 | 1,489,951 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Deferred income | 40 | 819,295 | 995,125 |
| | | 819,295 | 995,125 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 2,132,404 | 2,485,076 |
| **NET ASSETS** | | 12,999,050 | 9,872,230 |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated surplus/(deficit) | | 12,984,922 | 9,858,102 |
| MCR | | 14,128 | 14,128 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | 12,999,050 | 9,872,230 |

The Financial Statements for the year ended 30 June 2021 were authorized for issue by Councillors on 05/03/2022 and were signed on behalf of the Council by

Soud M. Mbogo
Council Chairman
05.03.2022
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA

Teresia A. Irafay
District Executive Director
05.03.2022
EXECUTIVE DIRECTOR
MLELE DISTRICT COUNCIL

## STATEMENT OF FINANCIAL PERFOMANCE FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Notes | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Local taxes | 9 | 940,566 | 905,717 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 315,257 | 117,749 |
| Amortisation of recurrent grants | 11 | 5,993,276 | 5,711,740 |
| Revenue from exchange transactions | 13 | 29,091 | |
| Amortisation of capital grant | 40 | 3,077,991 | 2,312,416 |
| Other own source revenue | 16 | 157,641 | 82,113 |
| | | 10,513,822 | 9,129,735 |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 17 | 5,691,784 | 5,273,444 |
| Supplies and consumables used | 18 | 987,751 | 1,120,355 |
| Maintenance expenses | 19 | 71,359 | 141,016 |
| Grants and other transfer payments | 20 | 168,233 | 109,197 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 29 | 372,086 | 307,392 |
| Provision for bad debts (Defaulters) | 24 | 95,789 | 378,407 |
| | | 7,387,002 | 7,329,811 |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | 3,126,820 | 1,799,924 |

The Financial Statements for the year ended 30 June 2021 were authorized for issue by Councillors on 05/03/2022 and were signed on behalf of the Council by

Soud M. Mbogo
Council Chairman
05.03.2022
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA

Teresia A. Irafay
District Executive Director
05.03.2022
EXECUTIVE DIRECTOR
MLELE DISTRICT COUNCIL

## STATEMENT OF CHANGE IN NET ASSETS FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Accumulated surplus/deficit TZS '000 | MCR TZS '000 | Total TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **At 1 July 2018** | 9,934,657 | 7,064 | 9,941,721 |
| **Prior year Adjustment** | 7,064 | (7,064) | |
| Surplus/(deficit) for the year | 824,375 | - | 824,375 |
| Minimum Contribution Reserve (LGLB) | | | |
| Restated | (14,128) | 14,128 | - |
| **At 30 June 2019** | 10,751,968 | 14,128 | 10,766,096 |
| **At 1 July 2019** | 10,751,968 | 14,128 | 10,766,096 |
| Surplus/(deficit) for the year | 1,799,924 | - | 1,799,924 |
| Net Asset transfer to Ruwasa | (2,693,790) | | |
| **At 30 June 2020** | 9,858,102 | 14,128 | 9,872,230 |
| **At 1 July 2020** | 9,858,102 | 14,128 | 9,872,230 |
| Surplus/(deficit) for the year | 3,126,820 | - | 3,126,820 |
| **At 30 June 2021** | 12,984,922 | 14,128 | 12,999,050 |

The Financial Statements for the year ended 30 June 2021 were authorized for issue by Councillors on 05/03/2022 and were signed on behalf of the Council by

Soud M. Mbogo
Council Chairman
05.03.2022
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA

Teresia A. Irafay
District Executive Director
05.03.2022
EXECUTIVE DIRECTOR
MLELE DISTRICT COUNCIL

## CASH FLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Note | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| ***Operating Receipts*** | | | |
| Local taxes | 9 | 844,777 | 556,350 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 275,377 | 117,749 |
| Recurrent Grants Received | 11 | 6,150,871 | 5,729,357 |
| Capital Grants Received | 55 | 2,809,814 | 1,581,011 |
| Transfer from other Government entities (Transfer receipts) | 12 | - | - |
| Revenue from exchange transactions | 13 | 21,471 | - |
| Finance income | 14 | - | - |
| Other own source revenue | 16 | 157,641 | 82,113 |
| Change in Deposit Account | 41 | (27,207) | 33,298 |
| ***Operating Payments*** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 17 | (5,822,845) | (4,983,770) |
| Amount transferred to exchequer- | 11 | (14,276) | (66,586) |
| Supplies and consumables used | 18 | (1,048,493) | (1,104,181) |
| Maintenance expenses | 19 | (106,944) | (171,062) |
| Grants and other transfer payments | 20 | (168,233) | (109,197) |
| **Net cash from operating activities** | | 3,071,953 | 1,665,082 |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | 55 | (2,953,489) | (2,255,666) |
| Purchase of property, plant and equipment (prepayment) | 55 | (165,356) | |
| Receipt from WYD groups | 38B | 47,961 | - |
| Grants and other transfer to Women | 38A | (105,000) | (115,950) |
| **Net cash from investing activities** | | (3,175,884) | (2,371,616) |
| **Cash flows from financing activities** | | - | - |
| Proceeds from borrowings | | - | - |
| Repayment of borrowings | | - | - |
| Grants transferred to deposit account | 0 | - | - |
| **Net cash used in financing activities** | | - | - |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | (103,931) | (706,534) |
| Cash and Cash Equivalents at Beginning of the Year | | 1,276,590 | 1,983,124 |
| **Cash and cash equivalents at end of the Year** | 24 | 1,172,659 | 1,276,590 |

The Financial Statements for the year ended 30 June 2021 were authorized for issue by Councillors on 05/03/2022 and were signed on behalf of the Council by

Soud M. Mbogo
Council Chairman
05.03.2022
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA

Teresia A. Irafay
District Executive Director
05.03.2022
EXECUTIVE DIRECTOR
MLELE DISTRICT COUNCIL



## 1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLED AND AUDITER GENERAL

Hon. Chairperson of the Council,
Mlele District Council,
P.O. Box 686,
MPANDA.

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Qualified Opinion**

I have audited the Financial Statements of Mlele District Council, which comprise the Statement of Financial Position as at 30 June 2021 and the Statement of Financial Performance, Statement of Changes in Net Assets and Cash Flow Statement and the Statement of Comparison of Budget and Actual Amounts for the year then ended, as well as the Notes to the Financial Statements including A Summary of Significant Accounting Policies.

In my opinion, except for the effects of the matter described in the basis for qualified opinion section of my report, the accompanying Financial Statements present fairly in all material respects, the Financial Position of Mlele District Council as at 30 June 2021, and its Financial Performance and its Cash Flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap. 290 [R.E 2019].

**Basis for Qualified Opinion**

Under Note 24, Mlele District Council has reported collected revenue through POS not banked amounting to TZS 474,196,000; TZS 95,789,000 in 2020/21 and TZS 378,407,000 in 2019/20 which were all impaired due to uncertainties in recoverability.

I however noted that, of the impaired amount of TZS 474,196,000; no any legal actions have been taken in respect of TZS 132,157,577 against staff and revenue collecting agents including reporting the matter to investigative organs to warranty the disclosure of contingent asset in line with IPSAS 19.

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the audit of the Financial Statements section of my report. I am independent of Mlele District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

### .2 REPORT ON COMPLIANCE WITH LEGISLATIONS

**Compliance with the Public Procurement Act, 2011 (as amended by the Public Procurement (Amendment) Act, 2016)**

**Subject matter: Compliance audit on procurement of works, goods and services**

I performed a compliance audit on procurement of works, goods and services for Mlele District Council for the financial year 2020/21 as per the Public Procurement Laws in Tanzania.

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that, except for the matters described below, procurement of goods, works and services of Mlele District Council is generally in compliance with the requirements of the Public Procurement Laws in Tanzania.

**(a) Annual Procurement Plan (APP) was not confirmed to have been approved by the budget approving authority and published in tender portal**

Regulation 69(7) of the Public Procurement Regulations, 2013 requires a procuring entity to draw up procurement plans for those requirements for which sufficient funds have been included in the approved budget, in the current financial year or if payment is due in the subsequent financial year, such payment has to be budgeted for. Further, Regulation 18(3) of the same Regulations states that, "A procuring entity shall publish the summary in the Journal and a full general procurement notice in the Tenders' Portal at least one month prior to any publication or notification of a tender or a request for proposals to prospective tenderers".

However, the annual procurement plan prepared by Mlele District Council for the year 2020/21 was not published in the general procurement notice through PPRA Tender Portal. Also, there was no evidence on whether the Annual Procurement Plan was approved by the budget approving authority as required by the aforementioned Regulations.

**(b) Non-use of Tanzania National e-Procurement system (TANePs) by the Council for procurements**

Regulation 342 of the Public Procurement Regulations, 2013 requires e-PPs to be implemented by all procuring entities in full or partially in parallel with the conventional manual procedures. Also, a Public Notice issued by PPRA on 20 August 2019 announced full application of TANePS with effect from the financial year 2019/20.

Mlele District Council did not use the system for all procurements made during the financial year 2020/21 contrary to the above-mentioned Regulation.

**(c) Performance bond not renewed to cover the extended time period TZS 439,016,506**

Regulation 29(6) of the Public Procurement Regulations, 2013 as amended by Regulation 12 of the Public Procurement (Amendment) Regulations, 2016 requires the performance security to be kept by the procuring entity until the final completion of the contract and shall be released after issuance of the certificate of acceptance of the final report or certificate of completion of works or services if there is no claim filed against the tenderer, contract guarantor or the surety company.

Performance bond for contract No. LGA.154/2018/2019/W/SS/01 amounting to TZS 2,195,082,530 between Mlele District Council and SUMA JKT for the construction of Mlele District Council Administration Block was not renewed following an extension of the completion time from 11 March 2021 to 06 September 2021 contrary to the aforementioned Regulation. Absence of performance security (bond) exposes the Council to the risk of losing its resources for on-going project in case contractor fail to execute the contract in full.

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General,**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**21 March 2022**

217065902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ongezeko la watalii nchini liwe chachu kuboresha huduma

**UTALII** ni moja ya sekta muhimu nchini katika kuchangia pato la taifa kutokana na kuwa na vivutio mbalimbali vikiwamo hifadhi za taifa ambazo zina wanyama wa kila aina, hivyo kuwafanya watalii kutoka mataifa mbalimbali na wale wa ndani kufika kwenye maeneo hayo na kujionea maliasili hizo.

Kutokana na umuhimu wa sekta hiyo katika kuchangia pato la taifa, serikali imekuwa ikijitahidi kutangaza vivutio vya utalii ambavyo vimezagaa karibu nchini kote ili kuwavutia watalii. Moja ya mikakati ya kutangaza utalii ambayo serikali imefanya ni filamu ya The Royal Tour aliyoicheza Rais Samia Suluhu Hassan ambayo imekuwa gumzo katika sehemu mbalimbali duniani.

Sambamba na filamu hiyo, kumekuwa na juhudi kubwa za kutangaza vivutio vya utalii katika ukanda wa kusini vikiwamo vile vilivyoko katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kwa maana ya Iringa, Njombe, Rukwa, Mbeya na Katavi ambavyo vimekuwa havipati watalii wengi kama ilivyo vile vya ukanda wa kaskazini.

Matokeo ya filamu hiyo yameanza kuonekana baada ya juzi Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, kubainisha kuwa kipindi cha Januari hadi Julai, mwaka huu, watalii 700,000 walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii. Idadi hiyo ni ongezeko kubwa na la kujivunia kulinganisha na watalii 450,000 waliotembelea kipindi kama hicho mwaka jana.

Akizindua mkakati wa kutangaza utalii kusini mwa Tanzania katika hafla iliyofanyika mkoani Njombe, Waziri alisema idadi hiyo inatoa matumaini na kwamba bado watalii wanamiminika, hivyo kuwapo na nuru kwamba sekta hiyo imeanza kukua na kuchangia pato la taifa.

Pamoja na ujio huo mkubwa wa talii, bado kuna haja kubwa ya kuendelea kutangaza vivutio vya kusini mwa Tanzania ambavyo ni vingi vikiwamo hifadhi za taifa za Ruaha, Kitulo, Katavi na Udzungwa. Hifadhi hizo zina wanyama na ndege wa aina za kipekee, hivyo jitihada za kutangaza maeneo hayo zinaweza kuzaa matunda na nchi kunufaika na maliasili hizo.


Sambamba na hifadhi hizo, viko vivutio zaidi kama vile maporomoko ya Kalambo na Ngome ya Bismark mkoani Rukwa, Makumbusho ya Mkwawa Kalenga mkoani Iringa, Kaburi la Nyundo na Kimondo cha Mbozi. Pia katika mkoa wa Mtwara kuna eneo maarufu kama Shimo la Mungu ambalo pamoja na vivutio vingine hivyo, ni hazina kubwa katika kukuza uchumi wa Tanzania.

Ili kufikia azma ya kupata watalii wengi katika mikoa ya kusini, ni wajibu wa serikali na wadau wa utalii kushiriki kikamilifu kutangaza vivutio hivyo ikiwamo kutumia mitandao ya kijamii katika kuvitangaza. Kwa mantiki hiyo, kila mkoa uandae mpango kabambe ambao utawezesha kuutangaza utalii ndani ya wilaya, mkoa na ukanda mzima.

Pia viongozi wa mikoa hiyo wanapaswa kuwahimiza wananchi wao kutembelea vivutio hivyo ili kujionea wanyama na vivutio vingine. Pongezi zinapaswa kumwendea Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, ambaye hivi karibuni aliandaa ziara kwa watendaji wa kata na maofisa tarafa kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuahidi kwenda kuwa mabalozi wa utalii kwa wananchi wao ili watembelee hali itakayokuza utalii.

Sambamba na mikoa na wilaya kuhamasisha utalii, jambo lingine la muhimu ni kwa wadau wa utalii hasa wamiliki wa hoteli na kampuni za kuongoza watalii, kuboresha huduma zao ili watalii wanapofika wasipate shida ya malazi na usafiri kwenda na kurudi kwenye hifadhi na maeneo mengine ya utalii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Beatrice Moses

# Hongera maofisa elimu kwa hatua hii

**MAOFISA** elimu kuanzia ngazi ya kata hadi mkoa jijini Dar es Salaam, badala ya kutembelea na kukagua shule pekee, kuanzia sasa wataingia darasani kufundisha masomo waliyobobea iwe sayansi, sanaa na hesabu, badala ya kufanya ukaguzi kama walivyokuwa wanafanya miaka ya nyuma.

Hatua hiyo imetajwa kuwa ni mojawapo ya mipango iliyowekwa katika kutekeleza miongozo na mikakati ya uendeshaji na usimamizi bora wa elimu katika tawala za mikoa na serikali za mitaa.

Katika mazungumzo na Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam (REO), Abdul Maulid, anabainisha kuwa wanaamini hatua hiyo itasaidia kuboresha au kubaini changamoto wanazokutana nazo wanafunzi au walimu katika masomo mbalimbali kwenye shule hivyo kushirikiana kutafuta ufumbuzi.

Awali, ilikuwa maofisa elimu wakifika shuleni kufanya ukaguzi lakini bila kufundisha lakini sasa mambo yamebadilika wanalazimika kufundisha kulingana na utaalamu wa somo ambalo wanalimudu zaidi.

Mfano, kama Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni mbobezi kwenye somo la English akifika shuleni ataongozana na mwalimu wa somo mwenye kipindi kwa muda huo ambapo atafundisha wanafunzi japo kwa dakika 45.

Hatua hiyo ni njema hasa ikifanyika kwa umakini ambao unaelezewa kuwa ni mbinu ambayo kwa kiwango kikubwa itawatia moyo walimu wa somo linaloongezewa ufanisi kwani kuna baadhi ya changamoto zinazomkabili zitabainika na kiongozi wake hivyo kujenga hoja ili kupata ufumbuzi na uboreshaji zaidi.

Mapema mwaka huu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa, alitoa maagizo kwa maofisa elimu wa mkoa na wilaya nchini kuwasimamia wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu wa masomo, kuzingatia kalenda ya utekelezaji wa mtaala, ili kuwa na ufundishaji na ujifunzaji wenye tija.

Waziri Bashungwa, anatoa maagizo hayo wakati akizindua kalenda za utekelezaji wa mitaala na mafunzo kwa maofisa elimu wa mikoa na wadhibiti wakuu wa ubora wa shule jijini Dodoma.

> **Kusoma na kujifunza kutoka kwenye vitabu na nyaraka mbalimbali mfano kama vile vitabu vya kiada na ziada, ambavyo vinapatikana katika programu zilizoko mitandaoni ni njia ya kupata elimu kwa ufanisi.**

Anawataka maofisa elimu mikoa, kutoa mafunzo ya matumizi ya kalenda ya utekelezaji, katika halmashauri, kabla au ifikapo Februari 1, 2023 kwa hiyo hatua hiyo iliyoelezewa na baadhi ya maofisa elimu kuwa inaonyesha ni kwa jinsi gani pia utekelezaji unavyozingatiwa.

Pamoja na mambo mengine maofisa hao wanapaswa kusimamia kikamilifu ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa madarasa ya awali ili kuhakikisha wanafunzi wanaingia darasa la tatu wakiwa wanamudu kikamilifu.

Ili kutimiza azma hiyo ni lazima wanafunzi wote wasome katika mazingira rafiki kuboresha utoaji wa taaluma na ufaulu katika mitihani ya kitaifa, manispaa zisimamie utekelezaji wa mafunzo ya walimu kazini, kupita kwenye vituo vya walimu na kubadilishana uzoefu na kujenga umahiri wa ufundishaji.

Maono haya ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni mazuri lakini yatafanikiwa iwapo kutakuwa na ushirikiano katika ya maofisa elimu na wakurugenzi pamoja na wadau wengine wa elimu, kwa kuwa kuzitembelea shule kunahitaji bajeti ikiwamo ya usafiri wa kuwafikisha shuleni.

Maofisa elimu, ni lazima wakumbuke kuwa uvivu na uzembe au kutojali kazi kutakwamisha kufikia malengo, hivyo wawe wa kwanza kuona umuhimu wa kutekeleza jambo hilo ipasavyo, hivyo wajitokeze kwa moyo kushiriki ili kufikia malengo.

Pia kwa kuwa ni jambo jema siyo tatizo kwa maofisa elimu wa mikoa mingine kuiga nia hiyo ikiwa ni kuhakikisha sekta ya elimu inakuwa na mafanikio yenye kuleta maendeleo kwa taifa.

## HABARI KITAIFA



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakitengeneza bomba kubwa la inchi 54 lililosababisha kuzimwa kwa mtambo wa kuzalisha maji Ruvu Chini, Jumamosi katika maeneo ya Mlalakuwa na Mwenge. Matengenezo yalikamilika na huduma kurejea kwa wakazi wa maeneo ya Bagamoyo hadi katikati ya Jiji. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri aagiza vidhibiti mwendo magari, mitambo huduma utalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, ameagiza mitambo minane na magari makubwa 23 yaliyonunuliwa kwa ajili ya kuboresha huduma za utalii katika hifadhi za taifa nchini, kufungwa mfumo wa kudhibiti mwendo, mafuta na vipuri.

Pia amekaribisha wawekezaji kujitokeza kuwekeza kwenye hifadhi za kusini ambazo zinahitji maeneo mengi ya watalii kupata chakula, kulala na mahitaji mengine muhimu katika sekta ya utalii ili hifadhi zote ziwe na uwezo mkubwa wa kupokea watalii na kukuza pato la taifa.

Akizungumza jana katika Hifadhi ya Taifa Tarangire, mkoani Manyara, wakati akikabidhi magari 23 na mitambo minane kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) yaliyonunuliwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 16 kati ya 45.7 zilizotolewa na serikali kutoka fedha za UVIKO-19, Balozi Chana alimshukuru Rais Samia Hassan Suluhu kwa kuipatia wizara fedha hizo ambazo zitaimarisha miundombinu ya hifadhi nchini.

"Sasa naomba utunzaji wa mitambo na magari haya na yafungwe mfumo huu wa kudhibiti mwendo, mafuta na vipuri ili kuhakikisha vyombo hivi vinadumu kwa muda mrefu na kunufaisha nchi yetu kwa kuweka miundombinu imara ya hifadhi zetu," alisema.

Pia aliagiza kufanyika mpango maalum wa kuwapatia mafunzo madereva wote watakoendesha mitambo na magari hayo maalum ili wayatunze vizuri inavyotakiwa.

Kuhusu uwekezaji, alisema kwa sasa vema wawekezaji wakajitokeza kuwekeza kwenye hifadhi mbalimbali nchini hasa za Kusini, sababu mitambo hiyo inaboresha miundombinu ikiwamo barabara za hifadhi hizo ili kuwe na hifadhi nyingi zenye uwezo wa kupokea watalii na kuwahudumia.

Alimpongeza Rais Samia kwa kutafuta Sh. trilioni 1.3 za UVIKO- 19 na kuipatia wizara hiyo Sh. bilioni 90.2 ambazo kati ya hizo, Sh. bilioni 46 zimepelekwa TANAPA ili kuimarisha miundombinu ya hifadhi kwa lengo la kulinda rasilimali za taifa na kuvutia zaidi watalii kwa lengo la kuongeza pato la taifa.

"Tunaamini pato la taifa likiongezeka miradi na huduma mbalimbali katika jamii zitaimarika nchini na kwa kuimarisha huduma hizo magonjwa ya mlipuko yatapotea hivyo Rais wetu ametumia akili za kuomba fedha hizi kuimarisha huduma mbalimbali nchini," alisema.

Alisema pia fedha hizo zitatumika kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 1,552 katika maeneo ya Hifadhi za Taifa Serengeti, Tarangire, Saadan, Mkomazi, Katavi na Nyerere.

Kwa mujibu wa waziri, fedha hizo zinakarabati viwanja vya ndege sita katika Hifadhi za Taifa za Tarangire (kimoja), Mkomazi (viwili) Saadani (kimoja) na Nyerere (viwili). Kati ya hivyo, vinne vimekamilika na vilivyosalia viwili kazi inaendelea kwenye Hifadhi ya Taifa Nyerere.


CCBRT

### Tender Notice: Sale of Used Motor Vehicles

**Introduction**
Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT) is a locally registered non-governmental organisation providing specialised healthcare services operating in Dar es Salaam and Moshi, Tanzania. From its inception as a provider of community based rehabilitation, CCBRT has become the largest provider of disability and rehabilitative services in the country.

**Details**
CCBRT welcomes competitive bids for the sale of its used motor vehicles on **'AS IS' and 'WHERE IS'** basis. The vehicles on sale by tender are as listed below and are available for viewing and inspection on week days from 30th September, 2022 from 8am to 2pm at the organizations premises situated, Off Kimweri Road, Msasani, Dar es Salaam, upon arrival call: 0767 123 482 or 0715 552 524.

1. Make Toyota, model Land Cruiser Hard Top, Year 2004, T401AKL.
2. Make Toyota, model Land Cruiser Hard Top, Year 2004, T405AKL.

**Content of the bid**
The bid must include the following information:

1. Name and surname, address, telephone number and e-mail address and physical location.
2. Description of the BID: The goods or services tendered must be described.

**How to submit bids**
Bids may be submitted:

a) In person and inside a sealed envelope, at CCBRT Hospital premises, Off Kimweri Road, Msasani, Dar es Salaam
b) By post, mail order etc. The envelope must be addressed as follows:

**Chief Executive Officer,**
**CCBRT**
**P.O.Box 23310**
**Msasani, Dar es Salaam**

**Terms and Conditions of Sale**

1. The vehicles are sold strictly on **'AS IS' and 'WHERE IS'** basis. CCBRT is not responsible for undertaking any repairs that may be required on the vehicles.
2. Deadline for the submission of the bids is **17th October, 2022, 12noon.**

**IMPORTANT: BIDS SUBMITTED AFTER THE DEADLINE WILL NOT BE ACCEPTED, REGARDLESS OF THE REASONS FOR THE DELAY.**

**Represented in the USA by:** Kupona Foundation

**PO Box 23310, Dar es Salaam, Tanzania • Tel: +255 (0)699 990 000• www.ccbrt.org**
**Email: communications@ccbrt.org • Facebook: www.facebook.com/ccbrttz**
**Twitter: @CCBRTTanzania**

217066002


## KABWELA



HABARI KITAIFA

# Waonywa kufanya uhalifu kisingizio cha kukosa ajira

**Na Martha Sambo,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, amewaonya vijana wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu kwa kisingizio ch a kukosa ajira na badala yake waache na kujikita kwenye kilimo.

Dendego alitoa agizo hilo jana wakati akifungua mkutano wa wadau wa kilimo wa Kongani ya Ihemi ulioandaliwa na Taasisi ya Kuendeleza kilimo Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini unaofanyika katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa (MUCE) mjini hapa wenye lengo la kutathmini maendeleo ya sekta ya kilimo.

Alisema hivi karibuni kumekuwa na wimbi la matukio ya kihalifu ikiwamo uporaji na unyang'anyi kwa kutumia silaha katika maeneo mbalimbali nchini yanayofanywa na vijana maarufu kama 'panya road' kwa kisingizio cha kukosekana kwa ajira.

"Uhalifu si mbadala wa ajira. Jikiteni kwenye kilimo na serikali itawawezesha, kufanya uhalifu si njia mbadala ya kupata ajira. Nawasisitiza vijana jiingizeni kwenye kilimo ili kujipatia kipato kwa njia halali. Acheni kuvunja sheria za nchi kwa kisingizio cha kukosa ajira, hii haikubaliki," alisema Dendego.

Mkuu huyo wa mkoa alisema vijana wengi wanajiingiza kwenye vitendo vya kihalifu kutokana na kuwa wavivu wa kufikiri.

"Vijana ni wavivu wa kufikiri, msipende njia za mkato. Jishughulisheni na kazi halali kama kilimo kujiingizia kipato halali," alisema Dendego.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Lauteri Kanoni, alisema mkoa umeanza mikakati ya kuendeleza sekta ya kilimo kwa kuboresha miundombinu mbalimbali, ikiwamo barabara pamoja na kuendeleza mazao ya kimkakati.

"Tumedhamiria kuendeleza mazao ya kimkakati ikiwamo parachichi na ngano mkoani Njombe," alisema.



Tingatinga likibomoa nyumba kupisha upanuzi wa Barabara ya Kawawa katika eneo la Msimbazi Centre, Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Uhaba watumishi waikumba NEMC

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limeomba serikali iwaongezee idadi ya wafanyakazi ili wamudu kukagua miradi zaidi ya 2,000 ambayo baraza linasajili kwa mwaka.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Menan Jangu, wakati akiwaelezea Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu majukumu ya baraza.

Alisema miradi ambayo baraza linasajili kila mwaka ni mingi kulinganisha na rasilimali watu waliyo nayo ambayo ni watumishi 209 ambao alisema hawawezi kutosheleza mahitaji ya kwenda kufanya ukaguzi kwa ajili ya kutoa vyeti vya mazingira mikoa yote.

Alisema wameshaomba waongezewe watumishi 463 ambao kwa tathmini waliyofanya watatosheleza kufanya shughuli zote za ukaguzi kwenda kanda zote nchini hivyo kufanya kazi ya utunzaji wa mazingira kuwa rahisi na endelevu.

Dk. Jangu alisema mbali na hitaji la watumishi, NEMC inahitaji kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapa ujuzi wa taaluma mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa viwango vya kimataifa.

Alisema ili kwenda na wakati, NEMC imeimarisha miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA kulingana na matakwa ya mfumo wa serikali mtandao e-government.

Alisema mfumo huo umesaidia kuongeza ufanisi wa baraza hususan kwenye utoaji wa vyeti vya mazingira kwani idadi ya vyeti vinavyotolewa imeongezeka maradufu mara baada ya kuanza kwa mfumo huo.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA NIA YA UGAVI WA NONDO (CHUMA)**
**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0008**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kitua cha Kupakia mafuta ghafi kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni wataalamu wenye uzoefu kueleza nia yao kwa huduma za:

**Uhandisi, Ugavi, Ukaguzi wa Nondo (Chuma) kwenye Mradi.**
Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.
Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
- Ugavi wa nondo / chuma kwa viwango vya B500 au ASTM A615.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:
- Wafanyakazi waliohitimu na kuidhinishwa kufanya kazi za Kudhibiti Ubora / Kuthibitisha Ubora (QA/QC);
- Dhamana ya Kazi kwa miezi 24 na miaka 5 ya kasoro fiche (Latent Defects) baada ya kumalizika kwa muda wa dhamana ya kazi;
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa taarifa za fedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha kusimamia kandarasi husika;
- Orodha ya tajiriba / uzoefu na historia ya ugavi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma husika kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linaloshabihiana,
- Chuma ya A3 (A3 Steel) kwa ajili ya uimarishaji wa zege, vipande vya nondo vya kuchomelewa,koili na bidhaa za chuma iliyokunjuliwa (decoiled product),
- BS EN 10080:2005 , Chuma kwa ajili ya kuimarisha zege, Chuma ya kuimarisha zege inayoweza chomelewa,
- A1064/A1064M , Vipimo na viwango vya chuma za Carbon-Steel na Uimarishaji wa Nondo zilizochomelewa, nondo za kawaida au zilizocharangwa, kwa ajili ya zege,
- Sera ya Ubora ya Kampuni, mipango ya Afya na usalama sehemu ya kazi na vyeti vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) au vyeti vinavyoshabihiana;
- Alama ya ubora ya CE kulingana na CPR na BS EN 1090;
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unapendekezwa zaidi.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa procurement@bbnjv.com . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 12 Oktoba 2022, Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi mahitaji yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu mchakato wa awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

217066102


## Wafundishwa kuikabili rushwa ya ngono shuleni

**Na Halfani Chusi**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Kijitonyama Kisiwani, Dar es Salaam, wamepewa elimu ya kukabiliana na rushwa ya ngono pamoja na ukatili wa kijinsia.

Elimu hiyo ilitolewa jana na Taasisi ya Utetezi wa Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), ikilengea kuwabadilisha mtazamo na namna ya kujiepusha na vitendo hivyo.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Janeth Mawinza, walisema wakati wa utoaji wa elimu hiyo kuwa wameamua kufika katika ngazi hiyo baada ya kubaini kundi hilo ni wahanga namba moja.

"Matukio mengi ya ukatili wa kijinsia ukiangalia yanatokea zaidi kwa wanafunzi wa shule za msingi kwa sababu wafanyaji wa matukio hayo huwa wanaona rahisi kuwarubuni wanafunzi kwa sababu hawana elimu," alisema.

Pia aliyataja madhara ya rushwa ya ngono ikiwa ni pamoja kifo, kupata magonjwa ambukizi kama vile kaswende, gono, kuharibika kisaikolojia, pamoja na kushindwa kutimiza malengo kwa mwanafunzi kutokana na mimba zisizotarajiwa.

Kutokana na hali hiyo, aliomba wadau wengine wa maendeleo kujitokeza kudhamini mradi huo, ili waweze kuzifikia shule nyingi ikiwamo za mikoani.

"Sisi tunafadhiliwa na Women Fund Tanzania (WFT) lakini tunaomba wadau wengine wajitokeze kutuunga mkono kwa sababu tunatamani elimu hii tuifikishe nchi nzima."

Mwalimu Mkuu Msaidizi, Sikudhani Semika, alisema taasisi hiyo imekuja kutia mkazo wa kile walichokuwa wanafundisha darasani akibainisha kuwa kitendo hicho kimeongeza zaidi uelewa kwa wanafunzi.

"Sisi kama walimu kila siku tunafundisha darasani vitendo vya ukatili wa kijinsia na tunawafundisha namna ya kujiepusha na vitendo hivi kwa hii taasisi kuja hapa shuleni kwetu na kutoa elimu imefanya jambo la maana sana," alisema.

Mwanafunzi wa darasa la nne katika shule hiyo, Nurati Almasi, alisema elimu hiyo imewasaidia kujua mambo mengi, ikiwamo sehemu sahihi ya kupeleka taarifa inapotokea wamefanyiwa vitendo hivyo.

HABARI KITAIFA

## Kizimbani kwa mashtaka kujitambulisha Rais TFF

**Na Grace Gurisha**

INNOCENT Chengula, mkazi wa Dar es Salaam, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kujitambulisha kama Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia na Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abass huku akijua siyo kweli.

Akisoma hati ya mashtaka juzi, Wakili wa Serikali, Mwanaamina Kombakono, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Yusto Ruboroga wa mahakama hiyo, alidai mshtakiwa anashtakiwa kwa makosa sita.

Alidai Julai 26, 2022 katika sehemu tofauti ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mshtakiwa huyo kupitia kompyuta yake aina ya Infinix, alijitambulisha kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete na kuwa yeye ni Dk. Hassan Abbas huku akijua siyo kweli.

Kombakono alidai Julai 8, 2022 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Chengula alijitambulisha kuwa yeye ni Rais Karia huku akijua siyo kweli.

Alidai kuwa Julai 26, 2022 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Chenguka alijipatia Sh. milioni nne kutoka kwa Ridhiwan baada ya kujitambulisha kuwa yeye ni Dk. Abbas.

Ilidaiwa kati ya Juni hadi Agosti 2022, Chengula alitumia laini za simu za watu wengine ambao ni Asha Shabani, Nuru Maulid na Deogratius Kimario bila kutoa taarifa mamlaka husika.

Baada ya Chengula kusomewa mashtaka hayo, alikana kuhusika na tuhuma hizo. Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kumsomea hoja za awali ambayo ilipangwa Oktoba 10, 2022.

Chengula alipelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ya kuwa na wadhamini wawili waliopaswa kutia saini bondi ya Sh. milioni 10.

# Kijiji chachangia fedha ujenzi kituo cha polisi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WANANCHI wa Kijiji cha Majalila, Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi wameungana na serikali kujenga kituo cha polisi kwa kuchangia Sh. milioni 11 pamoja na vifaa vya ujenzi.

Akipokea juzi mifuko 50 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni moja kutoka kwa Mbunge wa Mpanda Vijijini, Seleman Kakoso, Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu alimwagiza Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi kuhakikisha wanasimamia michango hiyo na kusiwapo upotevu wa aina yoyote.

Buswelu pia alitoa shukrani kwa wananchi na wadau mbalimbali waliojitokeza kuchangia ujenzi wa kituo hicho, alibainisha kuwa vifaa walivyochangia wananchi hao ni nondo na saruji.

"Serikali ya wilaya pamoja na wananchi wote na nguvu ya Mbunge Kakoso wameamua kushirikiana kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kujenga kituo cha polisi cha kisasa, ninawashukuru sana," alipongeza Buswelu.

Awali akikabidhi mifuko hiyo kwa niaba ya mbunge, Katibu wa Mbunge huyo, Said Wambali alisema ofisi ya mbunge imeona iungane na wananchi na wadau kuunga mkono juhudi za serikali kujenga kituo hicho ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa kituo hicho, Ramadhan Nyembe alimhakikishia Mkuu wa Wilaya kuwa michango iliyotolewa na wananchi pamoja na wadau mbalimbali haitapotea na atahakikisha inasimamiwa kikamilifu.

Diwani wa Tongwe, Frank Kibigisa alitoa mifuko 10 ya saruji, akisisitiza kuwa wakitaka kukomesha vitendo vya uhalifu, ni lazima wahakikishe kituo hicho kinakamilika.

Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Majalila walisema kukamilika kwa kituo hicho kutawasaidia kuishi kwa amani kwa kuwa wanaamini uhalifu utadhibitiwa na itakuwa rahisi kwao kufikika kwa haraka kituoni huko kwa kuwa sasa wanafuata huduma Kijiji cha Kibo kilichoko umbali wa takriban kilomita 10 kutoka kijijini kwao.

Hadi sasa ujenzi upo hatua ya msingi ambao umechimbwa kwa nguvu za wananchi na mradi huo unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 500.



Kinamama wasamaria wema wakisaidia kuinyanyua Bajaji ili dereva wake abadilishe tairi lililopata pancha katika Barabara ya Goba, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# DC Jokate ataka uzazi wa mpango kwa wazazi

**Na Faustine Feliciane**

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, amesema maendeleo ndani ya familia na jamii yanaanza kwa wazazi kutumia uzazi wa mpango.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uzazi wa Mpango Duniani ambayo kiwilaya iliadhimishwa katika Hospitali ya Mbagala Rangitatu kwa ushirikiano na Taasisi ya DKT.

Alisema uzazi wa mpango utawapa fursa wazazi kujipanga kwa maendeleo na kuwalea watoto wao katika maadili sahihi.

Alisema wazazi wanapozidiwa na idadi ya watoto hushindwa kuwalea katika maadili na kusababisha kuzalisha vijana wasio na maadili.

"Kwa sasa tuna hii kero ya panya road (vijana wahalifu wa mitaani). Ukiangalia kwa undani vijana hawa wadogo wanaofanya matukio haya wametoka kwenye familia zetu ambazo zimeshindwa kuwapa maadili na sababu ni wazazi kutengana au kuzidiwa na idadi kubwa ya watoto katika kuwalea," alisema.

Jokate alisema vijana wengi wanaofanya matukio hayo ni wale ambao wazazi wao hawakuwalea kwa sababu mbalimbali zikiwamo za malezi.

"Wana Temeke ninataka niwaaambie maendeleo yoyote yanatokana na kujipanga, kujipanga huku kunaanzia kwenye kuzaa, kama tutafuata uzazi wa mpango tutatupata nafasi ya kupanga mambo ya kifamilia kuelekea kwenye maendeleo, mnaona hata serikali inapotaka kutekeleza mambo ya maendeleo lazima ijipange na ndiyo maana tuna masuala kama ya sensa," alisema.



Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Kampuni ya DKT Tanzania, Deogratius Kitama, alisema wanatambua umuhimu wa uzazi wa mpango na ndiyo sababu ya kuandaa maadhimisho hayo huku akiwataka watu kufuata njia sahihi za uzazi wa mpango zinazoshauriwa hospitalini.

Alisema kuwa na watoto sahihi kunasaidia kuwalea vizuri na kuwapatia mahitaji yote muhimu kama elimu na afya bora.

"Taasisi yetu ya DKT Tanzania kwa kutambua umuhimu huu wa uzazi wa mpango, tunatoka elimu kwa watu wanaotaka kuanzisha familia na hata wale ambao tayari wameanzisha familia. Lengo ni kuwafanya kutimiza ndoto zao katika maendeleo," alisema Kitama.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Dk. Ireen Haule, alisema uzazi wa mpango ni eneo muhimu ambayo Manispaa ya Temeke inaiwekea mkazo.

Alisema wanashauri watu kutumia njia sahihi na salama za huduma hiyo zinazotolewa hospitalini.

"Faida ni nyingi sana, sisi kama ofisi ya DMO (Mganga Mkuu wa Wilaya) tunashauri na kusisitiza matumizi ya uzazi wa mpango," alisema Dk. Ireen.

# RC Dodoma apongeza utendaji WCF

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema hivi sasa wafanyakazi wanao uhakika wa kinga na kipato kutokana na majanga yanayosababishwa na ajali, magonjwa na vifo katika maeneo ya kazi kutokana na kuwapo Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Senyamule aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akifungua kikao kazi cha mafunzo ya tathmini za ulemavu unaotokana na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari wa mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma.

"Mfuko ndiyo unaobeba jukumu la gharama zote pindi mfanyakazi anapoumia, kuugua ama kufariki dunia kutokana na kazi," alisema.

Aliongeza kuwa waajiri nao wanapata muda zaidi wa kushughulikia uzalishaji na uendelevu wa biashara zao na hivyo kuongeza tija inayopelekea kuongezeka kwa pato la taifa.

Alisema kuwapo kwa WCF ni hatua mwafaka katika mazingira ya sasa, serikali ikiendelea kujenga uchumi wa kati na hivyo kuwa na ongezeko kubwa la maeneo ya uzalishaji.

"Katika hali ya kawaida ongezeko litakwenda sambamba na ongezeko la matukio na athari zinazotokana na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi katika mazingira haya.

"Jukumu la WCF siyo kulipa fidia pekee bali kushirikiana na wadau katika kubuni, kukuza na kuendeleza mbinu za kupunguza au kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi," alisisitiza.

Aliwaasa washiriki kuwa waadilifu wanapotekeleza jukumu hilo la kufanya tathmini ya ulemavu utokanao na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi ili WCF itoe fidia stahiki na kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu, Dk. John Mduma, alisema mfuko unajivunia kufanya vizuri katika uboreshaji wa mifumo ya kielektroniki ya utoaji huduma pamoja na punguzo la kiwango cha uchangiaji kwa sekta binafsi kutoka asilimia 0.6 hadi 0.5, pia punguzo kubwa la riba kwa madeni ya michango ya nyuma.

Alisema maboresho hayo yanalenga kukuza uzalishaji ambapo sasa waajiri wa sekta binafsi wamepewa nafuu kubwa ya kuelekeza nguvu katika uzalishaji mali, huku mfuko ukiendelea kulinda nguvukazi ya taifa.

"Kama unavyofahamu tayari kuna mabadiliko makubwa sana ya uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara nchini ndani ya kipindi cha serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, na sisi kama mfuko tayari tumejipanga kuhakikisha tunaendelea kutoa huduma bora wakati wote," alisema Dk. Mduma.

Aliishukuru serikali na taasisi zake kwa namna inavyosaidia katika kuhakikisha mfuko unaweka misingi imara katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Aliwakumbusha waajiri kutumia fursa hiyo adhimu iliyowezeshwa na serikali ili kuongeza uzalishaji na hivyo kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Akizungumzia kuhusu mafunzo hayo ya siku tano, alisema yameandaliwa na mfuko kama sehemu ya hatua muhimu kuuwezesha kutekeleza vyema jukumu la kufanya tathmini sahihi na kwa wakati pindi mfanyakazi anapoumia au kuugua kutokana na kazi.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu (kulia), akiongoza mkutano wa pamoja na wadau wa mradi wa kuwajengea wabunge uwezo awamu ya pili (LSP II), ulio chini ya UNDP, katika ofisi ndogo za Bunge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Wanufaika EBARR kupanda miti 8,000

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAKAZI wa Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja wanatarajia kupanda miti ya asili na ya matunda ipatayo 8,000 ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR).

Mradi huo wa miaka mitano unatekelezwa katika shehia tatu za Matemwe Kijini, Matemwe Mbuyutende na Metemwe Jugakuu kisiwani hapa.

Mkazi wa Kijini, Hamad Fakh Makame alisema upandaji miti kupitia mradi huo utasaidia kuhimili mabadiliko ya tabianchi, pia kuboresha lishe katika kaya.

"Tunajua kwa hakika kuwa kwa hatua hizi tutazuia uharibifu wa misitu, jambo ambalo ni zuri kwa mazingira," alisema na kupongeza mradi huo kwa kuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Miti ya matunda itakayopandwa siyo tu itasaidia kunyonya hewa ukaa na kuzuia mmomonyoko wa ardhi, bali pia itasaidia katika kuboresha lishe na afya kwa jamii.

"Mchakato ni mrefu kuanzia kuandaa kitalu, kuotesha miche hadi kupanda hiyo miche katika maeneo yaliyobainishwa. Lakini tumeweza kuandaa miche yetu kwa kufuata utaratibu huo wote.

"Ni matumaini yetu kuwa mradi huu utaboresha mazingira yetu na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na miti ya matunda itatusaidia kuboresha lishe.

"Kwa kifupi, ni kwamba mradi huu tulioanza kunufaika nao mwaka 2021 una manufaa makubwa na niwaombe wahusika waje na mradi mwingine baada ya huu kumalizika," Makame alishauri.

Mkazi huyo wa Kijini alisema kuwa kupitia mradi huo wa upandaji miti, watapata kuni, miti kwa ajili ya ujenzi na matumizi mengine na hatimaye kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mradi wa EBARR unahimiza utunzaji mazingira, usimamizi wa mifumo ikolojia na kutoa huduma muhimu ambazo jamii inahitaji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mratibu wa Mradi wa EBARR kwa upande wa Zanzibar, Alawi Haji Hija alisema kuwa pamoja na shughuli za upandaji miti katika maeneo yaliyoharibiwa katika shehia hizo, mradi pia utahusisha uchimbaji visima virefu vya maji ili kuwezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kilimo cha mboga.

Alibainisha kuwa jumla ya visima sita vimechimbwa huku mradi ukiwezesha vikundi vya uvuvi kwa kuwanunulia boti sita za kisasa na kuwezesha vikundi vya wanawake katika shughuli za utengenezaji wa sabuni, ushonaji na upakasaji.

"Athari za mabadiliko ya tabianchi ni dhahiri nchini na dalili nyingi zimeendelea kujitokeza ikiwamo majira ya mwaka yanayobadilika mara kwa mara, mvua isiyotabirika na kuongezeka kwa joto.

"Jamii za vijijini za wakulima, wafugaji na wavuvi zimekuwa waathirika wa athari hizi husussan katika maeneo ya nyanda kame," alisema mratibu huyo.

Mradi wa EBARR unatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP). Ulianza mwaka 2018 na unategemewa kukamilika mwishoni mwa 2023.

## Ismailia wapanda miti na kuzisafisha fukwe

**Na Halfani Chusi**

JUMUIYA ya Ismailia ya Agakhan nchini imepanda miti na kusafisha fukwe ikiwa ni sehemu ya kusherehekea Siku ya Kiraia ya Jamii ya Waismalia Duniani.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa upandaji wa miti, Mwakilishi Mkazi wa Mtandao wa Maendeleo ya Aghakan, Amin Kurji, alisema lengo ni kupanda miti zaidi ya milioni moja katika fukwe za Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Zanzibar.

"Leo (juzi) tumeanza upandaji miti kwenye fukwe na kuokota taka za plastiki, tumepanda miti 1,500 katika ufukwe wa Bahari ya Hindi maeneo ya Kigamboni, Mji Mwema na Kawe, tumeokota taka za plastiki zaidi ya kilo saba, lengo letu ni kufikisha miti milioni moja.

"Mpango huu utakuwa endelevu kwa sababu baada ya kumaliza fukwe za hapa Dar es Salaam, tutahamia Mtwara, Lindi na Zanzibar, lengo ni kuweka mazingira safi kwa jamii inayotuzunguka," alisema.

Kurji alisema tangu kuanzishwa kwa mpango huo mwaka 2020, mafanikio mengi yamepatikana katika nyanja za afya, elimu, maendeleo ya kiuchumi, usimamizi wa utunzaji wa mazingira na hifadhi za kiutamaduni.

Ofisa Tarafa Wilaya ya Kigamboni, Masele Idd alisema usafi fukwe na upandaji wa mikoko ni muhimu kwa kuwa una faida kubwa kwa viumbe wa baharini.

"Mikoko ndiyo miti ambayo ina uwezo wa kuchukua hewa ya ukaa na kutoa hewa ya oksijeni lakini ni moja ya kivutio cha utalii, inasaidia kupunguza mmomonyoko kando ya bahari. Kwa hiyo, jamii inapaswa kuitunza," alisema Idd.

Alionya wananchi wenye tabia kukata miti hiyo na kuitumia kama kuni, akibainisha kuwa kitendo hicho ni uvunjaji wa sheria na uharibifu wa mazingira.

Katibu Mkuu wa Taasisi Inayosimamia Mazingira ya Usafi wa Fukwe (BMU), Juma Abdallah alisema mikoko ikitoweka katika fukwe za bahari, kutasababisha kupungua kwa samaki.

# Kituo cha Forodha Namanga chakusanya mapato bil.91/-

Na Asraji Mvungi, ARUSHA

KITUO cha Forodha cha Namanga kilichoko Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, kimefanikiwa kukusanya mapato zaidi ya Sh. bilioni 91 kwa mwaka mmoja.

Licha ya mafanikio hayo, bado kinakabiliwa na tatizo la wafanyabiashara wasio waaminifu kuendelea kutorosha bidhaa kwa njia za panya.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa kituo hicho, Paul Kamukulu, alisema ukusanyaji wa mapato unaendelea kuongezeka kutokana na kufanyika maboresho makubwa ikiwamo kuondoa urasimu na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa kodi.

**Kamati hiyo imeridhishwa na kasi ya mabadiliko na utendaji wa kituo hicho.**

Kamukulu, alitoa taarifa hiyo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilyotembelea kituo hicho.

Kamukulu aliyataja matatizo mengine yanayotishia ustawi wa kituo hicho kuwa ni pamoja na ukosefu wa nyumba za watumishi.

Alisema: "Mwaka 2021/2022, Namanga tulipewa lengo la kukusanya shilingi bilioni60.2 lakini tukakusanya shilingi bilioni 91.3, sawa na asilimia 151. Kiwango ambacho hakijawahi kutokea.

Aliongeza: "Hata mwaka huu wa fedha wa 2022/2023, tumeongezewa malengo na sasa tunatakiwa kukusanya shilingi bilioni 99.8 kwa mwaka na tayari tumeanza vizuri."

Alifafanua kuwa katika kipindi cha Julai, lengo ilikuwa ni kukusanya Sh. bilioni 7.6 lakini tumekusanya Sh. bilioni 10.2 na Agosti, lengo lilikuwa kukusanya Sh. bilioni 7.8 na tumekusanya Sh. bilioni 8.8.

Mweyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, alisema kamati hiyo imeridhishwa na kasi ya mabadiliko na utendaji wa kituo hicho.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa (wa pili kushoto), akisalimiana na Mbunge wa Jimbo la Hanang', Mhandisi Samwel Hhayuma, akiwa katika ziara ya siku mbili mkoani Manyara juzi, kwa ajili ya kukagua na kutembelea sekta ya afya, elimu na miundombinu. **PICHA: GIFT THADEY**

# UVCCM Manyara yapata viongozi wapya

Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA

MKOA wa Manyara, umepata viongozi wapya wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) wa wilaya sita za kichama za mkoa huo.

Katibu wa UVCCM wa Mkoa wa Manyara, Ibrahim Kandumila, akizungumza jana na waandishi wa habari Mjini Babati alisema uchaguzi huo umekamilika kwa asilimia 100 na kufanyika kwa amani.

Aliwataja wenyeviti hao waliochaguliwa na wilaya zao kwenye mabano ni Solomon Mekiory (Babati vijijini), Justin Ammi (Hanang') na Magdalena Urono (Babati mjini).

Alisema wengine ni Hamza Mngia (Kiteto), Timothy Mollel (Simanjiro) na Elisante Michael (Mbulu).

"Nawapongeza na kuwashukuru wote walioshinda ila watimize majukumu yao ipasavyo na ambao kura hazikitosha wawape ushirikiano wale walioshinda," alisema Kandumila.

Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Babati Vijijini, Solomon Melkiory, aliwashukuru wajumbe wa jumuiya hiyo kwa kumchagua ili awaongoze na aliomba ushirikiano kwao.

Mwandishi wa Kituo cha FM Manyara na AYO TV, Charles Mangwe ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Babati Vijijini kupitia UVCCM aliwashukuru wajumbe kwa kumpa kura za ushindi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Babati Mjini kupitia UVCCM, Husna Mdinku, aliomba ushirikiano kwa wajumbe hao na kuahidi kuwaunganisha kupitia nafasi hiyo.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa UVCCM Wilaya ya Babati mjini, Elias Ernest ambaye ni mwandishi wa Kituo cha Wasafi aliwashukuru wajumbe kwa kumpatia nafasi hiyo.

## Mwenyekiti mpya UVCCM ataja mikakati yake

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya ya Arusha, Ally Mwinyimvua, amesema katika kipindi cha uongozi wake atahakikisha jumuiya inajiimarisha kiuchumi ikiwamo kuanzisha mradi mkubwa wa kufyatua matofali.

Alisema pia ataimarisha mradi wa ufugaji wa nyuki ambao ulianza kipindi cha uongozi wake kwa kupata mizinga 100 pamoja na kuanzisha miradi mitatu ya uchumi, katika kata tatu.

Mwinyimvua maarufu kwa jina la "Meku" alisema hayo jana baada ya kutangazwa mshindi katika uchaguzi uliofanyika ukumbi wa CCM Mkoa wa Arusha, kwa kupata kura 212 kati ya kura 274 zilizopigwa.

Alisema licha ya mradi huo atahakikisha anaimarisha mradi wa ufugaji wa nyuki, ili wapate asali ya kuuza pamoja na mazao mengine sita yanayotokana na nyuki.

Mwinyimvua alisema jumuiya hiyo lazima ijimaarishe kiuchumi na ana mkakati kabambe wa kuhakikisha kila kata inapata mradi.

"Ninajua jumuiya yetu haina miradi lakini ninataka niwaambie kuwa katika kipindi changu cha miaka mitano, lazima nishirikiane na viongozi wenzangu wa kata ili tuweke alama katika kila kata ili ziweze kujikwamua kiuchumi," alisema.

Alisema maadili katika jamii yameporomoka kwa kiasi kikubwa, hivyo atashirikiana na kamati ya elimu na malezi, kuhakikisha maadili yanaimarika katika jamii ya Wilaya ya Arusha.

## Wamlalamikia kigogo jumuiya ya CCM

Na Mwandishi Wetu, ARUSHA

BAADHI ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM Wilaya ya Arusha, wamemlalamikia Katibu wa Jumuiya hiyo, Eliman Nassari kwa kuhujumu uchaguzi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwa sharti la kutoandikwa majina yao, wajumbe hao walidai kuwa barua ya utenzi aliyokuwa nayo msimamizi wa uchaguzi ilionyesha kuwa jina la Mwinyimvua la ni la kwanza, Ally Mwinyimvua la pili na Meya Mstaafu Gaudence Lyimo ni la tatu.

Walisema lakini kwenye karatasi ya kupigia kura iliyoandaliwa na katibu huyo jina la Mwinyimvua lilikuwa namba mbili na Lyimo namba tatu.

"Mwinyimvua alitumia namba ya Lyimo kuomba kura na Lyimo akatumia namba ya Meku kuomba kura lakini baada ya upigaji kura kuanza wajumbe tukabaini jina la Mwinyimvua ni la pili na jina la Lyimo ni namba tatu ndipo tukaanza kuhoji," alisema.

Mjumbe huyo alidai kuwa wakati huo wajumbe kutoka kata zaidi ya nne walikuwa wamepiga kura hali iliyoibua maswali mengi ikiwamo kwa nini Eliamani hakufuata utaratibu.



# Wakulima wajiandikisha kupata ruzuku ya mbolea

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAKULIMA 30,000 Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wamejiandikisha kupata mgawo wa ruzuku ya mbolea, inayotolewa na serikali kwa lengo la kupunguza gharama ya ununuzi, kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo.

Ruzuku hiyo pia inalenga kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Wilaya ya Hai, David Lekei, wakulima wana fursa ya kuendelea kujisajili, kwa kuwa bado idadi hiyo ni ndogo, ikilinganisha na uwezo wa serikali wa kutoa ruzuku hiyo.

**Mbolea hizo ni zile zinazotumiwa na wakulima hapa nchini kwa kwa zaidi ya asilimia 50.**

"Ili wakulima waweze kupata ruzuku hiyo, wanapaswa kujisajili kwa mtindo wa kidigitali, ambao utawezesha kutambua wakulima wote wilayani hapo wenye sifa za kupata pembejeo za kilimo, kwa bei ya punguzo la serikali," alisema Lekei.

Utoaji wa ruzuku hiyo katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023, utazingatia mahitaji halisi ya mkulima, kulingana na taarifa za usajili na bajeti ya serikali iliyotengwa.

Kutokana na umuhimu huo, Wilaya ya Hai, imesema muda wa mwisho wa kujisajili ili kupata ruzuku hiyo ni Septemba 30, mwaka huu.

Mbolea zitakazohusika kwenye ruzuku hiyo ni mbolea za kupandia na kukuzia, ambazo ni DAP, inayotumika kwa ajili ya kupandia na UREA kwa ajili ya kukuzia.

Mbolea hizo ni zile zinazotumiwa na wakulima hapa nchini kwa kwa zaidi ya asilimia 50.

Aidha, inaelezwa kuwa mbolea za kupandia na kukuzia za aina zingine, nazo zitahusika kwenye ruzuku kulingana na mahitaji ya soko.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba (kulia), akimsikiliza kwa makini mmoja wa wamiliki wa ardhi ya eneo la Amboni, Teresia Ruwanda, ambaye ana mgogoro na mwekezaji wa kiwanda cha kutengeneza rangi, jijini Tanga juzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Serikali yaipa 5 hospitali utatuzi kero za wagonjwa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, amesema serikali imeridhishwa na menejimenti ya Hospitali ya Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro namna inavyotatua malalamiko ya wagonjwa kuhusu utoaji wa huduma.

Amesema hali hiyo inaongeza imani ya wananchi dhidi ya serikali.

Akizungumza juzi na watumishi wa hospitali hiyo, Dk. Mollel ambaye ni Mbunge wa Siha alisema: "Kweli nimefurahi sana kwa jinsi mnavyoendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Siha na kupunguza malalamiko mbalimbali ambayo yalikuwa yanatolewa hapo nyuma".

Alisema miaka ya nyuma baadhi ya watumishi wa hospitali hiyo, walikuwa wakituhumiwa kujihusisha na tabia ya ulevi, huduma zisizoridhisha na matumizi ya lugha zisizo na staha kwa wagonjwa wanaofuata huduma.

Akiwa katika hospitali hiyo, Dk. Mollel alifanya ukaguzi wa shughuli mbalimbali za ujenzi zinazoendelea hospitalini hapo.

Hospitali ya Wilaya ya Siha, inahudumia wakazi zaidi ya 116,313 (kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012) kutoka katika vijiji 60 vilivyoko wilayani humo.

Hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 2007 ikiwa kama kituo cha afya, baada ya vyama viwili vya ushirika wilayani humo kutoa ekari 40 za ardhi.

# Msako kufichua watoto wenye ulemavu waliofichwa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

IDARA ya Elimu ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, imetangaza kuja na mpango wa kupita nyumba kwa nyumba, kata kwa kata, kuwafichua watoto wenye ulemavu waliofichwa.

Pia itawafichua watoto walionyimwa kwa makusudi haki yao ya kupata elimu kwenye shule jumuishi zilizotengwa.

Januari mwaka huu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilizindua mkakati wa kitaifa wa elimu jumuishi wa miaka mitano 2021/22-2025/26, wenye lengo la kutoa elimu jumuishi.

Mkakati huo umekuja na mfumo ambao unatoa fursa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kuanzia ngazi ya awali hadi chuo.

Akizungumzia mkakati huo jana, wakati wa uzinduzi wa zana jumuishi za kufundishia na kujifunzia kwenye madarasa jumuishi, Ofisa Elimu wa Wilaya hiyo, Rose Sandi, aliagiza waratibu wa elimu kata wote, kuanza kujiandaa kutekeleza kazi hiyo kwa ajili ya kuandikishwa wenye ulemavu mwaka ujao.

Zana hizo zilizotengenezwa kwa umahiri mkubwa, zimetolewa na wabia wa maendeleo ya wilaya hiyo pamoja na Shirika la Connects Autism Tanzania (CAT).

"Hili ni agizo na siyo ombi, kwamba kila mratibu wa elimu kata apite kaya kwa kaya na amalize kata yake kwa kuwatambua na kuwasajili watoto wote wenye ulemavu, ambao hawajaandikishwa shule.

"Mwaka ujao (2023) tutawaandikisha kutokana na aina ya ulemavu alionao mtoto. Kila shule jumuishi itapangiwa aina ya watoto wenye ulemavu inaotakiwa kuwapa elimu."

Katika kikao kazi hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa CAT, GraceAnna Lyimo, alisema wao kama wadau muhimu wa elimu jumuishi, wanaunga mkono mpango wa serikali wa kuanza kufundisha walimu mbinu za kutengeneza zana za kufundishia watoto wenye mahitaji maalumu ili kupunguza tatizo hilo.

Alisema: "Bado kuna tatizo kwa wakazi wa wilaya hii kushindwa kuelewa dhana halisi ya mpango wa elimu jumuishi na utekelezaji wake.

Aliongeza: "Elimu jumuishi siyo programu au eneo la kuwahifadhi wanafunzi wenye ulemavu, bali ni utekelezaji kwa vitendo wa utoaji elimu utakaowafanya walemavu kuwa na thamani katika jamii.

Kimsingi, elimu jumuishi ni njia ya ufundishaji inayolenga kuwasaidia na kuwahudumia wanafunzi wenye ulemavu katika muundo wa madarasa ya kawaida." Alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Sanya Juu, Beatrice Matela, akieleza namna mkakati huo unavyosaidia kuwajengea uwezo walimu kutengeneza zana jumuishi za kufundishia, alisema zana hizo zimeongeza chachu kwa watoto wenye mahitaji maalumu kuelewa na kupenda zaidi masomo.



Ukurasa 15

**FATMA FEREJI: Rais Samia mleta mageuzi kidemokrasia anayefungua ukurasa mpya wa Tanzania**



Ukurasa 18

Ni wiki ya tatu William Ruto anachakata Baraza la Mawaziri



Ukurasa 19

**WAZIRI MKUU NETANYAHU 'BIBI'**

**Mbabe aliyeongoza serikali miaka 15 kiboko ya Iran, Palestina na Obama**


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 28, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


## KUFUKUZWA MBATIA:

# Wachambuzi wa siasa waeleza mtazamo wao kuhusu sakata hilo

- Wauliza au kachokwa? Wataka liwe funzo

**Na Sabato Kasika**

WAKATI mgogoro wa uongozi ndani ya Chama cha NCCR-Mageuzi ukiendelea kufukuta, inaelezwa kuwa kinachoendelea ni sehemu ya demokrasia na pia kuchokwa kwa uongozi uliopo madarakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Hebron Mwakagenda,anasema baadhi ya watu wanaamini kuwa demokrasia ni chama kutokuwa na migogoro, na kwamba si kweli.

"Katika kundi la watu wengi, kwa kawaida hawawezi kuwa na mawazo ya kufanana au mtazamo mmoja, watatofautiana, hivyo kinachoendelea ndani ya chama hicho ninakichukulia kama kutalamaki kwa demokrasia," anasema Mwakagenda.

Anafafanua kuwa jamii kuwa na imani kwamba migogoro ndani ya vyama ni si demokrasia ni fikra zinazopingana na dhana hiyo .

Anaongeza kuwa mtazamo huo si sahihi, kwa maelezo kwamba demokrasia inasimama na iko pande zote, ndiyo maana unafika wakati kunakuwa na misimamo ya kukubaliana kutokukubaliana na pia kuna wanaojiita wenye mirengo tofauti yote yakiwa ni kuwa na fikra tofauti.

"Kufukuzana katika chama au kuvuliwa uongozi ni sehemu ya demokrasia ili mradi katiba imefuatwa, hivyo hao waliokutana na kuchukua hatua hiyo ndiyo wanaojua kama mkutano ulikuwa halali au hapana," anasema.





James Mbatia (kushoto) na Joseph Selasini anayeratibu jukumu la kumwondoa Mwenyekiti wa Taifa kwenye chama hicho.
**PICHA: MTANDAO**

**UONGOZI UMECHOKWA**

Aidha, kwa upande mwingine, Mwakagenda anaongeza kuwa kinachoendelea ndani ya NCCR- Mageuzi kinapaswa kuwa fundisho kwa viongozi wengine waliokaa madarakani kwa muda mrefu.

Anasema Mbatia amekaa madarakani kwa zaidi ya miaka 20, na kwamba miongo miwili kwenye uongozi inawezekana wanachama wamejitahidi kutaka kubadilisha wakuu wa chama lakini wameshindwa, wakaona wafanye kila njia kuhakikisha anang'oka.

"Hatua hiyo inapaswa kuwa fundisho kwa viongozi wa vyama vingine vya siasa waliokaa madarakani kwa muda mrefu wajifunze kutoka NCCR- Mageuzi na kuachia ngazi pale wanapoona wamechokwa ," anashauri.

Anaeleza kuwa kila chama kina maamuzi yake, na kwamba haoni tatizo kama kilichofanywa na makada wa chama hicho kimezingatia matakwa ya katiba ya NCCR- Mageuzi, lakini pia anawakumbusha wanachama na viongozi kuwa kila mmoja ana haki yake na kwamba katiba ndiyo ya kuzingatia.

"Pamoja na hayo, nirudie kusema kwamba, kumuondoa kiongozi madarakani au kumfukuza katika chama, ni demokrasia, hivyo hatua iliyochukuliwa na NCCR-Mageuzi isitafsiriwe kama ukiukwaji wa demokrasia," anasema.

**KELELE ZA NINI?**

Mchambuzi mwingine wa masuala ya siasa na mwenendo wa demokrasia Gwandumi Mwakatobe, anaeleza kushangaa kusikia James Mbatia na wen-

**INAENDELEA UK. 20**

# Oktoba mwezi wa kazi kwa TLP, kuanza rasmi kusukwa upya

- Waliokimbia waitwa kurudi kundini,
- Wanaokaribishwa wanatoa masharti



Kaimu Mwenyekiti wa TLP Taifa, Alhaji Hamad Mukadam (kulia) na Katibu Mkuu wa chama hicho Richard Lyimo

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Tanzania Labour Party -TLP, kinatarajia kuanza mikakati ya kujiimarisha upya kuanzia Jumamosi Oktoba mosi, kwa kukutana na viongozi wa chama hicho wa ngazi mbalimbali wa mkoa wa Dar es Salaam ili kujiandaa na masuala makubwa ya mabadiliko huku jicho likielekezwa kwenye uchaguzi mkuu wa 2025 pamoja na wa serikali za mitaa.

Mara baada ya kumaliza katika mkoa huo, viongozi wa kitaifa chini ya Kaimu Mwenyekiti wa TLP Taifa, Alhaji Hamad Mukadam, watazunguka mikoa mingine ya Bara na Zanzibar kwa lengo hilo la kujiimarisha kisiasa na kufufua chama.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili wiki hii, Mukadam anasema kwa muda mrefu chama hicho kilikuwa hakifanyi kazi kikamilifu, hali ambayo ilisababisha kionekane kama kimekufa, lakini hilo sasa limepita na wameamka na kuongeza:"Lakini sasa tunakuja upya, Oktoba mosi tumepanga kukutana kwanza na viongozi wetu wa mkoa wa Dar es Salaam, ili kuweka mikakati ya kujiimarisha na kisha tutakwenda mikoani kwa kazi hiyo."

Kaimu mwenyekiti huyo aliyechaguliwa hivi karibuni uongozi baada ya kifo cha Mwenyekiti wa chama hicho Augustine Mrema, anasema TLP bado ina nguvu, ila imepitia vikwazo vingi vilivyosababisha iwe kama haipo kwenye anga za kisiasa.

"Chama chetu ni miongoni mwa vyama vyenye usajili wa kudumu, hivyo ni lazima kifanye shughuli za kisiasa, ndio maana tumepanga kuanzia Oktoba mosi tukutane na viongozi wa chama wa mkoa wa Dar es Salaam," anasema kwamba, kwa miaka mitatu Kamati Kuu haijawahi kukutana, wala Halmashauri Kuu na hata Mkutano mkuu wa chama haujawahi kufanyika vitu ambavyo ni muhimu ndiyo maana sasa wanajipanga upya.

> "Baada ya msiba wa Mwenyekiti wa TLP Taifa, tayari tumeshapata mtu anayekaimu nafasi hiyo, sasa kilichobaki kujipanga upya ikiwa ni pamoja na kuwaomba waliotukimbia warudi tuungane kukijenga chama chetu na kushiriki kwenye kuendeleza mchakato wa demokrasia za vyama vingi," anasema.



Wanachama wa zamani wa TLP Thomas Ngawaiya (kulia) na Hamad Tao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**WITO WALIOKIMBIA**

Katibu Mkuu wa chama hicho, Richard Lyimo, anawaomba wanachama wote walioihama TLP kutokana na sababu mbalimbali, warejee kundini ili kusaidiana kusuka upya chama hicho, akiahidi kuwa milango iko wazi na hakuna pingamizi wala lawama dhidi yao.

Lyimo anasema, kwa nyakati tofauti chama hicho kilikimbiwa na baadhi ya wanachama wake wakiwamo wenye majina makubwa ambao sasa anawaomba warejee nyumbani ili kusaidiana kuweka mikakati ya kukisuka upya. akisisitiza:"Ninawaomba wanachama wote wa TLP ambao waliondoka katika chama kwa kukwazwa au kutoridhishwa na uongozi warudi, ili tukijenge chama chetu kiwe kwenye hadhi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma," anasema Lyimo.

Anafafanua kuwa, hakuna masharti yoyote kwao, na kwamba jambo la msingi ni kuungana pamoja kukijenga chama hicho, ili kijiandae kwa ajili ya uchaguzi ujao wa mwaka 2024 wa serikali za mitaa na wabunge, rais na madiwani kwa 2025.

Miongoni mwa waliokikimbia chama licha ya kwamba hakuwataja ni pamoja na viongozi wakuu kama Katibu Mkuu Hamad Tao, Nancy Mrikaria, mwanachama na mfadhili mkuu Thomas Ngawia, pia mwasisi Leo Lwekamwa na mgombea urais wa TLP 2010 Mutamwega Mugayhwa.

"Baada ya msiba wa Mwenyekiti wa TLP Taifa, tayari tumeshapata mtu anayekaimu nafasi hiyo, sasa kilichobaki kujipanga upya ikiwa ni pamoja na kuwaomba waliotukimbia warudi tuungane kukijenga chama chetu na kushiriki kwenye kuendeleza mchakato wa demokrasia za vyama vingi," anasema.

**MASHARTI YA KURUDI**

Aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho Hamad Tao, alipoulizwa kuhusu wito huo wa TLP wa kurejea nyumbani , anasema yuko tayari kurudi, lakini anataka aelewane na uongozi kwanza kwa mambo yanayohusu kufanya shughuli za kisiasa.

"Pale TLP kuna watu wanang'ang'ania madaraka bila kufanya kazi, mimi si mtu wa kula na kulala, hivyo kama wanataka nirudi, wakubali nifanye mikutano ya hadhara kuingiza wanachama wapya, vinginevyo inakuwa vigumu kurudi, kwa sababu mimi ni mtu wa kazi," anatamba Tao.

Tao anasema, TLP imefikia hali hiyo ya kukosa wenyeviti wa serikali za mitaa, madiwani na wabunge, kwa madai kwamba viongozi wake wanataka kuwa na chama ambacho ni tishio kwa chama tawala na kuongeza:"Bila TLP kuchukua hatua za kweli za kujiimarisha, kinaweza kuendelea kuwa cha kusindikiza vingine, na kama viongozi wake sasa wanataka kubaadilika, wakubali kufanya kazi na si kuwa wasindikizaji wa vyama vingine," anasema.

Mwanasiasa mwingine aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa TLP, Nancy Mrikaria, ambaye kwa sasa amejiunga na Chama cha AAFP, anasema hawezi kuzungumzia lolote kuhusu ombi hilo."Ninaendelea na kazi yangu ya siasa kwingine, hivyo ninaomba uniache, siwezi kuzungumzia mambo ya chama kingine, lakini uniulize kuhusu maendeleo ya AAFP," anasema Nancy.

**HESHIMA KWA CCM**

Mbunge wa zamani wa Moshi Vijijini kupitia TLP, Thomas Ngawaiya, anasema haoni sababu yoyote ya kumtoa CCM kurudi upinzani, kwa madai kwamba chama hicho kimemfanyia mengi.

"Baada ya kuhama kutoka upinzani, niliaminiwa na chama na kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM mkoa wa Kilimanjaro, na kusimamia majukumu yangu vizuri hadi kustaafu, hivyo sioni sababu ya kunifanya nihamie upinzani," anasema Ngawaiya.

Aidha, anaongeza kuwa upinzani wa sasa sio kama wa miaka ya 90 wakati mfumo wa vyama vingi unarejeshwa nchini, na kwamba ameamua kupumzika siasa za majukwaani akiwa mwanachama hai wa CCM.

"Kinachotakiwa kwa sasa ni kuwaachia nafasi vijana, ili waonyeshe uwezo wao wa kuongoza, hivyo wakati huu ambao TLP wanapanga kujiimarisha upya, wakumbuke kuwapa nafasi za uongozi vijana wao," anasema.

Anasema, viongozi ambao kwa sasa ni watu wazima, hawana budi kuwaandaa damu changa, ili waje kushika nafasi zao, na kwamba TLP wanaweza kutafuta vijana wakati huu chama kinapoongozwa na mwenyekiti taifa wa mpito.

"Niwatakie maandalizi mema ya ujenzi mpya wa chama chao, lakini niwashauri kwamba, suala la uongozi waangalie zaidi katika kuwekeza kwa vijana kwani ndio wenye nguvu za kufanya harakati za kisiasa," anasema.

FATMA FEREJI:

# Rais Samia mleta mageuzi kidemokrasia anayefungua ukurasa mpya wa Tanzania

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JUHUDI za Rais Samia Suluhu Hassan, kuleta mageuzi ya kidemokrasia zinatajwa kuwa zinalenga kufungua ukurasa mpya kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao utajenga siasa za ustahamilivu, kuheshimiana na maelewano miongoni mwa Watanzania.

Mjumbe wa kikosi kazi cha Rais Samia, kinachokusanya na kuratibu maoni ya wananchi kuhusu marekebisho ya katiba, Fatma Alhabib Fereji , anasema hayo na kuongeza kuwa kazi kubwa inayofanywa na Rais Samia katika kuleta mageuzi ya kidemokrasia ni hatua muhimu kwa maendeleo kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Akizungumza na wanawake wanasiasa mjini Zanzibar, Fatma anasema, juhudi za Rais Samia zinastahiki kuungwa mkono kwa sababu lengo lake ni kufungua ukurasa mpya kwa Watanzania wote ili kuwaunganisha na kujenga siasa za ustahamilivu na maelewano.

Fatma mwanasiasa mkongwe aliyewahi kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, anasema kazi waliyopewa na Rais Samia ya kukusanya maoni kuhusu mwenendo wa kisiasa wameikamilisha na kumkabidhi.

"Rais Samia ametupa kazi kwa kuunda kikosi kazi cha kukusanya maoni ambapo jukumu hilo tumelimaliza na kumkabidhi na matarajio yetu mambo yote yaliokusanywa yatafanyiwa kazi" anasema Fatma ambaye ni mjumbe wa Kamati Kuu na Katibu wa Mambo ya Nje wa Chama cha ACT Wazalendo na kumpongeza Rais kwa kurejesha imani kwa viongozi wa vyama vya siasa.

Anawataka wanawake kujitokeza na kuwania nafasi za uongozi ili kufikia malengo ya uwakilishi wa asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vya kutunga sheria hasa Bunge na Baraza la Wawakilishi lakini pia kwenye nyadhifa nyingine nyingi zinazohitaji kila Mtanzania kushiriki.

Anasema dalili za kuwepo kwa mafaniko hayo zimeanza kuonekana kufuatia Tanzania kuwa na Rais mwanamama na teuzi mbalimbali anazozifanya zimekuwa zikizingatia usawa wa kijinsia, akitaja majaji wa mahakama za ngazi mbalimbali na wakuu wa mikoa na wilaya pia.

"Kwa mfano kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania Waziri wa Ulinzi kuwa mwanamke ambaye ameteuliwa katika uongozi wa Rais Samia, aidha .

Wizara ya Mambo ya Nje kwa miaka mingi imekuwa ikishikiliwa na wanaume licha ya mara moja kuongozwa na mwanamke Dk. Asha-Rose Migiro, lakini kwa uongozi wa Rais Samia nafasi hiyo imekwenda kwa mwanamke. Hizi ni wizara nyeti sana ambazo kwa miaka yote zimekua zikiongozwa na wanaume lakini katika awamu ya sita wanawake wenye sifa na vigezo vya kimataifa wamepewa majukumu,"anasema Fatma.



Fatma Alhabib Fereji.

> ''Nimefurahishwa na uongozi wa Rais Samia kwa kutoa nafasi nyingi za uongozi kwa wanawake kitendo ambacho kinajenga ujasiri kwa kundi hilo kufikia...

"Huu ni wakati wa kuhakikisha wanawake wanajiimarisha kielimu ili kufikia vigezo na sifa zinazohitajika katika nafasi mbalimbali za uongozi. Kadri siku zinavyosonga mbele dunia inabadilika ambapo masuala ya elimu ni miongoni mwa sifa na vigezo vinavyohitajika."

Fatma mwanamama wa pili kutoka chama cha upinzani cha CUF kushika nafasi ya uongozi kwa kuchaguliwa jimboni akiongoza jimbo la Mji Mkongwe kwa muda wa miaka mitano katika miaka ya 2000, anasema utafiti alioufanya amebaini kuwa wanawake wanakubalika katika jamii kwa kuchaguliwa na wananchi kushika nafasi za uongozi lakini changamoto kuu ni mfumo dume ambao hivi sasa unaanza kutoweka kutokana na elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali.

Anasema huu ni wakati muafaka kwa wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi kwa sababu mazingira yamebadilika na kuonyesha uwezo mkubwa wa wanawake kukubalika katika jamii.

''Nimefurahishwa na uongozi wa Rais Samia kwa kutoa nafasi nyingi za uongozi kwa wanawake kitendo ambacho kinajenga ujasiri kwa kundi hilo kufikia malengo ya kushiriki katika uchaguzi na kuchaguliwa" anasema na kuvitaka vyama vya siasa kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake kuingia katika harakati na kuchaguliwa kuongoza majimbo.

Anasema vyama vya siasa ni nyenzo kubwa ya wanawake katika kujenga ushawishi wa harakati za kisiasa na hatimaye kuingia katika uchaguzi na kuibuka na ushindi.

''Nimeona katika harakati za kisiasa za kuwania uongozi ikiwemo kampeni za uchaguzi ushawishi mkubwa upo kwa wanawake ambao ndiyo wenye kuamsha ari ikiwamo matayarisho ya mikutano na hamasa zake kwa ujumla,"anasema Fatma.

"Wakati muafaka kwa vyama vya siasa kuhakikisha sera na ilani zake zinakuwa na mabadiliko makubwa ikiwamo mgawanyo wa nafasi za uongozi kwa wanawake, mabadiliko hayo pia yanaihusu Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo ndiyo inayoratibu shughuli za vyama vya siasa kuona na kusimamia mabadiliko hayo muhimu kwa ajili ya kuleta mageuzi makubwa ya kisiasa kwa usawa wa kijinsia."

Anafahamisha kuwa ni muhimu kwa vyama hivyo kuweka katika katiba zao masuala ya usawa wa kijinsia ambayo yatatoa nafasi kubwa kwa vyama vya siasa kuwa na ushiriki wa wanawake na kuwawezesha kuwania nafasi za uongozi na kwamba wakati umefika kuwepo kwa mabadiliko makubwa ya mfumo wa sera na katika kuona wanawake wanapata nafasi za uongozi pamoja na mgawanyo wake .

**MAFANIKIO**

Fatma mwenye miaka 61, ameanzia masomo yake Shule ya Msingi Darajani kuanzia mwaka 1967 hadi 1973 kisha kujiunga na Sekondari ya Hamamni Zanzibar na kuhitimu 1976, alipata shahada ya kwanza ya Ualimu wa Sanaa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1986 na shahada ya uzamili ya ukutubi katika Chuo Kikuu cha Wales mwaka 1991.

Fatma ni miongoni mwa wanawake vinara ambapo mwaka 2013 Ubalozi wa Marekani ulimtaja kuwa mwanamke jasiri na kumpa tuzo, (Tanzania Women of Courage Award).

Kwa mujibu wa Ubalozi wa Marekani sababu za kuteuliwa kwake ni kutokana na mchango wake mkubwa katika kufanikisha ushiriki wa wanawake katika siasa.

Vigezo vingine ni mchango mkubwa alioutoa katika kufanikisha maridhiano ya kisiasa Zanzibar, ambayo yamefuta uhasama miongoni mwa wananchi wa Zanzibar mwaka 2009, kusimamia upatikanaji haki za wanawake na watoto, pamoja na kuhimiza na kusimamia utawala bora na uwazi serikalini.

Mwanamke mwingine aliyeteuliwa kupata tuzo hiyo ni Ndinini Kimesera Sikar, ambaye ni miongoni mwa waanzilishi wa taasisi inayoshughulikia Maendeleo ya Wanawake Wamasai (MWEDO), hasa katika kusimamia elimu, na kuwajengea uwezo wanawake na watoto katika jamii hiyo.

# Mwitaji anapoomba jicho la Rais kuinua uwekezaji

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

PAULETHA Leso licha ya kuishi na ulemavu wa miguu hana mpango wa kurudi nyuma wala kukata tamaa, akitamani kuwa mhandisi wa ufundi viatu vya ngozi za wanyama pia, mmiliki wa kiwanda kinachovizalisha.

Ni mkazi wa Nzuguni 'B' mkoani Dodoma anayesema anatumia maneno hayo hakuna kukata tama kujipa ujasiri wa kupambana na maisha ili kufikia ndoto yake ya kuwa mtaalamu wa masuala ya bidhaa za ngozi hasa viatu.

Pauletha, ambaye ana fani mbalimbali zinazomsaidia kujikwamua kiuchumi ni mama wa watoto wawili na mumewe ni Stephano Nyangebobu, ambaye pia anaishi na ulemavu wa miguu.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum, anasema, kutokata tamaa ni kama wosia aliopewa na baba yake enzi za uhai wake kwa ajili ya kupambania ndoto zake za kufikia kwenye kilele cha mafanikio.

"Napambana kufikia ndoto zangu za kuwa mhandisi wa ufundi hasa wa viatu vya ngozi na ninatamani niwe na shule ya ufundi itakayowasaidia wenzangu wenye ulemavu na mabinti wanaokabiliwa na hali ngumu kiuchumi ili tujikwamue,"anasema Pauletha.

**ANAKOTOKA**

Pauletha anasema, hakuzaliwa na ulemavu aliupata akiwa na umri wa miaka 11 baada ya kuugua polio lakini hakukata tamaa.

"Nilisoma hadi darasa la saba, nikafaulu Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora kuendelea na masomo lakini nilishindwa kutokana na ukweli kuwa miundombinu ya zamani haikuwa rafiki kwa wanaoishi na ulemavu. Niliishia kusoma muhula wa kwanza kuanzia Januari hadi Juni, nikarudi nyumbani baada ya kukwama kupanda ngazi nyingi."

"Nawashukuru wazazi wangu sasa wote ni marehemu walinishauri, baba alinisimamia kuhakikisha ndoto zangu zinatimia akisisitiza nisikate tamaa nilimwambia nahitaji ufundi wa ushonaji. Alinipeleka kwa watawa wa Veyula katika Chuo cha St. Gabriel nikajifunza ushonaji wa nguo kwa muda wa miaka miwili na sasa ninaweza,"

Anasema, alipohitimu aliamua kujitegemea akipanga chumba na baada ya hapo baba yake akafariki na muda kidogo mama yake naye. Baada ya vifo hivyo akabaki mwenyewe na ndugu zake lakini kwa kuwa alishajiwekea malengo alijituma kwa kila namna ili asiwe tegemezi, anaongeza. Anasisitiza kuwa, ulemavu aliuondoa kabisa katika maisha yake na hakuwa na manung'uniko akimshukuru Mungu wakati wote akifuata wosia wa baba wa kufanya kazi ili jamii imheshimu maana asipojituma kwenye kazi atakuwa mzigo na watu watamchoka.

Anasema, alitumia viungo alivyo navyo kuchangamkia fursa ili jamii imuone kuwa anaweza na hilo lilifanikiwa na kuongeza:"Nilijichanganya na watu hawakuninyanyapaa, niliungana na marafiki ambao sio walemavu hivyo nilikuwa nawatumia kama miguu yangu na wakitumia akili zangu,"anasema.



Mwenye muhitaji akielezea kero zake kwa kiongozi. **PICHA: MAKTABA.**

> "Nawashukuru wazazi wangu sasa wote ni marehemu walinishauri, baba alinisimamia kuhakikisha ndoto zangu zinatimia akisisitiza nisikate...

**VIKWAZO ASIVYOVISAHAU**

Anabainisha kuwa baada ya kutoka chuoni St. Gabriel alipanga chumba na kukaa mwenyewe ambapo alikumbana na kero nyingi ikiwamo choo cha kuchangia kisicho rafiki, lakini mwenye nyumba kumpangia zamu ya usafi bila kuangalia hali yake.

"Alikuwa ananipangia kwa wiki nzima lakini kwa vile nilikuwa na marafiki wazima walikuwa wanisaidia ndio maana nikajenga urafiki na watu ili nikihitaji maji wananiletea,"anasema.

Anaeleza kuwa, usafiri pia ilikuwa ni kikwazo kwake alikuwa anatumia baiskeli kutoka sehemu moja kwenda nyingine na wakati mwingine ulikuwapo usumbufu mwingi.

Pauletha ni mtu wa kuongeza ujuzi alikwenda hadi Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), kusaka fani ya kutengeneza batiki na sabuni akijifunza kwa wiki moja na kuhitimu na anatamani kuongeza ujuzi.

"Malengo yangu bado hayajakamilika, nitajifunza nini nikafikiria nikaona kwenye suala la batiki na sabuni watengenezaji ni wengi soko lina shida nikafikiria nikasema hapana kuna kazi nyingine nahitaji kujifunza siku moja nikasikia tangazo linatangazwa kuwa jijini Dar es salaam kuna watu wamejitolea kusaidia wenye ulemavu kujifunza kutengeneza viatu lakini nauli, gharama za malazi watajitegemea ila kule kila kitu ni bure ndipo nilipoamua kujikusanya na kwenda Dar nikajifunza kwa kipindi cha miezi sita kutengeneza viatu vya ngozi."

Anasema, anashona sare za shule na viatu vya ngozi vya watoto vya shule na vya watu wazima akitumia mikono lakini, akisisitiza kuwa ana ndoto ya kufungua darasa ili awafundishe wengine wenye mahitaji kwa vile hataki kuwaona wakihangaika.

**ALIVYOPATA MWENZA**

Pauletha na Stephano, walikutana Dar es Salaam alipokwenda kujifunza ufundi huo wakati huo Stephano akiwa fundi ameshaelewa kila kitu na alikuwa mwalimu wake.

"Mpaka sasa ni mwalimu wangu amenifundisha na baada ya hapo ndipo tulipoelewana kwa sababu naye alinitajia changamoto zake na mimi nikamwambia zangu. Anasema alipopata wachumba akipeleka posa walimkataa ,nami nikamwambia yangu ndipo tulipoona tukae pamoja tuongee tuelewane lakini ilileta shida kwa jamii hawakutukubali haraka waliona ni ajabu kwa Tanzania hii, kwa watu wenye ulemavu wote kwenda kufunga ndoa kanisani."

"Sisi tulipanga kufunga ndoa kanisani ili watu waone tena wajifunze, hatukutaka kuchukuana kienyeji tulisema twende kanisani, ndoa yetu ilipendeza watu walifurahi na walikuja wengi kushuhudia wengine wakikejeli tuone watazaa watoto wa aina gani lakini tumezaa watoto wawili wazima na wajukuu zetu wapo ni wazima na watu wa kawaida,"anasema.

Anasema, kwasasa wanaishi Dodoma na wamejenga nyumba huku wakiwa na maono ya kufungua kiwanda chao wenyewe.

"Sijawahi kujuta kuwa naye, nimefurahi kitu kimoja kazi tunafanya pamoja akikata ngozi mimi nashona au akishona mimi nakata kwa hiyo jioni tunarudi pamoja hakuna mtu wa kunisumbua. Ila kama mwanaume ambaye hana ulemavu pengine angerudi usiku wa manane nikimuuliza agenijibu anavyotaka lakini yeye tupo vizuri namshukuru Mungu na hatujagombana,"anasema.

**AOMBA HURUMA**

Pauletha, anaomba huruma ya Rais Samia Suluhu Hassan, amuunge mkono kuanzisha kiwanda kikubwa kitakachosaidia watu wengine wenye ulemavu na mahitaji maalum hasa wanawake wakiwamo wajane pia.

"Kwenye mikopo ya halmashauri tulikuwa na kikundi tulipata Shilingi milioni 10 lakini tulikuwa watano hivyo tuligawana 2,000,000 kila mmoja, sisi tukanunua mashine kwa ajili ya shughuli yetu ya viatu,"anasema.

Anasema; "Hali ya biashara ni ngumu kutokana na changamoto ya usafiri tunatamani kuwa na eneo pale soko la Ndugai ili tuweze kupeleka bidhaa kwa pamoja,kwa sasa tunalazimika kupeleka kwa mteja kidogo kidogo na kutokana na hali yetu ni lazima tukodi usafiri ambao ni gharama kubwa ukilinganisha na hela inayopatikana."

"Viatu vya shule ya awali hadi shule za msingi ni Sh.15,000 kwa bei ya kiwandani ila kikitoka na kwenda sokoni ni Sh.18,000 hadi 20,000 ,vya watu wazima Sh.20,000 kwa kiwandani na sokoni ni Sh.25,000, tunashona ngozi halisi,"anasema na kukaribisha wateja.

WABUNGE WAMESIKIA AJALI HIZI......

# Waje na sheria matumizi ya simu, miziki barabarani

• Ulazima mikanda kwa abiria wote kwenye mabasi

**NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA**



Ajali za barabarani zinahitaji sheria mpya na hasa zinazolenga kupunguza tatizo hilo linalokua na kuathiri kila sekta. **PICHA: MTANDAO**

KIFO au ajali barabarani huanzia na bajaji kujaza abiria kupindukia wakiwamo wanaokalia hadi usukani, boda nao madereva hujaza abiria kwa utaratibu wa mishikaki ya watu wanne.

Mambo mengine ni malori kujitanua kwa ubabe na kujitumbukiza barabarani yakiwawekea bodi magari madogo kwa ujeuri kuwa ni makubwa hivyo wadogo hawafurukuti. Matokeo yake ni ajali Watanzania wakimalizia safari ya maisha barabarani na mamia wakiishi na ulemavu.

Ajali za barabarani zinapoongezeka kutoka matukio 858 hadi kufikia 955 kwa mwaka mmoja ni kiashiria kuwa taifa lisipoziba ufa ujenzi wa ukuta unalisubiri.

Aidha, ni kuiamsha jamii kuanzia wabunge wanaotunga sheria, kupitisha bajeti ya serikali na wadau kufahamu kuwa udhibiti wa ajali za barabarani haukwepeki ni lazima kubuni na kutumia jitihada zote kuzipunguza kwa sababu ni chanzo cha vifo na umaskini.

Zinapotokea nyingine zinakatisha maisha ya watu, kusababisha ulemavu wa kudumu lakini pia huongeza yatima, wajane na wagane na utegemezi katika jamii, uharibifu wa mali hasa magari, miundombinu ya barabara na madaraja.

Vilevile ajali hizo zinasababisha matumizi ya mabilioni ya fedha kusafirisha na kuuguza majeruhi kwenye hazina ya taifa kwa vile mabilioni ya pesa hutumika kwenye Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), fedha ambazo yamkini zingeweza kutumika katika matumizi mengine ya kimaendeleo endapo ajali hizo zisingetokea.

Ndiyo maana wabunge wanaopitisha bajeti ya serikali na kutunga sheria mchango wenu unahitajika hapo. Ni vyema sasa muanze kuangalia na kuandaa sheria za kuzuia matumizi ya simu barabarani na pia suala la boda boda kubeba watoto na pia kuvaa mikanda kwenye mabasi bila kupendelea ya mikoani pekee.

Ikumbukwe kwa daladala anayevaa mkanda ni dereva pekee wengine wanasubiri nini, bunge lilitazame pamoja na wadau ili kuwe na Tanzania isiyo na ajali.

Mwishoni mwa mwezi uliopita Mkuu wa Jeshi la Polisi-IGP Camilius Wambura, akiwa Moshi mkoani Kilimanjaro kwenye kikao cha maofisa wa jeshi hilo anasema ajali zimeongezeka kutoka 858 Juni 2021, hadi 955 Juni mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la ajali 97, sawa na asilimia 11.3.

IGP Wambura anasema: "Takwimu zinaonyesha kuongezeka kwa ajali 97 katika kipindi hicho na tathmini tuliyoifanya imebaini kwamba ongezeko hili limetokana na mwendo kasi, kutojali na uzembe wa madereva wa magari, bajaji pamoja na bodaboda".

Kwahiyo, kutokana na ongezeko la ajali za barabarani, madereva na watumiaji wengine wa barabara wanapaswa kuwa makini wawapo barabarani ili kuepusha hasara kama hizo ambazo zinazuilika.

Wabunge nao na taasisi za umma za kusimamia sheria kama Kikosi cha Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafirishaji Ardhini (LATRA) zije na sheria na mpango kazi wa kudhibiti ajali hizo.

Pamoja na bunge kutunga sheria elimu kwa umma inayoambatana na kaulimbiu, ni muhimu kutolewa kwa wananchi wote ili kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani.

Wakati umefika Jeshi la Polisi na kitengo cha Usalama Barabarani kuanza na kutekeleza kampeni yenye kaulimbiu, "kawia ufike, jali maisha".

Kamanda Wambura anaposema mwendokasi umekuwa sababu kubwa ya ajali nyingi za barabarani ni kweli kwani baadhi ya madereva wa vyombo vya moto wanaharaka ya kufika wanapokwenda, na hivyo kuendesha kwa mwendomkali ambao mwisho wake, unagharimu maisha yao, abiria na watumiaji wengine wa barabara.

Wahenga wanasema, haraka haraka haina baraka, methali hii inasisitiza kuepuka kufanya mambo bila utimamu na uangalifu kwani mwishowe unaweza usiwe mzuri.

Kampeni ya "kawia ufike, jali maisha" iweke mkazo kwa madereva kuendesha vyombo vya moto kwa mwendo unaokubalika kisheria wa wastani wa kilometa 50 kwa maeneo hadi 80 au zaidi kwa saa ambao hata inapotokea kuwa kukatokea ajali, isiwe na athari mbaya zaidi, tofauti na ajali inapotokea wakati chombo kikiwa mwendokasi, ambapo idadi ya majeruhi, wanaofariki, uharibifu wa mali na miundombinu ni kuwa wengi na uharibifu mkubwa wa vyombo vya moto.

Kampeni isisitize kuwa ni bora kukawia kufika ila ufike salama, kuliko papara za kutaka kuwahi kwa kuendesha mwendokasi ambao ni chanzo kikubwa cha ajali. Lengo la wasafiri ni kufika salama kule waendapo bila kutokea matatizo njiani.

Kampeni itilie mkazo uendeshaji wa vyombo vya moto kwa mwendo wa wastani ambao utasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani. Endapo madereva wa vyombo vya moto kama vile magari na pikipiki watazingatia kikamilifu lengo hili la safari la kufika salama, watachukua tahadhari mapema katika uendeshaji wao kwa kuzingatia alama za barabarani.

Uhai wa watu ni jambo lenye thamani kubwa ambao haliwezi kulinganishwa na jambo jingine lolote. Wala thamani ya maisha haiwezi kulinganishwa na fedha, ardhi au dhahabu. Hivyo maisha kwanza.

Madereva wanapaswa kujali maisha yao, ya abiria na watumiaji wengine wa barabara kama vile wanaotembea , wasukuma mikokoteni na toroli, wafanyabiashara, wazee, wanafunzi na wanaofanya mazoezi.

Njia mojawapo ya madereva kujali maisha yao ni kuepuka kuendesha vyombo vya moto kwa mwendokasi, kuzungumza na simu kila wakati, kujidai kwa kutumia na kuzingatia sheria na alama za barabarani.

Vilevile, madereva hubeba abiriakupindukia wakisongana hasa kwenye mabasi -daladala na pikipiki wakiwaita mishikaki hata watu wane, kwenye bajaji watu wanajazana hata kukaa watatu kwenye kiti cha dereva ambako anatakiwa kukaa peke yake.

> Wakati umefika Jeshi la Polisi na kitengo cha Usalama Barabarani kuanza na kutekeleza kampeni yenye kaulimbiu, "kawia ufike, jali maisha".

Ni vyema madereva wakathamini imani ambayo abiria wao wamewaamini kwa kupanda katika vyombo vyao.

Madereva hawapaswi kuwa sababu ya abiria kujuta kupanda badi, boda, bajaji au kingine chochote kwa kuendeshwa kwa mwendokasi unahatarisha maisha yao.

Abiria waungane kwa pamoja kuwakemea madereva wanaoendesha magari kwa kasi na wanaofanya mambo yanayotishia usalama wao kwa kuwashauri wapunguze mwendo na kama ushauri huo utashindwa kuzingatiwa basi wapige simu moja kwa moja jeshi la polisi kikosi cha Usalama Barabarani kwa hatua zaidi.

Wamiliki kwa vyombo vya moto kwa upande wao, wanapaswa kujali maisha yao, ya abiria na watumiaji wengine wa barabara kwa kuvitengeneza na kuvirekebisha vyombo vyao mara kwa mara (service) ili kuvifanya viendelee kuwa na sifa ya kutumika barabarani.

Kwa ushirikiano wa pamoja baina ya serikali, wamiliki wa vyombo vya moto, madereva, abiria na watumiaji wengine wa barabara, ajali za barabarani zitapungua na kwamba watu wajali uhai na siyo kukurupuka kwa ajili ya kufanya chochote kingine mfano dereva anayeendesha lori anaweza kusukuma gari dogo au basi na kuumiza watu kwa kujiamini kuwa ana gari kubwa 'anawekea bodi' mambo hayo ni ujinga kuumiza watu wakati umebeba shehena.

Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

***Maoni: 0620-800462.***

# Ni wiki ya tatu William Ruto anachakata Baraza la Mawaziri

## • Kinamama hawakutajwa ugombea wenza wanamsubiri

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS WILLIAM Ruto wa Kenya wakati wowote kuanzia sasa atatangaza baraza la mawaziri wake wa kwanza na maofisa wakuu wa umma atakaosimama nao kuongoza taifa katika awamu ya kwanza ya miaka mitano ya uongozi wake.

Baraza hilo linatarajiwa kuangazia masuala ya kumaliza majanga ya uongozi wa kikabila lakini pia kuhakikisha taifa hilo linakuwa na uongozi wenye usawa wa kijinsia.

Aliyevunja rekodi kutangaza kwa haraka baraza la mawaziri ni Rais Mwai Kibaki (marehemu) aliyeacha historia kwa kutaja mawaziri lake siku tatu baada ya kuapishwa mnamo Desemba 30, 2002.

Kibaki alishinda uchaguzi wa urais Desemba 27, 2002, alikula kiapo Desemba 30 na kutaja baraza lake la mawaziri Januari 3, 2003, akiandika kwa mara kwanza historia na kuweka rekodi ya kufanya jukumu hilo kwa haraka.

Mtangulizi wa Kibaki Daniel Moi marehemu pia na Rais Kenyetta ambaye amemaliza muda wake walichukua wastani wa wiki mbili baada ya kula kiapo kutangaza timu ya baraza lao la mawaziri.

Ni siku 15 tangu Rais William Ruto achukue madaraka ya uongozi wa Kenya baada ya kuapishwa Septemba 13 jijini Nairobi.

Baraza la mawaziri linaundwa na watu 22 kwa mujibu wa katiba ya Kenya, lakini rais ana uhuru kuamua idadi ya watu anaotaka kuwateua kama makatibu wakuu na watumishi wengine wa umma wa kada ya juu wanaowajibika kusimamia wizara atakazounda.

Suala la usawa wa kijinsia halikwepeki, aidha ili kukabiliana na hoja za kuwasahau wanawake kwenye uteuzi wa mgombea mwenza kama alivyofanya mpinzani wake Raila Odinga katika uchaguzi wa urais, alimteua Martha Karua, Rais Ruto huenda akawa na angalizo kwenye uteuzi wa wanawake kwenye nyadhifa za baraza la mawaziri akiwapa nyadhifa nzito na muhimu.

Lakini hivi karibuni Naibu Rais Rigathi Gachagua katika mahojiano alidokeza kuwa huenda ikachukua wiki mbili zaidi kabla ya Dk. Ruto kutaja baraza lake la mawaziri.

Anaeleza kuwa Rais huyo anapanga kutaja Baraza lake la mawaziri pamoja na makatibu wakuu kwa pamoja ndiyo maana itachukua muda kukamilisha orodha.

Sambamba na hayo Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) kwa sasa inapokea maombi kutoka kwa watu binafsi wanaotaka kuchukua nyadhifa za Katibu Mkuu PS, na katiba ya Kenya inaruhusu kuwapo fursa hiyo.

Tume ya Utumishi wa Umma iliongeza muda hadi jana Septemba 27, ina jukumu la kupendekeza kwa Rais watu wanaotaka kuteuliwa kuwa makatibu wakuu. Tume inatakiwa kukaribisha maombi, kufanya usaili kabla ya kuwasilisha majina kwa Rais ili awaangalie ikimpendeza awateue.



Rais William Ruto, pamoja na kinamama wakati wa kampeni akiwaahidi kuwapa uongozi wa 50/50. **PICHA: MTANDAO**

> “Nimejitolea kuwa serikali ya Kenya itaunga mkono juhudi hizo zitakazoongozwa na Rais Kenyatta na ninataka kukushukuru kwa kukubali kwa ukarimu kutuunga mkono na kunisaidia katika juhudi hizo,” Rais Ruto anasema baada ya uteuzi huo.

Tayari, baadhi ya washirika wake wa karibu, ambao wamekuwa pamoja naye katika mitifuano ya kampeni, wanauangalia ukatibu mkuu na uteuzi kwenye baraza la mawaziri.

Wakati huo huo, baadhi ya mawaziri akiwamo Najib Balala Wizara ya Utalii, wanashawishi kimya kimya kuwa sehemu ya utawala unaokuja, akianza kwa kutuma ujumbe kwenye mtandao.

“Nina furaha na unyenyekevu na ninamshukuru Rais Kenyatta kwa kunipa nafasi ya kutumikia taifa. Namkaribisha Rais Ruto. Niko tayari kuhudumu katika serikali yake wakati wowote inapobidi.”

Itakumbukwa hivi karibuni amemteua mtangulizi wake Uhuru Kenyatta kuwa mjumbe wake wa amani katika Ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika ikiwamo Ethiopia.

Uteuzi unampa fursa ya ya kuendelea kuwa kiongozi (mwenyekiti) wa programu za amani za kikanda kwa niaba ya Serikali ya Kenya.

“Nimejitolea kuwa serikali ya Kenya itaunga mkono juhudi hizo zitakazoongozwa na Rais Kenyatta na ninataka kukushukuru kwa kukubali kwa ukarimu kutuunga mkono na kunisaidia katika juhudi hizo,” Rais Ruto anasema baada ya uteuzi huo.

Tangazo hilo linakuja wakati akitoa hotuba yake ya kwanza ya kuapishwa kama Rais katika Uwanja wa Kasarani jijini Nairobi, mara tu baada ya Uhuru kumkabidhi vyombo vya dola na mamlaka ya kuliongoza taifa.

Rais Ruto anasema hayo muda mfupi baada ya kula kiapo akisema serikali inatambua juhudi na diplomasia za watangulizi wake katika kukuza amani, usalama na utulivu katika eneo hilo, akiahidi kuunga mkono kikamilifu juhudi zake za kuingilia kati ili Afrika Mashariki, Pembe ya Afrika na Ukanda wa Maziwa Makuu kuwe na amani amani.

Aidha, anasema Kenya itaendelea kuwa mshirika aliyejitolea kushirikiana kupata amani, usalama na ustawi katika ukanda wa Afrika Mashariki, huku ikiwa bado ina jukumu muhimu katika diplomasia ya kimataifa .

Wakati wa uongozi wa Kenyatta ilisimamia mipango mbalimbali ya amani katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.

Uteuzi wa Kenyatta ulikuja muda mfupi baada ya vikosi vya Tigrayan kukubaliana kufanya mazungumzo na Serikali ya Addis Ababa, inayoongozwa na Waziri Mkuu Abiy Ahmed chini ya uangalizi wa Umoja wa Afrika.

> “Nina furaha na unyenyekevu na ninamshukuru Rais Kenyatta kwa kunipa nafasi ya kutumikia taifa. Namkaribisha Rais Ruto. Niko tayari kuhudumu katika serikali yake wakati wowote inapobidi.”

***CHANZO: MITANDAO***

JUKWAA LA VIONGOZI

WAZIRI MKUU NETANYAHU 'BIBI'

# Mbabe aliyeongoza serikali miaka 15 kiboko ya Iran, Palestina na Obama

• Hajatosheka uwaziri mkuu uchaguzi wa Novemba yumo

**Na Gaudensia Mngumi**

BENJAMINI Netanyahu ambaye sasa ni Kiongozi wa Upinzani na Mwenyekiti wa chama cha Likud -' National Liberal Movement,' anafahamika na wengi nje na ndani ya Israeli, kwanza akihudumu madarakani kwa miaka 15 na kumfanya kuwa waziri mkuu aliyekaa muda mrefu zaidi madarakani.

Aidha, alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza kuzaliwa Israel baada ya Azimio lake la Uhuru, akijulikana kama Benjamin au "Bibi" Netanyahu ni mwanasiasa aliyekuwa Waziri Mkuu wa tisa wa Israel kuanzia 1996 hadi 1999 na kisha 2009 hadi 2021.

Amezaliwa Oktoba, 1949 (leo ana miaka 72), katika jiji la Tel-Aviv leo ukijulikana kama Yaffo. Amekulia Jerusalem na kusoma sekondari nchini Marekani, mama yake ni Myahudi aliyezaliwa Israeli wakati baba yake Benzion Netanyahu alikuwa Myahudi wa kidini kutoka Poland, lakini pia aliishi Palestina.

Babake Netanyahu alikuwa Mzayuni 'Myahudi anayeamini kuwa Israeli ni taifa walilopewa na Mungu na kwamba ni nchi ya ahadi' akisisitiza kuwa Israeli inapaswa kuwepo pande zote mbili za Mto Yordani na kukataa maelewano na mataifa jirani ya Kiarabu.

Mnamo 1967, Bibi Netanyahu alijiunga na Jeshi la Israeli, akawa komando na msomi na kuwa nahodha wakati wa vita vya Waarabu na Israeli vya mwaka 1973.

**KUINGIA MADARAKANI**

Baada ya kutumikia Jeshi la Israel, Netanyahu alishika nyadhifa mbalimbali lakini alianza kupaa baada ya kuongoza Wizara ya Mambo ya Nje na kisha kushinda katika uchaguzi mkuu mwaka 1996.

Kabla ya hapo aliwahi kuwa Naibu Mkuu wa Ubalozi wa Israeli huko Washington, Marekani 1984, aliteuliwa kuwa Balozi wa Israeli Umoja wa Mataifa.

Alianza kupanda hadi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Likud cha mrengo wa kulia mwaka wa 1993, Netanyahu alipanga chama hicho kurudi kwenye mamlaka ya kisiasa baada ya kushindwa katika uchaguzi wa 1992.

Baadaye, alishindwa na Ariel Sharon, alikuwa mwenyekiti wa chama hicho na kuupata tena baada ya Sharon kuondoka Likud na kuunda chama cha Kadima mwaka 2005.

Amekuwa Waziri Mkuu mara nne, akifanya kampeni chini ya kauli mbiu ya "waziri mkuu mwenye nguvu", Likud ilipata viti vya kutosha baada ya kuunda muungano na vyama vya mrengo wa kulia vya Yisrael Beiteinu na Shas.





Waziri Mkuu Netanyahu (kushoto) nafasi yake inashikiliwa na Yair Lapid (kulia), lakini wote wanasubiri uchaguzi mkuu Novemba mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

Ameandika historia baada ya kushinda uchaguzi mwaka 1996, 2009, 2013 na 2015 na kuongoza kwa miaka 15. Kwa wafuasi na mashabiki wake yeye ni msemaji hodari wa masuala ya Israeli, ni mtetezi aliye tayari kuwaambia umma ukweli hata kama hawatapata raha na anayeweza kusimama dhidi ya maadui hasa Wapalestina na mataifa ya Kiarabu.

**MBABE WA 'HAPANA 3'**

Netanyahu ana msimamo wa maneno haya "hapana tatu" kwamba Hakuna Taifa la Palestina,' hakuna kurudi kwa Milima ya Golan hadi Syria' na 'hakuna majadiliano juu ya hali ya baadaye ya Yerusalemu.'

Licha ya kupinga mikataba mingi ya amani na Wapalestina, Netanyahu alitia saini Mkataba wa Mto Wye mwaka 1998 na Yasser Arafat, aliyekuwa Rais wa Mamlaka ya Kitaifa ya Palestina.

Kwa ujeuri, alijiuzulu wadhifa wa Waziri wa Mambo ya Nje, Agosti 2005, akipinga mpango wa Waziri Mkuu Ariel Sharon kujitenga na Gaza, sehemu ya ardhi ya Palestina.

**KUMCHANA OBAMA**

Ni mkosoaji wa Rais wa zamani wa Marekani Barrack Obama na uhusiano wake na Netanyahu unaelezwa kuwa ulikuwa "wa baridi", kwa sababu Obama alitaka kuvumiliana na mara kwa mara, akikosoa kuendelea kwa upanuzi wa makazi aliyoyaita 'haramu- illegal' ya Israeli kwenye ardhi ya Palestina inayoikalia kwa mabavu.

Mbabe Netanyahu akimjibu: "Tutaendelea kujenga Yerusalemu na katika maeneo yote yaliyo kwenye ramani ya maslahi ya kimkakati ya Israeli,"

KIPENZI CHA TRUMP

Rais wa zamani wa Marekani Donald Trump, alikuwa 'best' wa 'Bibi' kwanza kwa kukutana na Netanyahu, akisema ameupokea ushindi wake kama kichocheo tena umekuja baada ya miaka nane migumu katika mahusiano ya Marekani na Israel chini ya Obama.

Anayasema hayo baada ya mkutano wao huko Washington, DC uliokusudiwa kuashiria "kuweka upya" uhusiano kati ya wawili hao lakini ukitafsiriwa kuwa uliongeza ugumu kwa Wapalestina.

Mnamo Desemba 6, 2017 Trump alivunja sera za miongo kadhaa za Marekani na kutangaza kuwa Marekani inaitambua rasmi Jerusalem kuwa mji mkuu wa Israel na itaanza mchakato wa kuhamisha ubalozi wake mjini humo.

Netanyahu akaribisha uamuzi huo, na kusema ilikuwa "siku ya kihistoria" kwa Israeli. Jerusalem "umekuwa mji mkuu wa Israeli kwa karibu miaka 70", akisema katika taarifa yake.

**UBABE KWA IRANI**

Bibi ana maneno dhidi ya Iran, akihutubia Bunge la Marekani, anasema "wakati unakimbia kukabili Iran. "Tarehe ya mwisho ya kufikia lengo hili iko karibu sana," anasema.

Bibi hakuwaamini 'viongozi wa Iran wako timamu na anawaambia Iran ni kitisho kwa Israeli. Akitishia kuchukua hatua za kijeshi dhidi ya Iran mara kadhaa. "Nikiwa Waziri Mkuu, Iran haitakuwa na bomu la atomiki," anatamba mwaka wa 2013. "Ikiwa hakuna njia nyingine, Israeli iko tayari kuichukulia hatua za kijeshi.

**KASHFA RUSHWA**

Netanyahu anashtakiwa 2019 kwa rushwa akidaiwa kupokea zawadi nono ya marafiki wa mamilionea kwa madai ya kutafuta upendeleo wa udhibiti kwa matajiri wa vyombo vya habari ili kutangaza habari bora za kuwasifia.

Mashtaka dhidi yake yamekuwa suala kuu wakati wa chaguzi tatu ambazo hakuna mshindi wa wazi aliyeibuka. Alikana mashtaka mbele ya jopo la majaji watatu katika Mahakama ya Wilaya ya Jerusalem yenye ulinzi mkali, iliyoamua kwamba ushahidi katika kesi hiyo utasikilizwa baada ya uchaguzi wa mwaka huu.

**KUANGUKIA PUA**

Muda wa miaka 12 wa Benjamin Netanyahu kama Waziri Mkuu wa Israel ulifika kikomo, Juni mwaka jana serikali mpya ya mseto inayoongozwa na chama cha mrengo wa kulia cha Naftali Bennett.

Bennett angeongoza muungano wa vyama vya mrengo wa kushoto, wa kati na wa kulia, pamoja na chama kinachowakilisha raia wa Palestina wa Israeli, ambao wanachukua asilimia 21 ya idadi ya watu wa nchi hiyo. Vyama hivyo havina mambo mengi isipokuwa kutaka kumng'oa Netanyahu.

Chini ya makubaliano ya mzunguko, Bennett angekuwa Waziri Mkuu kwa miaka miwili, na kisha nafasi yake kuchukuliwa na kiongozi wa itikadi kali Yair Lapid, mbunifu mkuu wa serikali mpya.Yair Lapid anakuwa Waziri Mkuu wa 14 wa Israel akianza kazi Julai 1, 2022, lakini anayesubiri tena uchaguzi mwingine, baada ya Bunge la Israel Knesset, kupiga kura ya kujivunja na kuipeleka nchi kwenye uchaguzi mwingine Novemba kwa mara ya tano katika muda wa miaka minne

***CHANZO: MITANDAO***

# Wachambuzi wa siasa waeleza mtazamo wao kuhusu sakata hilo

**INATOKA UK. 13**

zake wakilalamikia kuvuliwa uongozi na kufukuzwa katika chama, huku akijua kuwa kuna amri ya mahakama.

Anawataka waache kupiga kelele, wasubiri maamuzi ya mahakama kuhusu amri kuzuia chama kufanya mkutano, kwamba ndicho chombo kitakachoamua ni upande gani uko sahihi kati waliofanya mkutano na wanaosubiri uamuzi wa mahakama.

"Kwa sasa malalamiko yote hayana mashiko, kinachotakiwa ni uamuzi wa mahakama, hivyo wanapaswa kuwa kimya, wakitambua kuwa walishafikisha sakata lao kwenye mkondo wa sheria," anawashauri Mwakatobe.

Aidha, anafafanua kuwa maamuzi ya wengi kikatiba ni uongozi bora, hasa kama yatakuwa yamefanyika kwa kuzingatia sheria, na kwamba mgogoro wa chama hicho kwa sasa una sura mbili.

Sura ya kwanza ni hiyo kuwapo kwa amri ya kuzuia kufanyika kwa mkutano hadi kwanza mahakama itoe hukumu na pia uhalali wa mkutano huo, ambao unalalamikiwa na upande wa Mbatia," anasema.

**MSIMAMO WA NCCR**

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa NCCR-Mageuzi aliyefukuzwa katika chama hicho Edward Simbeye, anasema upande wao anahitaji hatua mbili zichukuliwe ili kumaliza mgogoro huo.

"Kwanza kabisa tunaiamini na kuiheshimu mahakama na tunaiomba isimamie amri yake, kwani imevunjwa, kitendo kilichofanywa hakiwezi kuvumilika cha kukiuka amri ya mahakama kuzuia mkutano," anasema Simbeye.

Anaongeza kuwa wanataka kutafuta tafsiri ya kusikilizwa, kwa madai kwamba Mbatia na wengine wamefukuzwa katika chama bila kupewa nafasi ya kusikilizwa jambo ambalo hawawezi kukubaliana nalo.

Kwa mfano, ibara ya 14 ya katiba ya chama inaeleza kuwa mwanachama anapotuhumiwa anapewa siku 14 kuandika maelezo na kisha anaitwa katika kikao cha ngazi yake kujieleza," anasema Simbeye.

Anafafanua kuwa kwa mwenyekiti wa taifa, anaitwa kwenye Mkutano Mkuu kuhojiwa na kujieleza, na kwamba hilo halikufanyika huku akidai kuwa mkutano huo haukuwa na wajumbe halali.

Ajielezee mkutano utie majibu, hakukuwa na wajumbe wa mkutano mkuu, ni vijana toka Manzese na Chang'ombe Dodoma.

"Mkutano huo ulijaa wahuni kutoka Manzese na wengine wa Chang'ombe Dodoma, sisi tunaheshimu mahakama na tunasubiri hukumu ya shauri namba 150 la mwaka 2022, ambalo tuliweka kufuatia mgogoro Mei mwaka huu kama kikao wakati huo kilichotusimamisha kilikuwa halali au la," anasema.



Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa, ofisi yake bado haijazungumzia mgogoro wa NCCR-Mageuzi, uliofikishwa kwake miezi kadhaa iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

**UONGOZI NCCR-MAGEUZI**

Mbatia ni mwanaharakati ambaye tangu mwaka 1992, baada ya kuondolewa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alijiunga na vuguvugu la mabadiliko ya demokrasia nchini na akawa mmoja wa waasisi wa NCCR - Mageuzi.

Mbatia ni mtu wa kujituma na chama kilimchagua kuwa mwenyekiti wa kwanza wa vijana wa chama hicho kuanzia mwaka 1992 hadi 1994.

Amewahi kuwa Katibu wa Idara ya Oganaizesheni na Uchaguzi na kuanzia mwaka 2000 hadi leo, alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa NCCR kazi aliyoifanya kwa miaka 22 na sasa analazimishwa kung'atuka na wanachama wenzake, jambo ambalo hajalikubali akisubiri mahakama itoe maamuzi.

Mgogoro wa chama hicho ulianza Mei mwaka huu wakati Mbatia , alipokataa kukaa kando ya nafasi yake ya uenyekiti na kuanzia hapo mgogoro haujawahi kuzima.

Kamati Kuu ya NCCR- Mageuzi, iliwasimamisha kujihusisha na shughuli zozote ndani ya chama Mbatia na sekretarieti yake yote, kazi iliyoanzishwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya NCCR Mageuzi na Mwenyekiti wa Azimio la Kumsimamisha Mbatia, Joseph Selasini.

Akieleza sababu za kumuondoa madarakani anasema uongozi wa Mbatia na wenzake unasimamishwa kwa sababu Mbatia alifanya majukumu ambayo chama hicho hakikubaliani nayo na kuishutumu timu yake kuwa imekwenda kinyume na katiba ya chama chao ikiwa ni pamoja na kuwagombanisha wanachama kadhalika kutumiwa kisiasa.

## CHEMSHABONGO NA -00 7 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com


Dondoo: Kulia
5. Rais wa Palestina aliyefia Ufaransa
6. taarifa
8. tunda la mchungwa
11.faini
12.hekta 0.4
15.mkoa unaomaanisha kilele
16.osha nguo 18.choma mkate
19.kansa


Chini:
1. mnyama kama paka mwitu ambaye hukamata kuku
2. Walozi
3. siha
4. mto unaomwagwa maji yake bahari ya hindi nchini Kenya
7. mtu asiye na mali
9. bila ya shaka
10.kilimi, mtapa
13.nyanyua
14.isiyozaa 16.toa msaada
17.vunja kanuni za nchi




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| SARAKASI | UTU |
| AINISHA | AGO |
| AALIMU | HA |
| INNA | GOMA |
| IMAMU | GUNIA |
| ALUMNI | OSAMA |
| NAKALA | UMA |
| USALAMA | BA |
| UBABE | RAIS |
| MAKALI | UANGA |
| ALAMINA | HASI |
| EGESHWA | DUMA |
| MAKASHA | USO |







## Wavunja nyumba ya kikongwe wakimtuhumu kwa uchawi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAKAZI wa Kijiji cha Ibula kilichoko Kata ya Kiwira katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wamevunja nyumba ya mwananchi mwenzao na kuidhuru mifugo yake wakimtuhumu ni mchawi.

Mwananchi aliyevunjiwa nyumba ni Lucia Kasebele (54), wananchi hao walikuwa wanamtuhumu kuwa amekuwa akisababisha vifo vya baadhi ya watu kwenye kijiji hicho akiwamo kijana.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alisema mbali na wananchi hao kubomoa makazi ya bibi huyo, pia walichoma moto baadhi ya maeneo ya nyumba zake na kuivunja miguu baadhi ya mifugo.

Alisema kitendo walichokifanya wananchi hao ni cha ukatili wa kijinsia kutokana na aliyefanyiwa vitendo hivyo kuwa mwanamke ambaye hakuwa na uwezo wa kujitetea, hivyo aliagiza hatua kali zichukuliwa dhidi ya wahusika.

Alisema katika wilaya hiyo vitendo vya ajabu vimekuwa vikiongezeka kila siku hali ambayo inachafua taswira ya wilaya hiyo ambayo imekuwa kivutio cha wawekezaji kutokana na kuwa na hali nzuri ya hewa.

Pia aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuacha kujichukulia sheria mkononi pamoja na kuendelea kushikilia imani potofu kwa maelezo kuwa zinazua uhasama miongoni mwa wananchi.

Diwani wa Kata ya Kiwira, Michael Mwamwembe, alisema alipata taarifa asubuhi kwamba kuna tukio la wananchi kuvamia nyumba ya mama huyo na kuibomoa hali iliyomfanya akimbie haraka kwenda kuangalia.

Alisema kabla hajaondoka aliwasiliana na polisi ambao walimwambia kwamba wanaelekea katika eneo hilo na kwamba alipofika alikuta nyumba zimebomolewa na mifugo imejeruhiwa lakini wahusika wamekimbia.

Mwamwembe alisema walipofuatilia walibaini kuwa wananchi hao walikuwa wanamhisi mama huyo kuwa ni mchawi na walitumia mbinu hiyo kama njia ya kumfukuza kwenye eneo hilo.

Agness Kasebele ambaye ni mmoja wa watoto wa bibi huyo alisema alipopata taarifa hiyo alifika na kukuta nyumba imevunjwa na mifugo baadhi imevunjwa miguu.

# Mifugo inavyohatarisha uhai wa ikolojia ya Bonde la Ihefu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

HALI ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha bado ni tete kutokana na makundi ya mifugo kuendelea kuchungwa ndani ya Bonde la Ihefu lenye ardhi oevu ambalo lipo ndani ya hifadhi hiyo.

Uvamizi huo pia umesababisha uharibifu wa mazingira ndani ya hifadhi, hivyo kuiweka ikolojia ya hifadhi hiyo kuwa katika hatari ya kupotea.

Juzi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo alifanya ziara katika eneo hilo kwa lengo la kuangalia uharibifu wa mazingira uliofanywa na wafugaji, aliwataka wafugaji hao kuondoka kwa hiari.

Katika ziara hiyo, Waziri Jafo akiwa ameongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya na maofisa wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), walitumia ndege maalumu kufanya ukaguzi katika bonde hilo, walishuhudia idadi kubwa ya mifugo.

Waziri Jafo alisema mbali na mifugo hiyo kuonekana katika makundi makubwa lakini wafugaji hao wamejenga mazizi pamoja na nyumba za kuishi ndani ya bonde hilo, hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

**Idadi ya mifugo iliyoko ndani ya bonde hilo ni mingi kuliko hata wanyamapori walioko ndani ya hifadhi hiyo jambo ambalo linahatarisha uwepo wa hifadhi hiyo.**

Alisema hali waliyoishuhudia ndani ya eneo hilo isipodhibitiwa mapema Mto Ruaha Mkuu unaweza ukapotea na kusababisha miradi ya maendeleo inayotegemea mto huo ukiwamo Mradi wa Bwawa la kuzalisha Umeme la Nyerere kukwama.

Alisisitiza kwamba viongozi wakuu wa nchi wameelekeza mazingira kuhifadhiwa ikiwamo chanzo cha Mto Ruaha na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kwamba aliamua kwenda kufanya ziara hiyo baada ya kuona baadhi ya picha kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari.

Jafo aliwapongeza viongozi wa Mkoa wa Mbeya na wa TANAPA kwa kuanzisha operesheni maalumu ya kuiondoa mifugo hiyo na kwamba operesheni hiyo inatakiwa iendelee mpaka wahakikishe mifugo yote imeondolewa.

Mkuu wa Hifadhi ya Ruaha, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meng'ataki, alisema kwa sasa wanaendelea na operesheni ya kuiondoa mifugo hiyo ambayo walianza tangu Septemba 13, mwaka huu.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Julai 2021 mpaka sasa wamekamata mifugo zaidi ya 16,000 katika matukio 60 na kwamba zaidi ya wafugaji 190 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria.

Ole Meng'ataki alisema katika kipindi hicho cha mwaka mmoja wamekusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.6 ambazo zinatokana na faini ambazo wafugaji hao wamekuwa wakitozwa.

"Tunawatoza Sh. 100,000 kwa kila mfugo unaokamatwa lakini uzoefu tulionao ni kwamba wafugaji hawa wamekuwa jeuri sana, unaweza ukakamata mifugo hata 800 kwa siku lakini kufika kesho yake wanakuwa wamelipa faini na wanakuja kuchukua mifugo yao," alisema Ole Meng'ataki.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema idadi ya mifugo iliyoko ndani ya bonde hilo ni mingi kuliko hata wanyamapori walioko ndani ya hifadhi hiyo jambo ambalo linahatarisha uwepo wa hifadhi hiyo.

Alisema askari wa TANAPA wanaofanya operesheni ya kuondoa mifugo hiyo wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa maelezo kuwa wanaswaga umbali wa zaidi ya kilomita 50 kutoka hifadhini mpaka kwenye kambi ya Ikoga Mpya.

Hata hivyo Waziri Jafo aliahidi kurejea katika eneo hilo na mawaziri wenzake wanaohusika na masuala mbalimbali kwa ajili ya kujadiliana namna sahihi ya kuiondoa mifugo hiyo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamini Kuzaga, akionyesha kwa waandishi wa habari jana baadhi ya vifaa walivyokutwa navyo vijana wanne waliokuwa wanawatapeli wananchi kwa kutumia majina ya wasanii maarufu na viongozi wa serikali kwa njia ya mtandao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanne mbaroni tuhuma utapeli wananchi mitandaoni

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kuwatapeli wananchi kupitia mitandao ya kijamii wakitumia majina ya wasanii na viongozi wa serikali kwa kuwaahidi mikopo kwa gharama nafuu.

Aidha, vijana hao wanadaiwa kuwa walikuwa wanawaahidi wananchi hao kuwapatia ajira kwenye vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama ikiwamo Jeshi la Polisi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) endapo watatoa pesa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamini Kuzaga aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni mbalimbali ambazo jeshi hilo limekuwa likizifanya ndani ya mkoa huo.

Aliwataja vijana hao kuwa ni Ezekia Simon (19), Amasha Mbeyale (24) Shaban Mindu (28) na Benny Sanga (28) wote wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ambao walikutwa na wakiwa na nyaraka mbalimbali walizokuwa wanazitumia. Kamanda Kuzaga alisema watuhumiwa hao walikuwa wanawatapeli wananchi kwa kutumia mitandao ya kijamii hasa facebook ambako walikuwa wanatengeneza machapisho ya uongo yanayoonyesha kwamba wao wanatoa mikopo.

"Wamekuwa wakitumia majina ya msanii Nandy na Jokate Mwegelo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam jambo ambalo baadhi ya watu walikuwa wanawaamini na kuwatumia fedha," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema vijana hao walikuwa wanawatapeli pia wananchi kwa kuwatumia ujumbe mfupi wa simu zinazosema 'Nafasi za kazi za JKT kama una mtoto wako wasiliana nasi' na 'tuma pesa kwenye namba hii'.

Alisema watuhumiwa walipopekuliwa walikutwa na vitu mbalimbali ikiwamo laini 36 za simu za mitandao mbalimbali, simu za mkononi saba, nyaraka mbalimbali, picha za watu mbalimbali na machapisho mbalimbali.

Kamanda Kuzaga alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea na watuhumiwa watafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.



# Kamishna wa Elimu ataka taarifa ukatili kwa watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia amewataka watoto kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili wa kijinsia unaofanywa na watu walio karibu nao kwa kuwa umekuwa ukikatisha ndoto zao.

Venance Manori alitoa rai hiyo jana kwenye mahafali ya tatu ya darasa la saba katika Shule ya Msingi St. Mary's - Dodoma.

Alisema watoto wa kike hawapaswi kukubali vitendo vya kikatili vinavyokatisha ndoto zao za masomo walizojiwekea.

"Msikubali ndoto zenu kukatishwa na mtu yeyote, siku hizi ukatili unafanyika na watu wa karibu katika familia zenu, anaweza kuwa mjomba, kaka au mama yako, usikubali ndoto zako kukatishwa," aliagiza.

**Hakuna kitakachowapa mafanikio katika maisha yao zaidi ya kusoma kwa bidii na kuwa watiifu hata huko watakapokwenda katika ngazi zingine za masomo.**

Alisema kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo, yeyote atakayefanyiwa vitendo vya ukatili anapaswa kuripoti katika ngazi mbalimbali ikiwamo kwenye familia yake, lakini akawa na angalizo kwamba taarifa zitolewa kwa watu wanaoaminika.

"Msikae kimya mnapofanyiwa vitendo vya ukatili katika familia zenu, toeni taarifa ili msije katishwa ndoto zenu kutokana na ukatili unaofanywa na watu wasiokuwa na ubinadamu ndani yao," aliagiza.

Kiongozi huyo aliwataka wazazi kuacha kuwa sehemu ya kukatisha ndoto za watoto wao wa kike kwa kuwafanyia vitendo vya ukatili ikiwamo kuwaozesha katika umri mdogo.

"Leo hii hapa nimeambiwa wahitimu wa darasa la saba mwaka huu wasichana ndiyo wengi kuliko wavulana lakini unashangaa kadri watakavyozidi kwenda juu ndivyo wanavyopungua.

"Inabidi wingi huu wa watoto wa kike uendelee hata katika ngazi za juu za masomo tuache kuwafanyia ukatili ambao unawanyima hata haki yao ya msingi ya kusoma kwa kuwaozesha katika umri mdogo," alisema.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Benard Maalafu aliwataka wahitimu hao wa darasa la saba kuongeza juhudi katika masomo yao na kujiandaa vizuri katika mtihani wao wa kuhitimu darasa la saba mwaka huu.

Alisema hakuna kitakachowapa mafanikio katika maisha yao zaidi ya kusoma kwa bidii na kuwa watiifu hata huko watakapokwenda katika ngazi zingine za masomo.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Tibe Rwakatare alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali kwenye sekta ya elimu, wanapanga kuboresha utoaji wa elimu mkoani hapa ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa shule ya kisasa ya sekondari mwakani.



Mwenyekiti wa soko la wafanyabiashara wadogo 'machinga' la mitumba Nyerere Square, jijini Dodoma, Jackson Samweli, akizungumza na wamachinga kuhusu utaratibu wa kugawiwa vizimba vya kufanyia biashara zao kwenye soko jipya la wazi la Machinga Complex katika Barabara ya Bahi, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**.

# Jiji lashtuka uchakavu miundombinu ya soko

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeingia makubaliano na uongozi wa Soko la Mwembe kufanya ukarabati wa miundombinu na ujenzi wa vibanda vya wafanyabiashara vitakavyoendana na hadhi ya makao makuu ya nchi.

Makubaliano hayo yamefikiwa kutokana na soko hilo kongwe lenye zaidi ya miaka 35 kukabiliwa na uchakavu wa miundombinu mbalimbali pamoja na ujenzi holela wa vibanda.

Mwenyekiti wa soko hilo, Kimolo Rajabu, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tayari wameshaingia makubaliano na jiji kuanza kufanya ukarabati wa soko hilo.

"Tayari tumeshakutana na viongozi wa jiji na kutueleza nini wanataka kufanya na sasa wafanyabiashara tumekubaliana na mapendekezo hayo ili kutoa fursa kwa soko letu kuboreshwa ili liendane na hadhi ya makao makuu," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema jiji limeshaandaa ramani ambayo inaonyesha vibanda vitakavyojengwa pamoja na miundombinu mingine.

Rajabu alisema kukamilika kwa ukarabati wa soko hilo kutasaidia kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato kutokana na idadi kubwa ya wafanyabiashara, zaidi ya 200 waliopo sasa kati soko hilo.

Pia alisema ukarabati huo utasaidia wafanyabishara kutambulika kutokana na usajili watakaofanyiwa ambao utawasaidia kuaminika na taasisi za kifedha.

"Hivi sasa kutokana na namna lilivyo soko letu, ni vigumu mtu kukopesheka lakini mara baada ya kufanyika kwa maboresho haya na taasisi za fedha zitapata wateja wengi ambao watahitaji mikopo na wenye maeneo ya kuwadhamini," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na soko hilo kuwa na wafanyabiashara wengi wa kuku tayari wameshatafuta mwekezaji wa kujenga machinjio ya kisasa ili kuongeza thamani ya bidhaa hiyo.

"Hivi sasa biashara ya kuku katika soko hili ni kubwa sana, kuna wafanyabiashara wa kuku zaidi ya 90 na hakuna machinjio na hali hii ya uchinjaji holela si salama kiafya lakini tunatarajia muda mfupi ujao kuwa na eneo safi, zuri na salama kwa wafanyabiashara na walaji," alisema Rajabu.

# Wadau waanza kikao kujadili mitaala elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa elimu wameanza kikao chao cha ndani kujadili rasimu ya mapitio ya mitaala na sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 ili kutoa mwelekeo wa elimu ya Tanzania.

Pamoja na mambo mengine, wadau watapokea mapendekezo yaliyoandaliwa na timu zilizokusanya maoni ikiwamo hatma ya utekelezaji wa sera ya elimu inayotaka elimu ya lazima kuwa miaka 10 na kubainisha gharama za kufanya mageuzi kwenye sekta ya elimu nchini.

Akifungua mkutano huo juzi jijini hapa, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema wamekutana kujadili rasimu ya mapitio ya sera na mitaala kwa kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakikusanya maoni.

"Kwa mara ya kwanza tunakutana kujadili tukiwa na rasimu ya sera na mitaala. Kwa muda mrefu tumekuwa tukikutana na kukusanya maoni, sasa timu zetu zinazopitia sera na mitaala zina rasimu, kwa hiyo tuna kitu cha kufanyia majadiliano yetu," alisema.

Waziri huyo alisema maoni mengi yamepokewa kuhusu sera na mitaala na wanaendelea kuyapokea.

"Kazi ya sera hatukuwaambia waandike sera mpya, hatujaomba kutunga sera mpya, tumewaambia wachukue Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, waipitie waone ni nini kibaki vilevile au nini kibadilishwe kama mabadiliko ni makubwa sana lazima tuanze na sera mpya.

"Kama mabadiliko ni kidogo na ya msingi, basi tunatoa mabadiliko mapya ya sera yanaunganishwa yale yote yanayopaswa kuongezwa," alisema.

Kuhusu mitaala, alisema wanaipitia na kubainisha kuwa ni suala la kiufundi lakini kwa sasa linaangaliwa na kila mtaalamu na wenye uamuzi kulingana na matakwa ya wananchi.

Alisema kwenye sera ya mwaka 2014 ipo lakini suala hilo halijatekelezwa.

"Tutaambiwa tunahitaji kuwa na walimu wangapi ili tunapofanya mabadiliko tujue tunatumia njia gani kuboresha idadi ya walimu na vitendea kazi," alisema.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein, alisema mkutano huo ni muhimu kwa hatma ya maendeleo ya nchi kwa kuwa watakapokosea sera na mitaala watakuwa wamelikosea taifa.

"Lazima tujiulize kuwa somo au mada zinazofundishwa zinaendana na mahitaji yanayohitajika ya ulimwengu wa karne ya 21? Tujiulize inakuwaje mtoto hadi anamaliza elimu ya sekondari au chuo kikuu hana ujuzi wowote na anategemea kupata kazi ya kuajiriwa?" alihoji.





# Vijana 109,000 hawana ajira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imesema idadi ya vijana wasiokuwa na ajira imefikia 109,868 sawa na asilimia 27.4 kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alibainisha hayo wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi jana alipojibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari aliyetaka kujua takwimu sahihi za vijana wasiokuwa na ajira Zanzibar.

Alisema asilimia 27.4 ya vijana hawana ajira na serikali imechukuwa hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira ikiwamo kuibua miradi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Aliitaja miradi hiyo ni pamoja na fedha za UVIKO-19 ambazo zimetengwa na Serikali ya Zanzibar Sh. bilioni 36 kwa ajili ya kuwawezesha makundi mbalimbali ikiwamo vijana kujiajiri.

Alisema katika fedha zilizotengwa, zipo kwa ajili ya vijana waliojikita katika ujasiriamali wa kuzalisha mazao ya baharini ikiwamo ufugaji wa samaki, jongoo wa baharini na kaa.

Waziri huyo alisema kuwa zaidi ya mabwawa 100 yanatarajiwa kujengwa katika mradi wa kuwawezesha vijana kupata ajira katika uchumi wa buluu wa mazao ya baharini.

"Mheshimiwa Naibu Spika, tunalifahamu tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wetu ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukuwa juhudi mbalimbali kukabiliana na tatizo hilo ikiwamo kutenga fedha zitakazotumiwa kwa vijana kwa ajili ya kazi za ujasiriamali na uwekezaji wa miradi midogo na kujiajiri," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imeanza kujenga vituo vikubwa kwa ajili ya kuzalisha ajira kwa vijana katika kazi mbalimbali zikiwamo za mikono.

# Sheria ya Usalama Barabarani kufumuliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imesema ipo katika mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Usafiri Barabarani ya Mwaka 2003 ambayo itaanzisha faini za papo kwa papo ili kudhibiti ajali za kizembe zinazofanywa na madereva.

**Yamekuwapo matukio ya ajali nyingi ambazo zingine huwa za kizembe zinazosababishwa na madereva wanaopuuza sheria.**

Katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Khalid Salum Mohamed, alibainisha hayo alipotoa ufafanuzi na kujibu hoja za wajumbe waliochangia Taarifa ya Kamati ya Mawasiliano, Nishati na Ardhi ya Baraza la Wawakilishi iliyowasilishwa na Mwenyekiti wake, Yahya Abdalla Rashid.

Dk. Mohamed alisema yamekuwapo matukio ya ajali nyingi ambazo zingine huwa za kizembe zinazosababishwa na madereva wanaopuuza sheria.

Alisema njia pekee ya kukabiliana na matukio hayo ni kufanya marekebisho ya Sheria za Usalama Barabarani na kuweka utaratibu wa adhabu za faini za papo kwa papo ambazo matarajio ya wizara zitadhibiti makosa ya kizembe.

Alisema utaratibu wa adhabu kama hizo ni maarufu na unatumika katika nchi na hata Tanzania Bara (madereva bajaj na pikipiki) na umesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti matukio ya ajali za barabarani.

Alisema utaratibu kama huo ni mzuri na unapunguza na kuziba mianya ya rushwa ambayo hufanywa kati ya madereva na askari wa Jeshi la Polisi ambao ndiyo wanaosimamia mwenendo wa usalama barabarani.

"Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ipo katika hatua za mwisho za kufanya marekebisho ya sheria hiyo ambayo yataanzisha adhabu ya faini za papo kwa papo, hatua ambayo tunaamini itapunguza ajali," alisema.



Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Leila Mohamed Mussa, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kesi za udhalilishaji kijinsia zawapeleka jela

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KESI 14 za udhalilishaji zinazohusu makosa ya kutorosha, kubaka na kuingilia kinyume cha maumbile zimetolewa hukumu katika mahakama mbalimbali za Unguja kwa mwezi Agosti mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Naibu Mkurugenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mwanamkaa Muhammed Abdulrahman, kesi hizo zimetolewa hukumu katika mwezi tajwa.

Taarifa hiyo iliwataja washtakiwa waliotiwa hatiani katika Mahakama ya Mkoa Vuga kuwa ni pamoja na Haji Ali Haji (28), mkaazi wa Kwarara, Unguja aliyetiwa hatiani kwa kosa la kubaka na kuhukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 20 jela.

Alisema washtakiwa wengine ni Omar Juma Kombo (33) wa Kwarara, Unguja aliyetiwa hatiani kwa kosa la kunajisi mtoto wa kiume na kuhukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 14; na Juma Mohamed Kheir (32), mkaazi wa Chuini ametiwa hatiani kwa makosa mawili ya kutorosha (kifungo cha miaka saba gerezani) na kumwingilia mtoto wa kike kinyume cha maumbile (kifungo cha miaka 14 gerezani). Adhabu zinakwenda sambamba.

Alisema mahakama hiyo pia imemhukumu Abdulkadir Zuberi Mbarouk (27), mkaazi wa Melinne, Unguja kutumikia kifungo cha miaka 10 kwa kosa la kubaka; Mvita Khatibu Mvita (43) wa Mtoni Kijundu, amehukumiwa kifungo cha miaka 10 jela kwa kosa la kutorosha na miaka 14 kwa kosa la kulawiti, adhabu zinaenda sambamba.

Pia alisema Haji Hassan Haji (29) wa Mpendae ametiwa hatiani kwa kosa la kutorosha (kifungo cha miaka 10), kosa la kubaka (kifungo miaka 20) na kuingilia kinyume cha maumbile mtoto wa kike (kifungo miaka 20) na adhabu zinaenda sambamba wakati Seif Juma Nassoro (29) wa Miembeni ametiwa hatiani kwa kosa la kubaka (kifungo cha miaka 10) na kuingilia kinyume cha maumbile (kifungo miaka 10).

Alisema Ali Mselem Khamis (22), mkaazi wa Mwanakwerekwe, ametiwa hatiani kwa kosa la kumwingilia maharimu na kuhukumiwa kifungo cha miaka 25 jela na Yussuf Hamad Ndaro (51) wa Bububu Kijichi ametiwa hatiani kwa kosa la kubaka na kuhukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 10 jela.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa Mahakama ya Mkoa Mwera imewatia hatiani kwa makosa hayo ya udhalilishaji Ramadhan Juma Ujadi (22) wa Kwambani na kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili jela kwa kosa la kutorosha, kosa la kubaka (kifungo miaka 27) na kosa la kuingilia kinyume cha maumbile (kifungo miaka 10), adhabu zinakwenda sambamba.

Damas Madama Ndombole (55) wa Ndagaa Dongogwe ametiwa hatiani kwa kosa la kubaka na kuhukumiwa kutumikia kifungo cha miaka saba na Haji Mlenge Haji (24) wa Ndijani amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka miwili kwa kosa la kutorosha na miaka 20 kwa kosa la kubaka, adhabu zinaenda sambamba.

Vilevile, Mahakama ya Mkoa Mahonda imewatia hatiani mshtakiwa Moh'd Hassan Ali (51) wa Makadara kutumikia kifungo cha miaka saba kwa kosa la kubaka na Juma Makame Mwinyi (40) wa Mahonda kutumikia kifungo cha miaka mitatu kwa kosa la kutorosha na kosa la kubaka kifungo cha miaka saba, adhabu zinakwenda sambamba.

# Wenye ulemavu ngozi waomba mafuta kushuka

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA wa maduka ya dawa nchini wameombwa kupunguza bei ya mafuta ya kinga ya mionzi ya jua kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) ili kuwasaidia kumudu gharama za kuyanunua.

Kadhalika, watu wasiokuwa na ulemavu wa ngozi wametakiwa kujiepusha kutumia mafuta hayo hayo kwa kuwa yanaweza kuwasababishia saratani ya ngozi.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino (TAS) wilayani Kahama, Nisha Phabian, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema mafuta hayo yamekuwa yakiuzwa kwa Sh. 40,000 kwa chupa bei ambayo inawashinda watu wenye mahitaji hayo badala yake wanaamua kutumia mafuta ya kawaida.

**Baadhi yao wamekuwa wakipata shida kupata mafuta kinga na wakiyapata gharama yake iko juu.**

Phabian aliongeza kuwa ili kuondokana na madhara kwa kutumia mafuta ya kawaida ni vyema wafanyabiashara wa maduka ya dawa wakapunguza bei hadi kufikia Sh. 15,000 na yawe yanauzwa kila sehemu ili wanaoishi vijijini wayapate kwa urahisi.

"Tunaomba serikali katika bajeti yake ya kila mwaka kutenga fedha kwa ajili ya kununulia mafuta kinga ya ngozi na kuyauza katika maduka ya dawa yanayopatikana vituo vya afya na hospitali kwa gharama nafuu ili kila mmoja wetu ayapate kwa urahisi na kulinda ngozi yake," alisema.

Nisha alisema yeye anaagiza mafuta hayo kutoka Dar es Salaam kupitia kwa rafiki yake ambaye ni mlemavu wa ngozi na kwamba huwa anamtumia chupa moja hadi mbili kulingana na fedha aliyo nayo.

Naye Leokadia Charles, ambaye ni mlemavu wa ngozi, mkazi wa Halmashauri ya Msalala alisema baadhi yao wamekuwa wakipata shida kupata mafuta kinga na wakiyapata gharama yake iko juu.

Charles alisema kila baada ya miezi sita wamekuwa wakihudhuria kliniki ya ngozi na kuangaliwa hali ya ngozi zao zilivyo na wengi wanaofika huwa zinakuwa zimeharibiwa na jua.

Alisema mwenye ulemavu wa ngozi hatakiwi kufanya kazi juani na kwamba kutokana na ugumu wa maisha, wanajikuta wakifanya hivyo na kusababisha ngozi zao kuharibika.




Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba (kulia), akikabidhi msaada wa magodoro 10 kwa mwanzilishi wa kituo cha kulelea watoto Yatima cha Teenagers Foundation Tanzania, Elias Fue, eneo la Majengo Mapya, Kata ya Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mbunge Makamba awakumbuka yatima

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Salome Makamba, ametoa msaada wa magodoro na vitanda katika kituo cha watoto yatima cha Teenagers Foundation Tanzania Orphanage Centre, kilichoko eneo la Majengo Mapya, Kata ya Ngokolo katika Manispaa ya Shinyanga.

Makamba alitoa msaada huo juzi ikiwa sehemu ya kuunga mkono juhudi za wadau katika kusaidia watoto wenye uhitaji ili waishi katika mazingira mazuri pamoja na kusoma kwa bidii na kutimiza ndoto zao.

Alisema kusaidia wenye uhitaji ni kufungua milango ya neema na kupata thawabu kwa mwenyezi Mungu na kuwataka wadau mbalimbali wa maendeleo na wenye nafasi kujenga utamaduni wa kusaidia watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu.

"Nimeguswa na kituo hiki cha kulelea watoto yatima hapa Majengo Mapya, hivyo nikaona ni vyema na mimi nitoe mchango wangu wa kuwasaidia watoto hawa kwa kuwapatia vitanda vitano pamoja na magodoro 10 ili walale sehemu nzuri," alisema Makamba.

"Kwa nafasi niliyo nayo nitaendelea kuwatafutia wadau mbalimbali ili kuendelea kuwatatulia shida ambazo bado zinawakabili watoto hawa ikiwamo sehemu nzuri ya kujisomea na kuwapatia vitabu ili wasome na kutimiza ndoto zao," aliongeza.

Clemensia Clement, ambaye ni mtoto anayesoma kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Ngokolo, alimshukuru mbunge huyo kwa msaada wake ambao alisema umewaondolea shida ya kulala chini.

Naye mwanzilishi wa kituo hicho, Elias Fue, alimshukuru mbunge huyo kwa kuitikia maombi yao na kuamua kuwaunga mkono katika kutatua baadhi ya shida ambazo zinawakabili.

# Mwanafunzi afariki kwa kuzama ziwani

**Eliza Selemani,** SENGEREMA

MARIAM Masumbuko (9) anayesoma darasa la pili katika Shule ya Msingi Majengo, amefariki dunia kwa kuzama katika Ziwa Victoria wakati akiogelea na wenzake.

Tukio hilo lilitokea katika kitongoji cha Irenza B, mwaloni Kijiji cha Irenza Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Irenza, Semeni Fidel, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa lilitokea juzi majira ya saa 9:00 alasiri.

Kutokana na tukio hilo, mwenyekiti huyo aliwataka kuwa makini na watoto wao na kuwazuia kuogelea ziwani kwa kuwa ni hatari kwa maisha yao.

Naye baba mzazi wa mtoto huyo, Masumbuko Laurent, alisema alipewa taarifa ya mtoto wake kuzama akiwa kazini kwake majira ya jioni.

Alisema aliondoka kwenda kazini na kuwaacha watoto wake wakiwa nyumbani wanajiandaa kwenda kanisani.

Baadhi ya majirani waliozungumza na Nipashe walisikitika na kusema kuwa wanatakiwa wawe waangalizi kwa kila mtoto kwenye maeneo yao.

Polisi wa kituo cha Nyakarilo wilayani Sengerema walifika katika eneo la tukio na kuchukua mwili wa marehemu kisha kuupeleka nyumbani kwao kwa ajili ya taratibu za maziko.

**Baadhi ya majirani waliozungumza na Nipashe walisikitika na kusema kuwa wanatakiwa wawe waangalizi kwa kila mtoto kwenye maeneo yao.**

HABARI KIMATAIFA

## Wagombea urais wajiandaa kampeni Nigeria

**ABUJA, Nigeria**

SERIKALI ya Nigeria inatarajia kutangaza kuanza kwa kinyang'anyiro cha uchaguzi wa urais leo na kwamba wagombea 18 wana matumaini ya kuchukua uongozi wa nchi hiyo yenye watu wengi zaidi barani Afrika.

Kwa mujibu wa RFI, wagombea wakuu wawili walioko katika kinyang'anyiro hicho ni Atiku Abubakar wa Chama cha People's Democratic Party (PDP) na Bola Ahmed Tinubu wa Chama tawala cha Congress of Progressives (APC) ambao watamrithi Rais wa nchi hiyo, Muhammadu Buhari ambaye atakamilisha mihula yake miwili hivi karibuni.

Ilielezwa kuwa taifa hilo kubwa la Afrika Magharibi ambalo liliingia katika mfumo wa demokrasia mwaka 1999, wagombea wa vyama viwili vikuu hawaonekani kuwa na uhakika wa kuweza kushinda katika awamu ya kwanza ya uchaguzi.

Prof. Dapo Thomas wa Chuo Kikuu cha Lagos, alisema tofauti na chaguzi sita zilizopita, uchaguzi wa mwaka 2023 hautakuwa na wagombea wawili.

Tinubu na Abubakar, wote wanatajwa kuwa wana umri zaidi ya miaka 70 na matajiri wa kupindukia, watalazimika kuwashawishi wapigakura katika nchi ambayo asilimia 60 ya watu ni chini ya miaka 25.

Mgombea mwingine Peter Obi wa Chama cha Labour na gavana wa zamani, ametajwa kuibuka miezi ya karibuni huku akiungwa mkono na vijana pamoja kuwa na wafuasi wengi mtandaoni.

Inasema jumla ya wagombea 18 akiwamo mwanamke mmoja watashiriki upigaji kura utakaofanyika Februari 25, 2023, ambapo wananchi wa Nigeria pia watachagua wawakilishi wao bungeni.

Kampeni hiyo ambayo itafunguliwa rasmi leo itachukua muda wa miezi mitano, ambapo wachambuzi wa siasa walisema inaweza kuzidisha mizozo ndani ya vyama na migawanyiko katika nchi ambayo tayari ina mgawanyiko mkubwa kati ya waislamu wa kaskazini na wakristo wa kusini.

MGAWANYIKO KASKAZINI NA KUSINI

Mojawapo ya mada kuu ya uchaguzi wa rais wa 2023 ni hali maalum ya Nigeria kugawa maeneo, kulingana na makubaliano hayo ya kimya kimya, uchaguzi wa urais lazima ubadilishwe kila mihula miwili kati ya mgombea kutoka kaskazini, hasa Mwislamu na kutoka kusini Mkristo.

Ilielezwa kuwa kanuni hiyo inalenga kudumisha uwiano katika nchi yenye makabila zaidi ya 250 na ambapo mivutano kati ya jamii ni ya mara kwa mara.

Nigeria imekuwa ikipitia mzozo mkubwa wa kiuchumi tangu janga la Corona pamoja na mashambulizi ya Russia nchini Ukraine, ambayo yamesababisha bei ya chakula na mafuta kupanda juu.

**RFI**

# Wakili aliyejisalimisha ICC Kenya amefariki dunia

**NAIROBI, Kenya**

WAKILI Paul Gicheru, ambaye alishtakiwa katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Jinai (ICC) kwa madai ya kuwahujumu mashahidi ambao walikuwa watoe ushahidi dhidi ya Rais wa Kenya William Ruto amefariki dunia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na BBC, vyombo vya habari nchini Kenya viliripoti kuwa Gicheru alikutwa amefariki nyumbani kwake mtaa wa Karen jijini Nairobi Jumatatu usiku, ambapo chanzo cha kifo chake hakikubainishwa.

Gazeti la Daily Nation linaripoti kuwa familia yake imethibitisha kifo hicho.

Wakili huyo alishtakiwa kwa makosa ya kuzuia haki itendeke kwa kuwashawishi mashahidi wa Mahakama hiyo kwa rushwa.

Alijisalimisha kwa mahakama ya ICC Novemba 2, 2020, baada ya hati ya kukamatwa kwake kutolewa Machi 10, 2015 kuhusiana na ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa Kenya.

Mahakama hiyo ilimshtaki Paul Gicheru na wengine wawili kwa kuingilia mfumo wa sheria na kuwashtumu kwa kuingilia mashahidi wa waendesha mashtaka katika kesi dhidi ya wanaodaiwa kuwa waandaaji na wafadhili wa ghasia za mwaka 2007.

Mahakama ya ICC inamshutumu Gicheru na wengine na kufanya njama ya kuwasiliana na mashahidi, kuwadanganya na kutumia njia za ufisadi kulikowachochea kujiondoa kwenye kesi hiyo.

Rais William Ruto na Rais aliyeondoka madarakani Uhuru Kenyatta walikuwa miongoni mwa watu sita walioshtakiwa na mahakama ya ICC kwa jukumu walilotekeleza kwenye ghasia za baada ya uchaguzi.

Baada ya miaka kadhaa, mwendesha mashtaka wa ICC alitupilia mbali kesi dhidi ya Kenyatta mwaka 2015, huku ya Ruto nayo ikifuata mkondo huo mwaka mmoja baadaye akilaumu kuingiliwa kwa mashahidi.

***BBC***



Mke wa waziri mkuu wa zamani wa Japan Shinzo Abe, Akie Abe (katikati), akiwa amebeba majivu ya mume wake wakati wa mazishi. **PICHA; MTANDAO**

## Marufuku yatolewa kutoka nje usiku Goma

**CONGO, DRC**

SERIKALI nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo imeondoa amri ya kutotoka nje usiku katika mji wa Goma ulioko mashariki mwa nchi hiyo, eneo ambalo mamlaka ya kijeshi iliweka amri hiyo kwa ajili ya kulinda usalama.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, mamlaka ya kijeshi mkoani Kivu Kaskazini iliondoa amri hiyo iliyodumu kwa zaidi ya mwaka moja kwa ajili ya kufuatilia hali ya usalama katika mkoa huo.

Amri hii iliyokosolewa na baadhi ya mashirika ya kiraia kwanza itafanya kazi katika mji wa Goma huku maeneo mengine katika jimbo hilo yakiendelea kuzingatia amri ya kutotoka nje usiku.

Baadhi ya raia wakiwamo wafanyabiashara za usiku, waendesha bodaboda, wenye migahawa pamoja na hoteli katika mji wa Goma walisema wameridhika na kuondolewa kwa hatua hiyo iliyosababisha kuporomoka kwa uchumi wao.

Ilielezwa kuwa licha ya kuwekwa kwa mkoa huu chini ya utawala wa kijeshi hadi sasa zaidi ya mwaka mmoja, mji wa Goma bado ni miongoni mwa miji isiyo na usalama mashariki mwa Congo.

Inasema kuna ongezeko la visa vya ukatili yakiwamo mauaji yanayotekelezwa na magenge ya watu wenye silaha pamoja na utekaji nyara watoto hali inayoongeza hofu kwa wananchi wanaovilaumu vyombo vya usalama kwa uzembe katika utendaji kazi wao jambo ambalo mara nyingi limekuwa likisababisha mvutano kati ya raia na serikali ya Congo.

Mashirika ya kiraia pamoja na wanaharakati wanaotetea demokrasia waliendelea kuitisha mgomo wa siku mbili kulalamikia ukosefu wa usalama katika mkoa wa kivu kaskazini.

Katika siku ya pili baadhi ya wananchi walisalia majumbani mwao kuitikia wito huo huku baadhi ya maduka na masoko yakiwa yamefungwa.

***DW***

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NAM ENTERPRISES LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **FORD RANGER** yenye usajili namba **T970 DQH**, CHASSIS NAMBA : **6FPPXXMJ2PK670432** na ENGINE NAMBA : **SA2LPKC70432.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/382340/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABSALOM GIDEON KITULO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2499/0068** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia TUSIIME SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/TAB/RB/381348/2022**

## KUPOTEA KADI YA GARI

**CHRISPIN JOHN MKUNGILWA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI **(ISUZU JOURNEY)** yenye namba za usajili **T152 DKV** Chasis Namba: **LR311J2556945** Engine Namba: **6BD1438590** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **MKB/RB/140/2022.**

## KUPOTEA KADI YA GARI

**ATUPAVYE SALON MGAYA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI **(ISUZU JOURNEY)** yenye namba za usajili **T391 DPK** Chasis Namba: **LR212J300183** Engine Namba: **68G1837452** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **MKB/RB/142/2022.**

## KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**ROBERT CASMIR MALLYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 446 BEW** yenye Chassis namba **MD6M14PKXG4A29730.** Engine namba **OK4AG4305156.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/382811/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RASHID ALLY SEMBO** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GAR I(ISUZU JOURNEY) yenye namba za usajili **T476 DRX** Chasis Namba: **LR332J3000303** Engine Namba: **6HE1667776** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **MKB/RB/141/2022.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA DODOMA LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 218 YA MWAKA 2021**

**YALED NHASA MASAMBI......................MUOMBAJI**

**VERIUS**

**VERONIKA FELIX NZINDO .................MJIBU MAOMBI**

**KWA: VERONIKA FELIX NZINDO
POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 28.09.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANAGALIZO:** - kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hayi ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe **26 ya mwezi wa Septemba,2022.**

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 138 OF 2022**

**In the matter of the Estate of the late LEVINA LAURENT TARIMO of Dodoma Municipality**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ESTER JOSEPH SWAI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN NO. 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above- named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **17 Day of 10,2022.**
**Dated at Dodoma this 27 day of 9, 2022.**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 137 OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PETER MWENDA STEPHEN of Dodoma Municipality**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY FLAVIANA SWARE KIJUU**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN NO. 369 OF 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **17 Day of 10,2022.**
**Dated at Dodoma this 27 day of 9, 2022.**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE
Kituo cha JUMUISHI mkoa DSM
Usimamizi wa mirathi Na. 1717/2022
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SWALEHE BAKARI KIMBOKO
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MOHAMED HAMIS KISENGO**

**TANGAZO**
**(kanuani ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowowte/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 mwezi 09 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 08 mwaka 2022

HAKIMU

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MOBETO, BABA LEVO BALAA ZITO

Na Mwandishi Wetu

MWANAMITINDO na mjasiriamali, Hamisa Mobeto, amepuuzia mbali madai ya Baba Levo kuwa, Diamond Platnumz anampatia fedha nyingi kwa ajili ya matunzo ya mtoto.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Baba Levo aliweka maoni hayo muda mchache tu baada ya kutoa ushauri mrefu kwa Ommy Dimpoz kumaliza tofauti zake na baba yake mzazi.

Ommy, aliweka wazi kwamba, hakuna mtu yeyote anayeweza kumuambia kitu kuhusu baba yake kwa kile alichosema mzee huyo alimtelekeza na Baba Levo alimtaka kumsaidia ili aondokane na umaskini.

Na baadaye Baba Levo alimtania Mobeto kwamba, naye asije akasema Diamond hamshughulikii mwanawe, jambo ambalo lilikanushwa vikali na kusema mwanawe anamtegemea yeye mwenyewe katika kila kitu na Diamond hajawahi kutoa hata senti.

"Kwako ushahidi tunao, tajiri anamwaga mahelaaaa," aliandika Baba Levo.

"Tajiri gani kwanza tuanzie hapo? Anazimwaga wapi huenda nikakusaidia tukaenda kuziokota," alijibu Mobeto.

"Basi mama, huenda kweli hatoi chochote," Baba Levo alitania tena.

## LULU AMSIFIA ZUCHU KWA UZURI WA ASILI




Na Mwandishi Wetu

MSANII Amber Lulu ameibuka na kumsifia nyota wa kike wa Bongo Fleva kutoka familia ya WCB, Zuhura Othman maarufu kama Zuchu kuwa ana uzuri wa asili.

Lulu ambaye awali alikuwa kama video Vixen kwenye nyimbo za wasanii wa Bongo Fleva kabla ya kujikita kwenye muziki wenyewe, amesema uzuri alionao Zuchu ni wa kuzaliwa nao.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram (Insta Story), Lulu aliandika kuwa amegundua Zuchu ni mzuri sana.

"Zuchu ana uzuri wa asili na hili halina ubishi wowote. Kitu kizuri lazima kisifiwe na huo ndio ukweli."

## DIAMOND: NIPO NJIANI KUOA

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya msemaji wa Klabu ya Yanga, Haji Manara, kutangaza kupitia Instagram yake kuwa ameongeza mke mwingine, msanii wa muziki wa Bongo Fleva, Nasib Abdul 'Diamond Platnumz', amesema kuwa na yeye yupo njiani kuoa.

Usiku wa jana Manara alifunga ndoa na kuongeza mke wa tatu baada ya miezi kadhaa nyuma kufunga ndoa na mwanamke wa pili.

Hii ni ndoa ya tatu kwa Manara baada ya mwaka mmoja nyuma kufunga ndoa ya kwanza na miezi mitano iliyopita alifunga ndoa na mwanamke mwingine.

Kupitia mahojiano aliyofanya na vyombo vya habari, Manara alithibitisha kuwa aliachana na mke wake wa kwanza, hivyo alibaki na mke mmoja ambaye alifunga naye ndoa miezi kadhaa nyuma.

Na Diamond, kupitia ukurasa wake wa Instagram alimpongeza Manara na kusema na yeye yupo njiani kuoa InshAllah.

"Nami niko njiano kuoa IshAllah," aliandika Diamond.

Diamond mkali wa Bongo Fleva tayari ana watoto wawili na mrembo Zarinah Hassan maarufu Zari The Boss Lady.

Pia, amezaa na Hamisa Mobeto mtoto mmoja wa kiume na Tanasha Donna kutoka Kenya ambaye naye amezaa naye mtoto mmoja wa kiume.

# KIPANGA: SIMBA KIPIMO SAHIHI KWETU KUWAVAA WATUNISIA CAF

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba leo usiku ikitarajia kucheza dhidi ya Kipanga FC kwenye mechi ya kirafiki itakayopigwa Uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Hamisi Hassan, amesema kwao ni fahari na faraja kucheza na timu hiyo kwani watapata kipimo sahihi cha kucheza mechi yao ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Club Africain kwa sababu zote ni timu bora Afrika.

Kocha huyo alisema kuwa anachoona ni kwamba Simba na Club Africain wapo kwenye levo moja, hivyo kitu watakachokipata kwenye mechi hiyo kitawasaidia sana kwa mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho.

"Simba ni timu nzuri na bora kwa sasa Afrika, iko kwenye nafasi ya 14, nadhani inaizidi hata hiyo Club Africain, yaani tuongee tu kama watu wa ufundi, tusiwe kama mashabiki, hii ni timu kubwa na imetuzidi kwa mbali sana huo ndiyo ukweli kwa hiyo wachezaji wetu hata ukiwaangalia kila mmoja anatamani kucheza mechi hii, kila mtu anatamani kucheza na Pape Sakho, Clatous Chama, Aishi Manula, Moses Phiri ili nao waweke historia," alisema kocha huyo.

Alisema analishukuru Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kwa kuwatayarishia mechi hiyo kubwa kwa ajili ya kujiandaa na mechi yao hiyo ambayo anasema itakuwa ngumu.

"Tayari tumeongea na wachezaji wetu, tumewaweka sawa kisaikolojia, tumewaambia kuwa mechi itakuwa na watu wengi na wanacheza na timu kubwa na kama wakiweza kuonyesha uwezo, basi wanaweza kufanya vema hata kwenye hiyo mechi kwa sababu Simba ina uwezo sawa na timu tunayocheza nayo, au inaizidi. Tunajua wenzetu wana wachezaji wazuri ambao unatakiwa uwe na tahadhari nao, ni wazoefu na rahisi kukuadhibu, hivyo sisi ni lazima tuwe na 'plan' (mpango) namba moja na ikishindikana twende namba mbili," alisema kocha msaidizi huyo.

Kipanga imeingia kwenye raundi ya kwanza ya michuano hiyo baada ya kuiondosha Al Hilal Wau ya Sudan kwa mikwaju ya penalti 4-3, kutokana na matokeo ya sare ya bao 1-1 ilizopata timu zote mbili zikicheza nyumbani na ugenini.

Kuelekea kwenye mechi hiyo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema kambi ipo shwari tofauti na mijadala inayoendelea kuwa hakuna utulivu.

Ahmed alisema wapo tayari kwa mechi hiyo ambayo itakuwa ya pili, huku akikanusha taarifa zinazozagaa kuwa hakuna maelewano baina ya baadhi ya wachezaji wa timu hiyo.

"Kilichotokea ni kwamba Dejan (Georgijevic) alimshutumu Okrah (Augustine) kuwa alikaa sehemu nzuri hakumpa pasi na hiyo ilitokea wakati wanafanyiwa mabadiliko, lakini yalisemwa yakaisha na hii ilitokea wakati damu inachemka na inatokea kwenye soka popote duniani, kwa hiyo niwatoe hofu wanachama na mashabiki wa Simba kuwa kambi ina utulivu," alisma Ahmed.




Balozi wa Promosheni ya 'Wakishua Twenzetu Qatar' kushuhudia Kombe la Dunia, Feisal Salum' Fei Toto', akizungumza na balozi mwenzake kwa njia ya mtandao, Aishi Manula, wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo inayoendeshwa na Kampuni ya Tigo na Kampuni ya Hisense, aliyeshika vipaza sauti ni Meneja Mawasiliano wa tiGO, Woinde Sishaeli. Kampeni hiyo inalenga kuwapeleka Qatar mashabiki 50 wa soka nchini kwenda kushuhudia fainali hizo wakilipiwa kila kitu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mmachinga amfunda Mayele Yanga

**Na Aam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Yanga, Mohamed Hussein 'Mmachinga', amesema amechoka kuona rekodi yake ya kuwa mfungaji bora wa muda wote anaendelea kuwa nayo, sasa anataka ivunjwe na mchezaji yeyote wa Ligi Kuu, huku akimtaka Fiston Mayele kuifanya kazi hiyo.

Mchezaji huyo ambaye ni kinara wa upachikaji mabao wa muda wote wa Ligi Kuu Tanzania Bara, akipachika mabao 26 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara (zamani Ligi Daraja la Kwanza) mwaka 1996, alisema anamtaka Mayele msimu huu avuke idadi hiyo ya mabao kwenye ligi ili avunje rekodi ambayo anaishikia mpaka sasa.

"Haiwezekani miaka yote rekodi niishikilie mimi tu, siyo vizuri na siyo vema kwenye soka ambalo linaendelea, rekodi hii inatakiwa ivunjwe, sasa wa kuivunja ni nani? Nataka wachezaji wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara wajitume ili waivunje, ila nina imani na Meyele, jitahidi na kuzidi kujituma, akijitahidi anaweza kuivunja msimu huu, nakumbuka huko nyuma Meddie Kagere alifikisha hadi mabao 23, angekuwa makini kidogo tu angeweza kuvunja," alisema mchezaji huyo wa zamani ambaye kwa sasa ni mmoja wa makocha wasaidizi wa Yanga Princess.

"Kwa kweli jinsi anavyocheza, anajua jinsi gani ya kujiweka kwenye sehemu nzuri, sisi wanamichezo tunasema kukaa kwenye njia za mipira na alivyoanza kwa kasi tofauti na msimu uliopita, anaweza aongeze juhudi," alisema.

Kuhusu mchezo kati ya Yanga na Al Hilal ya Sudan, alisema utakuwa ni mgumu, lakini ameitaka timu hiyo kuimaliza mechi hiyo nyumbani ili kujiweka kwenye mazingira mazuri kuelekea mchezo wa marudiano ugenini.

"Yanga inatakiwa mechi ya nyumbani lazima ishinde, mabao matatu kwenda mbele, mechi ni lazima iishe nyumbani, na hii hamasa ya mashabiki ni kweli wanatakiwa kuwa wengi kuleta hamasa ili wachezaji wafanye vizuri," alisema Mmachinga ambaye amewahi kuichezea Simba kwenye miaka yake ya mwisho kabla ya kutundika daluga.

Akiizungumzia Ligi Kuu Tanzania Bara, alisema kinachotakiwa kwa Yanga ni kukusanya pointi mapema kwani kila raundi zinavyozidi kwenda mbele zinazidi kuwa ngumu.

## Kombe la Azam Dar kuanza kesho

**Na Mwandishi Wetu**

MICHUANO ya Kombe la Azam Sports Federation kwa Mkoa wa Dar es Salaam, yenye lengo la kuendeleza vipaji vya soka nchini, inatarajiwa kuanza kesho katika Uwanja wa Karume.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Dar es Salaam, Ramadhan Missiru, alisema maandalizi yote kuelekea michuano hiyo yamekamilika na timu zipo tayari.

"Maandalizi yamekamilika kwa asilimia 99, timu zote zipo tayari kwa ajili ya michuano hiyo," alisema.

Missiru alizitaja timu ambazo zitashiriki michuano hiyo kuwa ni Global Weries, Huduma, Magereza, Eagle, Navy, Tandika United, Farwa na timu ya Wauza Matairi.

Katibu huyo alisema mchezo wa funguzi kesho utakuwa kati ya Global Weries dhidi ya Huduma huku Septemba 30, mwaka huu, timu za Magereza na Eagle zikitarajiwa kupambana katika Uwanja wa Karume.

Oktoba Mosi, timu ya Navy itacheza na Tandika United, Oktoba 2, mwaka huu, Farwa itachuana na Wauza Matairi.

## Singida Big Stars tayari kuivaa Azam

**Na Camila Bonanza, TUDARCo**

TIMU ya Singida Big Stars imewasili jijini Dar es Salaam na kuanza kujifua katika Uwanja wa Uhuru tayari kwa mchezo wao ujao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC utakaopigwa dimba la Azam Complex, Chamazi.

Msemaji wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, amesema wamejiandaa kupata ushindi baada ya kutofanya vizuri katika mechi mbili mfululizo dhidi ya Dodoma Jiji FC na Mbeya City, ambazo walitoka sare.

Alisema wachezaji wote waliosafiri nao wapo fiti kwa mchezo huo huku straika Meddie Kagere aliyekuwa katika majukumu na Timu ya Taifa ya Rwanda, akitarajiwa kujiunga na wenzake kabla ya mchezo huo.

Timu hizo zitakutana zikiwa na alama sawa (pointi nane) kila moja baada ya kushuka dimbani mara nne, lakini kwenye msimamo wa ligi hiyo, Azam ikishika nafasi ya nne juu ya Singida Big Stars kutokana na idadi kubwa ya mabao ya kufunga.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM KUTUA LIVERPOOL
KIUNGO wa kati wa England na Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, ambaye amehusishwa na uhamisho wa kwenda Liverpool, analengwa na Real Madrid na huenda wakamsajili msimu ujao wa uhamisho. ***(Marca)***

### MUDRYK AWANIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inafikiria kuwasilisha dau la pauni milioni 50 kumnunua winga wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### LEAO ANG'ANG'ANIWA MILAN
MKURUGENZI wa Ufundi wa AC Milan, Paulo Maldini, amesema mshambuliaji wa Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23, ambaye amehusishwa na kuhamia Chelsea, anajua mustakabali wake uko katika klabu hiyo ya Serie A licha ya matatizo ya uhamisho wa awali kuathiri mazungumzo ya kuongeza mkataba wake hapo San Siro. ***(Dello Sport)***

### DUMFRIES AWINDWA CHELSEA
CHELSEA wanapanga kuongeza ofa ya msimu wa majira ya joto waliyotoa kwa mlinzi wa Inter Milan na Uholanzi, Denzel Dumfries hadi euro milioni 50, lakini watakuwa tayari kumtoa kwa mkopo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, katika klabu hiyo ya Serie A kwa miezi sita iwapo mkataba huo utafanyika. ***(Corriere dello Sport)***

### DENZEL ATAKA TAJI INTER
MLINZI wa zamani wa PSV Eindhoven, Denzel Dumfries amesema ripoti kuwa anasakwa na Chelsea na Manchester United "kunanipendeza" lakini analenga kurejesha taji la Serie A akiwa na Inter. ***(De Telegraaf, Express)***

### MARTINEZ ATAKIWA UNITED
MANCHESTER United wanamfuatilia kwa karibu mlinda mlango wa Aston Villa na Argentina, Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 30. ***(Football Insider)***


### MILAN KUPELEKWA SOKONI
INTER Milan haijapiga hatua yoyote katika mazungumzo ya kuongezwa muda wa Milan Skriniar, ambaye mkataba wake unakamilika msimu ujao wa majira ya joto, kwa hiyo Paris St-Germain wanaweza kumnunua mlinzi huyo wa Slovakia mwenye umri wa miaka 27, katika kipindi cha uhamisho wa majira ya baridi Januari. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### DIAZ KURUDISHWA MADRID
REAL Madrid inapanga kumrejesha winga wa Hispania, Brahim Diaz mwenye umri wa miaka 23, ambaye zamani alikuwa Manchester City, kutoka kwa muda wa mkopo katika klabu ya AC Milan ili kuchukua nafasi ya Marco Asensio mwenye miaka 26, mkataba wake utakapokamilika msimu ujao. ***(Football Espana)***

### ESENSIO SAFI BARCA
MARCO Asensio tayari amesaini mkataba wa awali na wapinzani wa Real Madrid, Barcelona ambao utadumu kwa miaka minne kuanzia msimu ujao wa majira ya joto. ***(RAC1)***

### FERNANDEZ HATAKIWI LIVERPOOL
LIVERPOOL haijapinga uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Benfica na Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 21, ambaye ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 120 katika mkataba wake. ***(Liverpool Echo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI: NAPENDA ZAIDI KUCHEZA NA NEYMAR

●●● Tumefahamiana kwa muda mrefu, tangu Barca, lakini sasa nimekutana naye tena Paris na tuna furaha...

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi anatamani angecheza na Neymar kwa muda mrefu zaidi kule Barcelona, lakini amependa kuunganishwa tena na Mbrazil huyo pale Paris Saint-Germain.

Neymar na Messi walianzisha urafiki na uhusiano mkubwa uwanjani kwa miaka minne wakiwa pamoja kule Camp Nou.

Walikuwa sehemu ya timu ya Barca iliyoshinda mataji mawili ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, mataji matatu ya Copa del Rey na Ligi ya Mabingwa Ulaya, kati ya mataji mengine, kabla ya PSG kuvunja rekodi ya uhamisho wa dunia na kumsajili Neymar kwa euro milioni 222.

Licha ya kuingiza fedha nyingi, Barca walikumbwa na mdororo wa uchumi na klabu hiyo kushindwa kumpa Messi mkataba mpya mwaka jana.

"Mimi na Neymar, tumefahamiana kwa muda mrefu, tangu Barcelona," alisema Messi akiiambia TUDN.

"Ningependa tungecheza kwa muda mrefu zaidi Barcelona.

"Lakini sasa nimekutana naye tena Paris na tuna furaha kuwa pamoja. Ninapenda kucheza naye."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,034,9
MECHI KALI
CSKA MOSCOW
VERSUS
SOCHI
1 | 2.06
X | 3.44
2 | 3.10
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SOUTHGATE AWATETEA MAGUIRE, POPE



**LONDON, England**

KOCHA Gareth Southgate amekataa kuwalaumu Harry Maguire au Nick Pope baada ya makosa yao makubwa yao kusababisha sare ya mabao 3-3 dhidi ya Ujerumani kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa, Jumatatu.

Maguire beki wa Manchester United alizomewa na mashabiki jina lake liliposomwa na alifanya kosa la kumpasia mpira mpinzani wake, Jamal Musiala na kisha kumfanyia madhambi kwenye eneo la hatari na kusababisha penalti.

Ilkay Gundogan alifunga mkwaju huo wa penalti kabla ya Kai Havertz kufanya matokeo kuwa 2-0, lakini 'Simba Watatu' hao walirudi mchezoni na kuwa mbele kwa mabao 3-2, yakifungwa na Luke Shaw, Mason Mount na Harry Kane.

Hata hivyo, Nick Pope alifanya kosa lililomuwezesha Havertz kuuwahi mpira na kufunga bao lake la pili na la tatu kwa Ujerumani na hivyo mchezo kumalizika kwa sare hiyo.

Kuhusu kosa la penalti ya Maguire, Southgate alisema: "Ni vigumu kutofautisha upande mmoja na mwingine. Kupeana mpira ndio tatizo, lakini tazama, kama kundi wamekutana wiki hii. Kimekuwa kipindi kigumu wao, lakini wamecheza vizuri.

"Kwa kiasi, siku zote tunakabiliwa na shinikizo. Tulicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Ivory Coast Machi. Wiki hii tumejifunza kiasi kikubwa. Imebidi kupiga hatua mbele na kuja pamoja - itatunufaisha kwa muda mrefu."

Kuhusu Pope, alisema: "Ni makosa na bila shaka atakuwa anajilaumu, lakini timu inapaswa kuwa pamoja na tumefanya hivyo wiki nzima.

"Usiku wa leo (juzi), makosa kadhaa yametugharimu, lakini nitazingatia ukweli kwamba walicheza kwa ari kubwa na walionyesha imani ambayo hatujaonyesha katika michezo michache iliyopita. Nadhani umati uliona hivyo."

England haitacheza tena hadi mechi yao ya kwanza ya Kombe la Dunia dhidi ya Iran Novemba 21, mwaka huu.

# Araujo hatihati Kombe la Dunia

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA wamethibitisha kuwa Ronald Araujo atafanyiwa upasuaji wa jeraha la paja baadaye wiki hii, na anatarajiwa kukosa Kombe la Dunia mwaka huu nchini Qatar.

Beki huyo alipata tatizo katika mechi ya kirafiki ya Uruguay dhidi ya Iran na akarejea Katalunya kwa uchunguzi zaidi.

Na Barcelona walithibitisha Jumatatu kwamba jeraha hilo litahitaji upasuaji, na taarifa ilisema: "Mchezaji wa kikosi cha kwanza Ronald Araujo atafanyiwa upasuaji Jumatano (jana) kwenye mguu wake wa kulia. Operesheni hiyo itafanywa na Dk. Lasse Lempainen, chini ya uangalizi wa wahudumu wa afya wa klabu mjini Turku nchini Finland. Upasuaji utakapokamilika kutakuwa na taarifa nyingine ya matibabu.



"Majeraha hayo yalitokana na mchezaji aliyekuwa kwenye majukumu ya kimataifa wakati wa mchezo kati ya Iran na Uruguay ambapo alilazimika kutoka uwanjani baada ya dakika tano za mchezo."

Araujo amecheza mechi saba kwenye kikosi cha kwanza katika msimu wa sasa wa 2022/23.

Ripoti kutoka Hispania zinasisitiza kuwa Araujo anaweza kukosa kucheza kwa kipindi cha hadi miezi mitatu, na ingawa haikuwekwa wazi katika taarifa ya Barcelona, atakosa kuichezea Uruguay kwenye Kombe la Dunia.

## HABARI MICHEZO

905,195/-

# LORITA AVUNJA REKODI NNE MICHUANO KUOGELEA TAIFA

**Na Mwandishi Wetu**

MWOGELEAJI chipukizi wa Klabu ya FK Blue Marlins, Lorita Borega, amevunja rekodi nne katika mashindano ya wazi yaliyomalizika hivi karibuni kwenye Bwawa la Kuogelea la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) Masaki, Dar es Salaam.

Mbali ya kuvunja rekodi hizo, Lorita ambaye alishinda nafasi ya kwanza kwa waogeleaji wenye umri kuanzia miaka tisa na 10 katika mashindano hayo baada ya kukusanya jumla ya pointi 116, pia ameweza kushinda medali tano za dhahabu, moja ya fedha na kikombe baada ya kuwapiku waogeleaji wengine 16 katika mashindano hayo yaliyoandaliwa na Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA).

Akizungumza baada ya mashindano hayo kumalizika, Lorita alisema amejisikia faraja kubwa kuibuka mshindi wa jumla katika mashindano hayo huku ikiwa ni mara yake ya pili kushiriki.

"Mashindano yalikuwa magumu na kila muogeaji alikuwa anawania nafasi ya kwanza, namshukuru Mungu kwa mafanikio niliyopata na sasa nina wapa pongezi makocha wangu, wazazi wa Klabu ya FK Blue Marlins, waogeaji wenzangu na wazazi wangu kwa kunipa sapoti kubwa," alisema Lorita ambaye anasoma darasa la sita katika Shule ya DIS.



Mwogeleaji Lorita Borega akiwa ameshika kikombe cha ushindi wa jumla katika mashindano ya wazi ya Taifa huku akipongezwa na baba yake. **MPIGAPICHA WETU**

Mwogeleaji huyo alishinda medali kwenye shindano la mita 50 katika mtindo wa butterfly, mita 100 (butterfly), mita 50 (freestyle), mita 100 (Individual Medley) na mita 100 katika mtindo wa freestyle.

Pia alishinda medali ya fedha katika mtindo wa breaststroke mita 50. Lorita pia alivunja rekodi na kuweka mpaka katika staili ya butterfly ya mita 50 kwa kutumia muda wa sekunde 35.27 kuiondoa rekodi ya Sydney Hardeman aliyoiweka mwaka 2018 kwa kutumia muda wa sekunde 37.38.

Lorita pia alivunja rekodi katika staili ya butterfly kwenye mita 100 kwa kutumia muda mpya wa dakika 1.23.60 na kuiondoa rekodi ya Sydney aliyoiweka mwaka 2018 ya muda wa 1.24.24.

Matokeo hayo yanaonyesha kuwa Lorita alivunja rekodi ya mita 50 katika staili ya freestyle kwa kuweka muda wa sekunde 32.62 na kuifuta rekodi ya Crissa Dillip ya sekunde 32.72 na vile vile kuifuta rekodi nyingine ya Crissa ya dakika 1.11.62 kwa kutumia muda mpya wa dakika 1.11.60 katika mtindo wa freestyle. Crissa aliweka muda huo mwaka 2021.

## Mwamuzi pambano la Mandonga afungiwa

INATOKA UK. 32

meridhishwa na maamuzi yaliyotolewa na kamati ya utendaji ni maamuzi ambayo nimeyapokea kwa mikono miwili, ilikuwa bahati mbaya kwani nimechezesha mapambano mengi sijawahi kufanya kosa kama hilo," alisema Mkarafuu.

Alisema jambo hilo alikuwa analihitaji na kukiri kufanya kosa kwenye pambano hilo na kitu ambacho atajirekebisha.

Aliomba radhi mashabiki pamoja na wadau wa mchezo huo na kuahidi kuendelea kushirikiana nao bega kwa bega.

# CEO mpya aipa jeuri Yanga kuitoa Al Hilal

INATOKA UK. 32

atatusaidia kufikia malengo na Yanga kufika mbalimbali katika michuano ya Afrika.

"Kwa sasa tunakabiliwa na mchezo wa kimataifa, kwa uzoefu wake tunaimani tutapiga hatua katika mechi hizo na michuano ya Afrika ambayo Yanga tuna malengo makubwa," alisema Hersi.

Naye Mtine alisema anafurahi kufanya kazi Yanga kwa sababu ni klabu kubwa na atahakikisha kwa ushirikiano mkubwa wa uongozi watafikia malengo yanayotarajiwa.

Alisema ana uzoefu mkubwa katika utendaji na kufahamu soka la Afrika jambo ambalo litasaidia katika kuifikisha klabu hiyo katika malengo yanayotarajiwa.

"Nimefurahi kuja Tanzania na kufanya kazi Yanga katika klabu kubwa, ninaimani kwa ushirikiano na viongozi na sekta mbalimbali katika uongozi wa klabu hii, tutafikia malengo yanayotarajiwa kwa klabu kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa, ikiwamo kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Mtine.

Wakati huo huo, Yanga imetambulisha mfumo mpya wa website, App ambao utawasaidia wanachama na mashabiki kupata nafasi ya kujisajili, lakini pia kupata taarifa za klabu yao.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/10/22 | 17:00 | Coventry vs Middlesbrough | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 02. 01/10/22 | 17:00 | Fulham vs Newcastle | 3.04 | 3.39 | 2.27 |
| 03. 01/10/22 | 17:00 | Rotherham vs Wigan | 2.33 | 3.19 | 3.09 |
| 04. 01/10/22 | 17:15 | Getafe vs Valladolid | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 05. 01/10/22 | 18:00 | Strasbourg vs Rennes | 2.92 | 3.36 | 2.32 |
| 06. 01/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 07. 01/10/22 | 19:30 | Werder Bremen vs Borussia Monchengladbach | 2.58 | 3.57 | 2.48 |
| 08. 02/10/22 | 14:00 | Lorient vs Lille | 2.92 | 3.42 | 2.30 |
| 09. 02/10/22 | 14:00 | Stoke City vs Watford | 2.38 | 3.18 | 3.03 |
| 10. 02/10/22 | 15:00 | Espanyol vs Valencia | 2.73 | 3.22 | 2.58 |
| 11. 02/10/22 | 16:00 | AJ Auxerre vs Brest | 2.67 | 3.36 | 2.52 |
| 12. 02/10/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.47 | 3.36 | 2.72 |
| 13. 02/10/22 | 16:00 | Sampdoria vs AC Monza Brianz | 2.31 | 3.29 | 3.04 |
| 14. 02/10/22 | 16:30 | Hertha BSC vs Hoffenheim | 2.97 | 3.56 | 2.21 |
| 15. 02/10/22 | 17:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 16. 02/10/22 | 18:30 | Leeds vs Aston Villa | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 17. 02/10/22 | 19:30 | Girona vs Real Sociedad | 3.19 | 3.14 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 28/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 4158 | Cong Anh Nhan Dan vs PHU Dong FC | 1.23 | 5.09 | 10.77 |
| 13:00 | 1835 | QNK Quang Nam vs K. Khanh Hoa | 2.29 | 2.85 | 3.45 |
| 13:00 | 3890 | Binh Phuoc vs DAK Lak | 2.42 | 3.04 | 2.80 |
| 14:00 | 1321 | TP Can Tho vs PHO Hien FC | 3.82 | 2.70 | 2.14 |
| 15:00 | 1907 | Ural Yekaterinburg vs Torpedo Moscow | 1.78 | 3.35 | 4.14 |
| 15:00 | 3339 | Mjondalen 2 vs Tromso IL 2 | 2.17 | 4.62 | 2.36 |
| 16:00 | 1564 | FK Imt Novi Beograd vs FK Loznica | 1.25 | 5.20 | 11.00 |
| 16:00 | 1856 | FK Novi Sad vs Metalac | 4.12 | 3.29 | 1.81 |
| 16:00 | 2202 | FK Jedinstvo UB vs FK Radnicki Beograd | 1.80 | 3.19 | 4.31 |
| 16:00 | 3048 | Al-Jalil vs Alia Club | 1.27 | 4.91 | 9.42 |
| 16:00 | 4390 | CSM Jiul Petrosani vs FC Otelul Galati | 6.10 | 4.53 | 1.40 |
| 16:00 | 4400 | Huracan Reserve vs San Lorenzo de Almagro Res. | 1.80 | 3.48 | 3.87 |
| 16:00 | 4576 | FC Rad vs OFK Vrsac | 2.07 | 2.99 | 3.53 |
| 16:00 | 4888 | FCM Suceava vs UTA Arad | 7.65 | 4.80 | 1.31 |
| 16:00 | 5844 | Kuala Lumpur vs Sarawak | 1.60 | 3.88 | 4.61 |
| 16:30 | 2329 | Mes Shahr-e Babak vs Saipa Karadj | 1.73 | 3.08 | 5.08 |
| 16:30 | 2633 | ACS Unu Fotbal Club Gloria vs Unirea Slobozia | 4.50 | 3.65 | 1.71 |
| 16:30 | 2951 | NK Fuzinar Ravne vs NK Aluminij | 4.70 | 3.82 | 1.60 |
| 16:30 | 3492 | Scolar Resita vs CS Mioveni | 4.12 | 3.58 | 1.73 |
| 16:30 | 5702 | CS Ocna Mures vs CSM Slatina | 2.50 | 3.63 | 2.35 |
| 17:00 | 3611 | Gimnasia de la Plata Reserve vs CA Barracas Central Reserve | 1.44 | 4.22 | 5.89 |
| 17:00 | 3622 | Rosario Central Reserve vs Racing Club Reserve | 1.99 | 3.23 | 3.48 |
| 17:00 | 3907 | Kheybar Khorramabad FC vs Esteghlal Khuzestan | 1.81 | 2.94 | 4.80 |
| 17:30 | 1845 | FK Khimki vs Lokomotiv Moscow | 3.00 | 3.35 | 2.14 |
| 17:30 | 3612 | Gazovik Orenburg vs Dinamo Moscow | 3.28 | 3.38 | 2.01 |
| 17:30 | 3782 | Esteghlal Mollasani vs Arman Gohar Sirjan | 2.13 | 2.50 | 4.32 |
| 18:00 | 1042 | Hifk vs Ilves Tampere | 4.11 | 3.73 | 1.70 |
| 18:00 | 1278 | Inter Turku vs Haka | 2.14 | 3.34 | 3.01 |
| 18:00 | 3420 | FK Trajal vs Indjija | 3.55 | 3.00 | 2.13 |
| 18:00 | 5065 | Seinajoen JK vs KuPS Kuopio | 3.53 | 3.43 | 1.91 |
| 18:00 | 5659 | Lahti vs VPS Vaasa | 3.14 | 3.52 | 2.01 |
| 18:30 | 2280 | IFK Mariehamn vs AC Oulu | 1.84 | 3.62 | 3.57 |
| 18:30 | 2583 | Primeiro De Agosto vs Kuando Kubango FC | 1.33 | 4.42 | 8.05 |
| 18:45 | 3095 | ACS Viitorul Selimbar vs Petrolul Ploiesti | 3.34 | 3.14 | 2.07 |
| 20:00 | 3563 | TSV Steinbach II vs SC 1929 Waldgirmes | 4.90 | 4.90 | 1.49 |
| 20:00 | 3991 | CSKA Moscow vs Sochi | 2.06 | 3.44 | 3.10 |
| 20:00 | 4699 | FC Krasnodar vs Nizhny Novgorod | 1.55 | 4.01 | 4.89 |
| 20:00 | 5268 | 1. Hanauer FC 93 vs Bayern Alzenau | 2.00 | 4.10 | 3.00 |
| 20:00 | 5455 | Carl Zeiss Jena vs Energie Cottbus | 2.18 | 3.45 | 2.86 |
| 20:00 | 5718 | 1. SC Feucht vs DJK Gebenbach | 2.44 | 3.70 | 2.50 |
| 20:11 | 1698 | KP Polonia Warsaw vs KKS 1925 Kalisz | 1.82 | 3.39 | 3.93 |
| 20:30 | 3973 | Breitenrain vs Juventus Zurich | 1.38 | 4.73 | 6.11 |
| 21:00 | 4434 | Deportivo La Coruna vs CF Talavera De La Reina | 1.26 | 5.32 | 8.46 |
| 21:05 | 1150 | Chelsea W vs West Ham W | 1.03 | 10.73 | 25.36 |
| 21:15 | 2299 | Academia Cantolao vs FC Carlos Stein | 2.01 | 3.35 | 3.30 |
| 21:30 | 5395 | CS Afumati vs Rapid Bucuresti | 10.79 | 6.08 | 1.19 |
| 21:45 | 2537 | Gosport Borough vs Poole Town | 2.19 | 3.45 | 3.00 |
| 22:00 | 1531 | Independiente vs Talleres | 2.37 | 2.95 | 2.95 |
| 23:00 | 5831 | Deportes Quindio vs Atletico Huila | 1.56 | 3.67 | 5.34 |
| 23:30 | 2018 | Sport Huancayo vs Deportivo Municipal | 1.33 | 4.71 | 7.26 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Septemba 28, 2022

Nipashe




UKURASA 30

## Southgate awatetea Maguire, Pope

HUYU HAPA...




Rais wa Yanga, Mhandisi Hesri Said (kulia), akimtambulisha Mtendaji Mkuu (CEO) mpya wa klabu hiyo, Mzambia Andre Mtine, jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# CEO MPYA AIPA JEURI YANGA KUITOA AL HILAL

## ●●● Aanika 'madini' yote ya Ibenge, pia ana taaluma ya ukocha huku...

**Na Saada Akida**

ZIKIWA zimebaki takriban siku 11 kabla ya Yanga kuikaribisha Al Hilal kwenye mechi ya kwanza ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa klabu hiyo umemtambulisha rasmi Mtendaji wao Mkuu (CEO), Mzambia Andre Mtine, ambaye wameingia naye mkataba wa miaka miwili akichukuwa nafasi ya Senzo Mbatha aliyemaliza 'kandarasi' yake hivi karibuni.

Mtine amewahi kufanya kazi katika klabu mbalimbali hapa Afrika ikiwamo Zesco ya kwao Zambia, TP Mazembe ya DR Congo na kuhudumu katika Shirikisho la Soka Afrika (CAF) katika kitengo cha fedha.

Yanga sasa inajivunia uzoefu CEO huyo ambaye anamjua vema Kocha Mkuu wa Al Hilal ya Sudan wa sasa, Florent Ibenge, tangu akiwa anafanya kazi nchini Congo kabla ya wote kuondoka.

Tayari imeelezwa Mtine ameanza kushusha hesabu zote zitakazoisaidia Yanga kuwashangaza matajiri hao wa Sudan, ikiwamo mikakati ya kocha wa timu hiyo, Ibenge ambaye ni raia wa DR Congo.

Kutokana na uzoefu na kufahamu uwezo wa Mtine katika soka, mabosi wa Yanga wameshaanza kuchukua tahadhari na hesabu zote na CEO huyo kuzingatia mechi mbili ili kupata matokeo chanya dhidi ya Al Hilal.

Yanga itaanzia nyumbani dhidi ya Al Hilal Oktoba 8, mwaka huu, kabla ya timu hizo kurudiana baada ya wiki moja nchini Sudan, na mshindi wa jumla atatinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Yanga, Hesri Said, alisema kwa uzoefu wa Mtine, anaamini timu yao itafikia malengo makubwa katika mipango yao kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika wakianza dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Alisema baada ya mchakato wa kupitia maombi ya waliomba kazi, Mtine amekidhi vigezo kwa sababu ya kuhudumu kufanya kazi sehemu mbalimbali katika soka la Afrika.

"Tumempa mkataba wa miaka miwili na kumtambulisha Mtine, tunaimani na uzoefu wake kwa kuhudumu katika nchini mbalimbali za soka ikiwamo CAF,

INAENDELEA UK. 31

# Mwamuzi pambano la Mandonga afungiwa

**Na Shufaa Lyimo**

KAMATI ya Utendaji ya Chama cha Waamuzi wa Ngumi za Kulipwa Tanzania, imemfungia mwamuzi, Habibu Mkarafuu, kutojihusisha kuchezesha mapambano kwa kipindi cha miezi miwili.

Mkarafuu amekumbwa na rungu hilo la kufungiwa kutokana na kufanya makosa ya wazi katika pambano alilochezesha Jumamosi iliyopita kati ya bondia Karimu Mandonga na Salum Abeid kutoka (Tanga), ambalo lilifanyika mkoani Mtwara.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Waamuzi wa Ngumi Tanzania, Emanuel Mlundwa, alisema baada ya kamati hiyo kukutana, imetoa maamuzi hayo mpaka hapo atakapopata kozi ya miezi miwili.

Alisema kamati imebaini kuwa waamuzi wengi hapa nchini hawajapitia kozi na semina ya kuwasaidia kuzifahamu vema sheria za mchezo huo.

"Kamati ya Utendaji imemfungia Mwenyekiti wa Chama cha Waamuzi, Habib Mkarafuu baada ya kubainika kufanya makosa ya wazi katika pambano alilolichezesha Septemba 24, mwaka huu mkoani Mtwara kati ya bondia Karim Mandonga na Salum Abeid ili iwe fundisho kwa wengine," alisema Mlundwa.

Katibu huyo alisema wameamua kuchukua maamuzi hayo haraka kwani makosa hayo yanaharibu taswira ya mchezo wa ngumi hapa nchini.

Alisema pambano ambalo litafanyika Septemba 30, mwaka huu jijini Dar es Salaam litachezeshwa na mwamuzi Antony Ruta, ambaye atachukua nafasi ya Mkarafuu.

Kwa upande wa Mkarafuu, alisema ameridhika na maamuzi yaliyotolewa na kamati hiyo.

"Ni-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >